ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID - SPIKA

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria

		na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo,

		Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais
19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa

		na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake
28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini

30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe. Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil	-	Uteuzi wa Rais
33. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
34. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
35. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
36. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
37. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
38. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
39. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
40. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
42. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
43. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
44. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
45. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
46. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
47. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
48. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
49. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini

50. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo

51. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani

52. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando

53. Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu

54. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni

55. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile

56. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae

57. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini

58. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini

59. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake

60. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole

61. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani

62. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake

63. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake

64. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani

65. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani

66. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni

67. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde

68. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

69. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni

70. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake

71. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
72. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
73. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
75. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
76. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
77. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
78. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
79. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
80. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
82. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
85. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
86. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Sita - Tarehe 14 Februari, 2018

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Mgeni Hassan Juma) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Omar Seif Abeid (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuweka Hati Mezani ya Hotuba ya Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2017/2018 Mheshimiwa naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 43

Chuo Cha Mafunzo na Urekebishaji Tabia za Watoto

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Chuo cha Mafunzo kipo katika harakati za ujenzi wa jengo la ghorofa moja kwa ajili ya urekebishaji tabia kwa wanafunzi na watoto, fedha ambazo zinatokana na Serikali na kwasababu hadi kufikia mwezi wa Mei, 2017 jengo hilo limeshafikia hatua ya kusimamishwa nguzo za ghorofa.

a) Je, gharama halisi za ujenzi huo ni kiasi gani na ni kiasi gani cha fedha kinahitajika hadi kukamilika kwake.

b) Je, ujenzi huo utachukuwa muda gani na sasa hivi umefikia hatua gani.

(c) Je, baada ya kukamilika ujenzi huo ni wanafunzi na watoto wangapi watakao hudumiwa katika jengo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake Nam. 43 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Chuo cha Urekebishaji Wanafunzi Watoto ambao unaendelea huko Hanyegwamchana ulianza mwaka 2016/2017 ambapo kwa mwaka wa Fedha 2016/2017 jumla ya shilingi 250,000,000 zilipangwa kutumika kwa ajili ya ujenzi wa msingi wa jengo hilo. Jumla ya shilingi 239,000,000 zilitumika kwa ujenzi wa msingi. Na kwa mwaka wa Fedha 2017/2018, jumla ya shilingi 600,000,000 ziliidhinishwa katika mradi kwa ajili ya ujenzi wa matofali, kuweka zege ya ghorofa pamoja na kuezeka. Lakini hadi kufikia Disemba 2017, jumla Fedha ya shilingi 371,100,000 sawa na asilimia 62 zimepatikana. Gharama halisi za ujenzi huo hadi kukamilika kwake inatarajiwa kuwa ni shilingi 2,300,000,000 na kwa sasa ujenzi unaendelea na hatua ya kuweka zege ya ghorofa.

b) Ujenzi huu unatarajiwa kukamilika katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2016/2017 hadi 2018/2019, ili jengo hilo liweze kutumika.

c) Baada ya kukamilika kwa ujenzi huo, jengo hilo litakuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi 200 ambapo watahudumiwa kwa viwango vya kitaifa na kimataifa Mhe. Naibu Spika, ahsante.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri wa Serikali, ambapo imetenga kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya ujenzi huo ambao utahudumia watoto wanaokinzana na tabia, ambao umefikia kiwango cha kuridhisha lakini nilikuwa swali dogo tu la nyongeza nililokuwa nikitaka nifahamu.

a) Je baada ya kukamilika kwa ujenzi huu wa kituo hichi cha Hanyegwamchana. Wizara ina mpango gani wa kujengo kama lile kwa Pemba ambapo wapo baadhi ya vijana wenye tabia kama hii inayofanana na wa hapa Unguja.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ukweli ni kwamba katika mikakati na mipango mbalimbali ambayo yakuendeleza kuimarisha majengo pamoja na majengo mengine mapya na yale ambayo yamechakaa sana, Serikali kupitia Kikosi chetu cha Mafunzo kimekusudia kufanya mambo mengi katika kutayarisha mazingira kwa wapiganaji wetu kwa Unguja na Pemba. Lakini kutokana na hali ya upatikanaji Fedha.

Mhe. Naibu Spika, kwa sasa katika maeneo ya Pemba tunaendelea na ujenzi wa Mahanga pamoja na ukarabati wa majengo ambayo yamechakaa sana kutokana na hali ya uhalisia wake. Lakini, naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba kwa sasa tunaendelea na ujenzi huu katika jengo hilo la Hanyegwamchana na pale utakapokamilika, basi serikali haitosita kuona kwamba inaelekeza nguvu katika upande wa pili wa Kisiwa cha Pemba.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa ruhusa ya kuuliza swali dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza lenye kifungu (a) na (b). Kwanza, naipongeza wizara kwa kuweza kuhakikisha inajenga majengo mazuri ya kuweza kuweka wanafunzi watukutu. Mhe. Naibu Spika, kama sikosei Mhe. Waziri juzi katika majibu yake alijibu kwamba wizara yake ina mafundi wa vikosi.

a) Mhe. Naibu Spika, nataka kujuwa hili jengo wanalojenga la ghorofa sasa ni mafundi gani wanaowatumia kujenga jengo hili.
b) Ni *contractor* na mshauri elekezi alowekwa katika ujenzi wa jengo hilo, ili kuhakikisha jengo lile litakuwa salama kwa wanafunzi hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, nikweli naomba nikiri katika majibu yangu ambayo nimeyatowa jana ni kweli nilisema kwamba, mafundi

tulionao katika mafundi wetu miongoni mwao wengi wao ni wale ambao tumewakuza kwa kupitia shughuli zao ufundi wao wa asili ambao wametoka na huko na katika maeneo mengine. Lakini hatahivyo, nitowe majibu kwamba ujenzi huu unaoendelea unajengwa au unaendeshwa na maaskari wetu ambao ni mafundi kutoka vikosini kama ambavyo nimejibu jana.

Mhe. Naibu Spika, katika ujenzi huu katika mafundi wetu hao ni kwamba hushirikiana na wataalamu kama vile ambavyo wametaka kujuwa wataalamu elekezi na kwa sasa hivi kwa jengo hilo linae mshauri elekezi ambae ni *engineer* ambae anatoka katika Kampuni moja inaitwa *Sailara Building Construction* ambayo huyu ni mzawa wa hapa hapa nchini. Hivyo, naomba kwamba nimwambie tu Mhe. Mwakilishi kwamba ujenzi unaoendelea kujengwa uko imara, na unazingatia vigezo vyote katika ufundi au katika ujenzi wa ghorofa na aondoe hofu kwamba hakuna madhara ambayo tunatarajia yatatokea katika utaalamu huwo unaoendelea.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nami kunipa fursa hii kuuliza swali la nyongeza. Lakini, kabla sijauliza swali la nyongeza niwapongeze Chuo cha Mafunzo Pemba kwa juhudi yao kubwa walionesha kujenga ofisi yao kubwa katika sehemu yao pale Pemba kwa gharama zao wenyewe na iliyo nzuri tena ya kisasa sana nawapongeza sana. Mhe. Naibu Spika, baada ya pongezi hizi namuomba nimuulize swali la nyongeza Mhe. Waziri kama ifuatavyo:-

Pamoja na kuwa chuo au wizara ina mpango wa kujenga majengo na pia ambavyo kuwa Pemba kuna jengo kama hilo ambalo kuwa wanalizungumza nalo linakuwa na siku nyingi halijaweza kufanyiwa ukarabati mkubwa sana ipasavyo. Vilevile, kwa kuwa Chuo cha Mafunzo niliweza kukitembelea karibuni nikaona kero ambayo kuwa inawasumbua wanafunzi wa kule.

Je, ni lini kero hii ya kuweza kupatiwa sehemu ya kujifunzia ya kuweka charahani, kwa ajili ya wanafunzi walioko kule kama vile amali hizi zinazotolewa hapa Unguja, ni lini mtaweza kuweka sehemu ya kujifunza wanafunzi eneo la kupata huu ushoni katika Chuo cha Mafunzo Pemba ambao kwa sasa hakuna ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali la nyonge kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, ni kweli katika uasilia moja katika miongoni mwa majukumu wa Chuo cha Mafunzo ni kufundisha wanafunzi pale wanapoingia katika wanapokinzana na sheria. Lakini kutokana na hali ziliopo katika Magereza yetu, kwahiyo ni dhahiri kwamba baadhi ya maeneo ni kwamba baadhi ya huduma au baadhi ya vitendea kazi vya kuwafundishia wanafunzi hao vimekuwa ni pungufu sana ukilinganisha na baadhi ya maeneo.

Kwahivyo, nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba ushauri wake tutauchukuwa na tutaufanyia kazi kwa kadri hali itakavyokuwa ikiruhusu ndio hivyo hivyo tutaendelea kutowa huduma kazi kama hizo ambazo ameziona katika maeneo ya hapa Unguja na huko Pemba, kwa kuwa serikali haina lengo la kuwanyima fursa wanafunzi basi ni juhudi mbalimbali tutazichukuwa, ili kuona kwamba kila eneo wafungwa wanapata haki au wanapata yale mahitaji ambayo wanahitaji wakiweko Chuo cha Mafunzo, ili kusudi baada ya kutoka waende wakawe raia wema huko nchini au katika jamii.

Nam. 17

Uimarishaji wa Vyanzo vya Mapato ya Utalii na Maeneo ya Historia

Mhe. Suleiman Sarahani Said - Aliuliza:

Maeneo mengi ya kitalii na kihistoria inaonekana haujawekwa umakini wa kukusanya mapato na kuyatilia mkazo maeneo ambayo hayajapata umaarufu na badala yake tumebakia katika maeneo maarufu tu.

a) Je, katika vyanzo vya utalii na maeneo ya historia ambayo wanakwenda wageni na wenyeji kutembelea, kuna mabuku ya wageni na risiti za malipo zinazotambulika na serikali.

b) Sekta ya utalii imejikita zaidi kwa vyanzo vya mapato katika mahoteli, lakini katika sekta ya utamaduni haionekani kuwa na vyanzo vya mapato, kwanini sekta hii ya utamaduni haikuboreshwa kimapato.

c) Ni TV gani ambazo zinarusha matangazo ya kipindi maalum cha utalii wetu Zanzibar, ili kuonesha vyanzo vyetu vya utalii na maeneo ya kihistoria Unguja na Pemba kwa lengo la kuitangaza Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahani Said swali lake Nam. 17 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Katika maeneo ya utalii yanayotembelwa na wageni na wenyeji ambayo yanaratibiwa na serikali, kuna utaratibu

maalum wa kurikodi wageni waliotembelea eneo hilo, ili kujuwa takwimu zake. Na wageni wote wanaohudumiwa katika maeneo hayo hupatiwa risiti zinazotambuliwa na serikali.

b) Mhe. Naibu Spika, Sekta ya utamaduni imeboreshwa sana kimapato na kwa mwaka uliopita ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi milioni 120 kwa mwaka, na imeweza kukusanya jumla ya shilingi milioni 100, ni sawa na shilingi milioni 10, kwa mwezi. Vyanzo hivyo vinatokana na vibali, vya muziki, wasanii, wanaokuja ndani pamoja na matamasha yanayofanyika Zanzibar.

c) Serikali kupitia Kamisheni ya Utalii imekuwa na utaratibu wa kuandaa vipindi mbalimbali vya utalii vyenye nia ya kuwaelimisha na kuwashajihisha wananchi kushiriki katika sekta ya utalii kwa kuekeza, kuzalisha, kuhudumia au kuwa mtembeaji kwa kutumia redio na televisheni. Kamisheni imetumia *ZBC TV* na *ZCTV* kurushia vipindi hivyo kwa upande wa Zanzibar na *TBC* ya Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Spika, nakiri kwamba kasi ya utayarishaji wa urushaji wa vipindi kwa njia ya televisheni imekuwa ni ndogo kutokana na gharama za utayarishaji na urushaji wa matangazo hayo. Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Sarahani Said: Nashkuru Mhe. Naibu Spika pamoja na Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini nataka nimuulize katika swali langu moja lenye (a) na (b). Katika eneo la Pemba kuna maeneo mengi sana ambayo tunaita labda maeneo tunaita maeneo ya kumbukumbu au yale ambayo yalikaliwa zamani katika sehemu za utalii kama vile Mkamandume, Kaburi ya Mwanamwari, Msikiti Chooko na mengine.

a) Je, yuko mtu angalau mmoja katika maeneo ya kumbu kumbu aliyewekwa pale kwa ajili ya kukusanya mapato au angalau tu kuhifadhi yale yale mazingira.

b) Ni kwamba katika msitu wa Ngezi barabara yetu inayokata pale inakuwa haina geti la kuweza kumjuwa mtu huyu anaingia kwenye msitu au ana kitu gani. Je, serikali ina mpango wa kubadilisha njia ambayo isipitie kwenye msitu kwa vile anaekuwa anaenda kwenye msitu ndo aweze kulipa aliyekuwa hawezi kwenda apite njia nyengine

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye vipengele (a) na (b) vyote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, katika maeneo yote yale ambayo wanatembelea wageni wapo wafanyakazi wetu ambao wanahudumia wakati wanapokuja wageni kwa upande wa Pemba. Lakini inategemea na wamda ambao Mhe. Mwakilishi kasema alikwenda lakini hakukuta mfanyakazi inategemea na muda ambao amekwenda yeye ukizingatia kwamba wafanyakazi wetu wanaishi maeneo ya mbali sana na hali halisi ya mazingira yetu ya Pemba kama yalivyo. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba wafanyakazi hawa wapo na wanatowa huduma hizi kama vile sehemu nyengine za Unguja.

(b) Ni kweli kwamba pale Ngezi hapana geti ambalo linaonyesha uingiaji wa sehemu ile ya msitu ama wanaopita njia kwa kawaida. Lakini pale wapona wafanyakazi wetu, hasa ni wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na unapokwenda pale lazima usimame pale

kwa yule ambaye anaingia kwenye msitu ule na kupata maelezo na kutembezwa katika msitu ule. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf: *Bismilahi Rahman Rahim*. Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali kwa Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo nitaomba nimuulize swali lenye kifungu (a) na (b).

a) Kwakuwa, nchi yetu tunategemea sana palo la utalii na uchumi wa utalii na vilevile nchi nyingi sana katika sehemu zote za fukwe na za utalii wameweka polisi maalum, ambao wanazunguruka kuweza kuimarisha ulinzi wa watalii, na hapa kwetu Zanzibar kushaanza kuashiria kwa vitu vidogo waporaji wa kamera, simu na *hand bags* na vitu vyengine kwa watalii. Ni lini sasa Wizara yake itaunda au itapeleka Polisi maalum kwenye maeneo yote ya kitalii ya Zanzibar, ili kuimarisha ulinzi kwa ajili ya watalii na wananchi kwa jumla.

b) Kwakuwa utalii Zanzibar ndio kila kitu na barabara zetu zote zinazoingia kwenye mahotali yetu Zanzibar hii ni mbovu, gari ya chini haiwezi kufika kwenye maeneo lazima itagonga, itavunjika na watu wengine hawawezi kwenda. Ni lini sasa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo itatuhakikishia njia zile za kuingia kwenye mahoteli zinajengwa kwa kiwango cha kifusi au lami.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwalishi swali lake lenye vipengele (a) na (b) yote kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba katika maeneo yetu ya utalii hasa ya kihistoria kwamba hapana askari maalum pengine wa

kudumisha usalama kwa wageni ambao wanakwenda pale. Lakini kuna vituo mbalimbali katika barabara ambazo wanapita wageni wetu kuna askari polisi na kuelekea katika maeneo yale.

Aidha, Mhe. Naibu Spika, naomba nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba tunauchukua ushauri wake na tutaweka askari hawa katika vituo vyetu vyote ambavyo wanatembelea wageni hawa ili kuona kwamba usalama unapatikana katika maeneo yale ya kiutalii.

Mhe. Naibu Spika, juzi swali hili nimelijibu linalohusu barabara katika maeneo yetu ya kiutalii hasa kwa upande wa kule Pemba. Lakini, njia zetu kwa upande wa Unguja ziko sawa kwa yale maeneo ambayo wanakwenda wageni wetu. Hatahivyo, isitoshe kama ni hivyo tutashirikiana na wizara husika wanaotengeneza barabara, ili tuone kwamba maeneo yote yale yameboreshwa na yanasikika kwa haraka kwa ajili ya wageni wetu.

Mhe. Suleima Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nashkuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuuliza suala dogo la nyongeza. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini Mhe. Waziri katika majibu yako umesema kwamba katika maeneo yale ya utalii ya historia kuna wafanyakazi wanaotoka Wizarani, lakini kutokana na geography ya Pemba wafanyakazi wale huwa muda mwengine hawapaswi kufika kule kutokana na masafa wanayokaa.

Je, huoni upo umuhimu wa kuwatafuta wakaazi wa pale katika maeneo husika ili kudhibiti mapato yale kwa wale watalii wanaoingia kinyemela?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nakiri kwamba ipo haja na kuna umuhimu mkubwa wa kuwatafuta wakaazi wa maeneo ya kihistoria, ili kuona wageni wanapokwenda pale kwa bahati mbaya kama mfanyakazi wetu ameshaondoka katika maeneo yale. Lakini naomba nimueleze Mhe. Mwakilishi kwamba maeneo yote ambayo yapo shamba hasa kwa upande wa Pemba wapo watu wa vijiji ambao wanawakilisha wafanyakazi wetu na wanapokuja wageni wanawahudumia au wanatoa taarifa siku ya pili kwa wafanyakazi wetu.

Nam. 41

Nafasi za Ajira Katika Sekta ya Afya Pemba

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza:

Kwakuwa, Wizara ya Afya imeshawaajiri vijana ambao walifanya usaili kwa upande wa Unguja na Pemba, lakini hadi leo zoezi la kuwaajiri vijana hao kwa upande wa Pemba linaendelea taratibu sana pamoja na kwamba kuna upungufu mkubwa wa wafanyakazi katika sekta hiyo ya Afya kwa upande wa Pemba, ambapo kwenye uwekaji wa jiwe la msingi wa kituo cha Afya cha Sizini kwenye sherehe za kutimiza miaka 54 ya Mapinduzi ya Zanzibar kwenye hotuba ya kitaalamu ilisema kwamba kitahitaji wafanyakazi 14 wenye fani tafauti.

(a) Je, ni lini serikali itakamilisha utaratibu wa ajira kwa vijana hao.

(b) Je, ni idadi gani ya vijana ambao wanatarajiwa kuajiriwa kwa Pemba mara hii.

(c) Je, ni lini serikali itazirejesha nafasi za ajira 25 ambazo zilifutwa kwa upande wa Pemba mwaka jana.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mwakilishi swali lake Nam 41 lenye vipengele (a), (b) kwa na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, uajiri kwa vijana walioomba nafasi za kazi Pemba unaendelea kwa mujibu wa taratibu za uajiri na hadi ifikiapo Mwezi Machi 2018 tunategemea tuwe tumeshawaajiri vijana 47 na kuwapanga katika vituo mbalimbali vya afya kikiwemo kituo cha Sizini.

Pia jumla ya wafanyakazi 78 wa kada mbalimbali ambao wamo katika mchakato wa kukamilisha taratibu za uajiri, tumepanga kuwaajiri kisiwani Pemba kwa lengo la kujaza nafasi wazi yaani zilizoachwa na waliostaafu pamoja na waliofariki duinia pamoja na zile nafasi 25 za ajira zilizositishwa mwaka 2017.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba nipatiwe jibu dogo tu la swali langu la nyongeza linalohusiana na hao vijana 25 ambao ajira zao zilisitishwa.

Mhe. Naibu Spika, vipi utaratibu wa vijana wale, ili kuweza angalau kuwapatia kwasababu walishafikia hatua ya mwisho ya uajiri na mambo mengine. Wizara ina mpango gani angalau wa kuwachukuwa wengine japo kama itakuwa wote haiwezekani, basi kuwapunguza kidogo kidogo kuwarejesha.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, vijana wale 25 ambao walisitishwa kwa utaratibu kwa usalama utaratibu wa kuwarudisha vijana wale kwa bahati nzuri walipewa taarifa ya usitishwaji wao na walitakiwa kuomba tena. Sasa kila ambaye alijitokeza kuomba ataingia katika mkumbo huu, isipokuwa sio rahisi kumchukua tu hivi hivi kwa vile utaratibu mzima ulisimamishwa kwa mujibu wa usalama wa nchi yetu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri naomba nivitaje vituo hivi vilioko Pemba usikilize kwa utaratibu.

Jadida, Tungamaa, Makundeni, Mtambile, Junguni, Kangani, Vumba, Chwale, Mzambarauni, Kambini, Shamiani, Vundo, Kiongoni, Wambaa, Wete, Kisiwani, Kojani, Uwondo, Kengeja, Bogoa, Junguni, Ukutani, Mwambe, Kiuyu, Makondeni, Tasini, Shambani, Shidi vituo hivi vyote karibu 30 nilivyovitaja hapa vina ukosefu wa madaktari, ishirini na tano hawa watatosha wapi. Na lini atavitemebelea vituo hivyo nilivyovitaja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kam ifutavyo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri wa Afya, kama unaweza kujibu ruhusa na kama huna majibu kwa sasa, basi usilijibu kwasababu halitokani na swali la msingi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nilijibu. Vituo vyote alivyovitaja pamoja na vyengine ambavyo hukujaaliwa kuvitaja ambavyo vina upungufu wa wataalam yaani madaktari, vyote vimepangwa kuongezwa madaktari na wengine kuwekewa madaktari katika uajiri huu wa vijana 78 ambao tunategemea kuwaajiri wakati wowote kuanzia sasa. Na vijana hawa 78 ukijumlisha na vijana wale wa mwanzo 47 ina maana tutapata vijana tutakaowaajiri kama 125, ambao

tunahisi watakidhi kidogo watapunguza changamoto za utendaji wa madaktari katika vituo mbalimbali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, vituo ambavyo alivyonitajia Mhe. Mwakilishi natarajia kuvitembelea rasmi baada ya kumaliza likizo yangu ambapo sasa hivi nina likizo, nategemea kufanya ziara rasmi na nitahakikisha vituo ambavyo amevitaja nitavitembelea. *(Makofi)*

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Kwakweli, nina matumaini miongoni mwa vituo ambavyo vina upungufu mkubwa wa wafanyakai wa kada hii ya afya ni kituo cha Mfenesini na Chuini.

Je, Mhe. Naibu Waziri anatuahidi vipi katika vituo hivyo nao watapata wafanyakazi hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kama nimemfahamu maana *echo* ilikuwa inasumbua sikuipata vizuri maneno yake. Lakini Mhe. Naibu Spika, naomba aridhike Mhe. Mwakilishi kwamba kama tulivyopanga hapa 125 tunawaajiri Pemba, basi huku Unguja sikueleza tu ni wangapi, lakini wapo ambao wataajiriwa pia kwa upande wa Unguja na wanaendelea kuajiriwa.

Kwahivyo, naomba kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba katika tutakaowanga katika vituo tumepanga vituo vyote tuvifanyie utafiri ambacho kimepungua, ambacho hakikidhi madaktari waliopo na wataalam wengine basi tuweke nguvu kwa kuongeza, na wapo wengine tutawatia uhamisho katika vituo ambavyo tunahisi wapo wawili au zaidi ya wawili, ili kukidhi katika vituo ambavyo vina mapungufu. Mhe. Naibu Spika, naomba uridhike kwamba tutafanya kadiri iwezekanavyo

kuhakikisha kwamba huduma bora zinapatikana kwa wananchi katika vituo vyetu vya afya.

Nam. 23

Ujenzi wa Barabara ya Mwakaje - Mwachelale Hadi Bumbwini

Mhe. Machano Othman Said - Aliuliza:

Katika kuimarisha maisha ya wakulima hasa vijijini, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar walianzisha ujenzi wa barabara na masoko kupitia mradi wa MIVARF. Hatahivyo, kwa bahati mbaya barabara hizo zimejengwa chini ya kiwango na kusababisha kuharibika kwa haraka sana.

(a) Kwakuwa barabara ya Mwakaje – Mwachealale hadi Bumbwisudi imeharibika vibaya, ni lini barabara hiyo itafanyiwa matengenezo na ni taasisi gani inayowajibika kufanya matengenezo hayo.

(b) Wananchi wa maeneo hayo wakati wa ujenzi wa barabara hiyo, mazao yao yaling'olewa kupitisha ujenzi huo na baadhi wamelipwa, je, waliobaki watalipwa lini.

(c) Ni sababu gani zilizopelekea barabara hizo kuchelewa kukabidhiwa kwa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 23 lenye vipengele (a), (b)na(c) kwanza naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Naibu Spika, Barabara ya Mwakaje – Mwachealale hadi Bumbwisudi nimiongoni mwabarabara zilizojengwa kupitia mradi wa *MIVARF* kupitia mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB).* Aidha mradi huo ulikuwa ukiratibiwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili,Mifugo na Uvuvi.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu kama ifuatavyao:-

(a) Mpaka sasa barabara hiyo na zote zilizojengwa kupitia mradi wa *MIVARFU* bado ziko chini ya Wizara ya Kilimo, Maliasili,Mifugo na Uvuvi.

(b) Malipo ya fidia yanaratibiwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ambapo hivi sasa wanaendelea na zoezi la kuwalipa walioathirika kwa kungolewa mazao yao. Hivyo basi, tunawaomba wale wote ambao bado hawajalipwa fidia zao kuwa wavumilivu kwani watalipwa stahiki zao hatua kwa hatua.

(c) Serikali, inaendelea na taratibu za kisheria za kuzipeleka barabara hizo kwenye taasisi ambayo itaonekana itafaa kuzihudumia na Waheshimiwa Wajumbe mtajulishwa kwa vile barabara hizi zimejengwa maeneo mengi Unguja na Pemba.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana lakini pia nimshukuru Naibu Waziri wa Mawasiliano, Ujenzi na Usafirishaji. Mhe. Naibu Spika, barabara hizi zimejengwa zaidi ya miaka miwili na hata barabara za kimataifa basi *guarantee* yake sana inakuwa mwaka mmoja tokea kukabidhiwa, lakini hizi zina miaka miwili hazijakabidhiwa. Barabara hizi zimeharibika na lengo la serikali naona linapotea.

a) Je, ni lini au serikali ituahidi ni lini barabara hizi zitakabidhiwa kwa wahusika, ili ziweze kufanyiwa marekebisho kwa kiwango ambacho kimekusudiwa.

b) Wakati wa ujenzi wa barabara hizi wananchi wa maeneo ya Bubwisudi, Mwachealale na Mambosasa miundombinu yao ya maji iling'olewa kutokana na ujenzi huo wa barabara, lakini hadi leo haijarejeshwa. Je, na hili nalo pia linangojea mpaka wakabidhi barabara hizi au linaweza kufanywa hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali lake yenye vifungu (a) na (b) kama ifutavyo.

Ni kweli zinatakiwa zifuate taratibu kwasababu ni mradi ambao ulikuwa wa kimataifa lakini napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba ni juzi tu ambapo Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein alipokua akifungua soko la Kinyasini tarehe 9/12/2018 alitoa ahadi kwamba hizi barabara tutazichukua na kuzijenga hatua kwa hatua hadi zimalizike ambazo ni kilomita 152.

Hivi sasa sisi tumeshaanza Makangani/Mkanyageni na karibuni tu tutaitia lami. Kwahivyo, ni *process* ambayo ilichukuwa muda mrefu lakini tuna imani kubwa sana baada ya ahadi na agizo alilotoa Mhe. Rais hizi barabara zitajengwa kwa kuptia njia ya lami.

Kuhusu swali lake la miundombinu ya maji, ni kweli mimi mwenyewe karibuni nilipita niliona wananchi wa kule wanavyopata tabu ya maji, nitalichukua suala hili kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, ili kuhakikisha kwamba hili suala linafanyiwa kazi kwa lengo la

kuwasaidia wananchi wa kule nao wanaathirika na hii kadhia ya maji na kuhakikisha wanapata maji kama wenzao.

Mhe. Suleiman Sarahani Said: Nashkuru Mhe. Naibu Spika, mimi jina langu halina matatizo ukitaja Said Sarahan Suleimanga lote sawa *no problem*. Nashkuru Mhe. Naibu Spika, na mimi nimwambie Mhe. Waziri namshukuru kwa majibu yake mazuri, lakini nataka nimuulize swali moja lenye (a) na (b).

Katika mvua za masika za mwaka jana ziliharibu miundombinu mingi sana kule Pemba wafanyakazi wa kule Pemba walifanyakazi usiku na mchana kurudisha hali ile, lakini mpaka hii leo watu wale hawajalipwa.

a) Je, Waziri unayo taarifa hiyo.

b) Na kama unayo lini watu wale watalipwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naopenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a) na (b) kama ifutavyo.

Ni kweli mimi nakiri hilo na juzi tu nilipokuwa katika ziara ya Pemba nilikutana na wasimamizi wote wa ile miradi ambayo wanahusika na ile kadhi, na kusema kweli wamelipa mwezi wa Disemba. Lakini nimewaambiwa la mwanzo waanze kulipa Mwezi wa Mei na Juni ni miezi ambayo ina pesa kidogo, lakini miezi ambayo na mimi nilikuwepo walifanya kazi kubwa sana hadi saa tano za usiku na pia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alishuhudia hilo. Barabara nyingi ziliharibika kipindi kile, na nasema kwamba barabara nyingi ziliharibika kipindi kile na hili suala tunalichukua na tunalifanyia kazi na karibuni kwa maagizo niliyowapa wataanza kuwalipa wale wahusika.

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kuniona kuweza kunipa suala la nyongeza, Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali moja la nyongeza kama ifutavyo.

Ni lini barabara zangu kutoka Gogefar-Tumbe kuelekea bandarini na pale Kizota kwendea Finya zitajengwa, ili wananchi wangu wa Jimbo la Tumbe waondokane na usumbufu ambao unapatikana hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naopenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifutavyo.

Tunazijua zile barabara fika na kwamba anavyosema mwenyewe zile barabara zinakwenda sehemu muhimu sana kwenye soko la uvuvi. Kwahivyo, mimi namhakikishia kwamba baada ya kukaa na tutakapopata pesa basi tuangalie namna gani zile barabara tuzinusufu.

Nam. 15

Upatikanaji wa Huduma za Kitaalamu na Usafi Skuli za Sekondari

Mhe. Suleiman Sarahani Said - Aliuliza:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Rais Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa makusudi iliamua kujenga skuli za kisasa za Sekondari kila Wilaya za Zanzibar, ili kurahisisha upatikanaji wa elimu. Lakini skuli hizo kila moja inaendeleza masomo yake kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa katika skuli

hizo ambazo zilijengwa kwa madhumuni maalum na pia zilitakiwa kuwa na ukaribu katika uangalizi kwa taaluma zilizowekwa.

(a) Je, serikali inaziangali vipi skuli hizo kwa ukaribu wake kiusafi wa majengo na taaluma zinazotolewa na walimu.

(b) Kwakuwa skuli hizi zimejengwa kwa madhumuni maalum ya kitaaluma. Je, serikali inazikagua na kuonesha skuli gani bora kwa kila mwaka kimasomo na usafi.

(c) Je, kuna zawadi, shukurani au pongezi zozote zinazotolewa kwa walimu ambao wamefanya vizuri katika skuli zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 15 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo ya ugangulizi kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Benki ya Dunia ilijenga skuli 19 za Sekondari na Chuo cha Ualimu cha Benjamin William Mkapa huko Mchangamdogo kwa madhumuni ya kuongeza nafasi za upatikanaji wa elimu ya sekondari na mafunzo ya walimu na kuimarisha kiwango cha elimu hapa nchini. Skuli hizo zimepatiwa vifaa mbalimbali vya kufundishia ambavyo vimesaidia katika kuweka mazingira bora ya ufundishaji katika skuli hizo.

Baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakialihi kama ifuatavyo:-

(a) Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu inazifanyia ukaguzi wa masomo na mazingira ya skuli, skuli zote za Serikali na za binafsi zikiwemo skuli hizo mpya. Katika kipindi cha mwaka 2015/2016 hadi 2017/2018, jumla ya skuli 19 za kisasa zilifanyiwa ukaguzi. Skuli hizo ni skuli ya sekondari ya Mpendae, Kiembesamaki, Faraja, Kombeni, Jumbi, Paje Mtule, Mapinduzi, Mlimani, Mikindani na Umoja Uzini kwa Unguja na kwa Skuli ya Sekondari ya Wete, Chasasa, Konde, Chwaka Tumbe, Madungu, Dkt. Omar Ali Juma, Kiwani Mauani na Maendeleo kwa upande wa Pemba. Wakaguzi hutoa ushauri na mapendekezo ya hatua za kuchukua na maelekezo ambayo husaidia katika kuzitunza na kuziimarisha skuli hizo.

(b) Hadi sasa Wizara haijaanzisha utaratibu wa skuli hizo peke yake kuwa ushindani wa ubora wa kimasomo na usafi. Utaratibu uliopo ni skuli kuangaliwa ubora wa skuli zote, Hadi hivi sasa, matokeo ya Mitihani ya Taifa ya Kidato cha Pili na cha Nne ndiyo yanayotumika kuitambua skuli bora kiwilaya na kitaifa kwa kila mwaka. Katika Mitihani ya Kidato cha Pili ya mwaka 2017, miongoni mwa skuli mpya zilizofanya vizuri ni pamoja na Skuli ya Chasasa, Wilaya ya Wete, Madungu, Wilaya ya Chake na Kiembe Samaki Mchepuo wa Dini, Wilaya ya Magharibi "B". Kwa upande wa Mitihani ya Taifa ya Kidato cha Nne, miongoni mwa skuli zilizofanya vizuri ni pamoja na Skuli ya Chasasa Wilaya ya Wete, Madungu Wila ya Chakechake, na Kiembesamaki mchipuo wa dini, Wilaya ya Magharibi.

Kwa upande wa mitihani ya Kitaifa Kidatu cha Nne, miongoni mwa skuli zilizofanya vizuri kwa Zanzibar ni Skuli ya Kiembesamaki "A" Wilaya ya Magharibi "B"

(c) Wizara inazipongeza skuli zilizofanya vizuri badala ya mwalimu mmoja mmoja. Tunaamini kuwa mafanikio ya skuli na wanafunzi yanachangiwa na walimu wengi badala ya mwalimu mmoja anaefundisha somo moja au mawili. Aidha, wizara hutoa zawadi kwa paneli za masomo. Kwa mwaka 2017, wizara ilizizawadia paneli mbalimbali za masomo kaka vile katika somo la *"Building Construction*", skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni, paneli za masomo ya *Physics* na *Chemistry,* Skuli ya Sekondari ya Lumumba na Fidel Castro na paneli ya somo la *"Commerce",* Skuli ya Biashara Mombasa. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, naomba nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri lakini kwa heshima ya kipekee kwanza nimshukuru sana Dkt. Ali Mohamed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa makusudi kutoa ahadi ya kuzijenga shule zile na akaweza kuzitimiza kwa muda ambao lengo lake lilokusudiwaa.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri,

a) Je, huwoni kwamba kutoa zawadi au kutoa cheti au kufanya jambo lolote ambalo litakuwa na shukurani kwa walimu ambao watazitunza skuli zile ama kwa mafanikio ya wanafunzi kutoka wengi au kwa usafi kutasaidia wale walimu kupata moyo wa kuweza kuzitunza zaidi, nikimaanisha "mcheza kwao hutunzwa."

b) Ni lini tutaanzisha hekta maalum ya kuweza kuwapa zawadi watoto wanaofanya mitihani wakatokezea katika nafasi nzuri au skuli inayofanya vizuri. Lini tutaweza na sisi kuwapa hidaya au angalau kuonesha kwamba tunajali kwa kuwapa zawadi maskuli yetu na wanafunzi wetu na

walimu wetuu wakuu ambao ndiyo wanaosimamia zile skuli.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Ni kweli kwamba ki-*psychology* ya uwalimu zawadi inasaidia sana kuwatia ari wanafunzi, walimu na hata jamii kwa ujumla wake kwa hivyo utaratibu huo ni mzuri.Lakini utaratibu huu unaweza ukafanywa na taasisi mbali mbali sio lazima serikali peke yake, unaweza ukafanywa na kijiji, Kamati ya Skuli, *NGO* na unaweza unaweza ukafanywa na serikali. Kwa upande wetu serikali tumeanza kama tulivyosema hapa baadhi ya wanafunzi wanaopata madaraja ya kwanza katika kidatu cha sita wanafunzo 15 mara hii kwa mfano tumewapa ufadhili wa masomo. Hiyo ni jumla moja ya zawadi ambayo tunawapa wanafunzi. *(Makofi)*

Aidha, kwa upande wa skuli pia tunampango mzuri katika Wizara ya Elimu kwamba skuli itakayofanya vizuri zaidi tutawapatia fedha, kwa ajili ya kuimarisha masuala ya masomo. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kuweza kunipa fursa hii. Katika majibu ya Mhe. Waziri anazungumzia suala zima la mitihani ya kidatu cha nne lakini imeonesha wazi katika skuli zilizofanya vibaya katika mtihani ule ni skuli za Zanzibar.

Je, wizara yake imejitathmini vipi kuona kadhia ile ya kila mwaka skuli zetu za Zanzibar hushika nafasi za mwisho katika matokeo ya kitaifa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, sikubaliani kwamba Skuli za Zanzibar zimefanya vibaya. Nakubaliana kwamba baadhi zipo kwenye orodha ya mwisho. Skuli za Zanzibar katika ujumla wake tumefikisha wastani wa alama 70.8 asilimia hii si mbaya kwa kweli ni lazima tukubaliane hiyo siyo mbaya katika 100 wamepasi 70 siyo mbaya. Tatizo liliopo ni kwamba baadhi ya watu wanashindwa kuzitafsiri kwa usahihi takwimu hizi za kimasomo. Dasturi ya takwimu hizi za kimasomo tunaziita katika taaluma tunaziita *measure of central attendance* hizi zinajumuisha wastani *mode standard aviation* na mambo kama haya. Sasa, kwa hakika nataka nifafanuwe zaidi, wanafunzi wetu Zanzibar kwa mwaka huu wa Kidato cha Nne wamefanya vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano mwaka jana tulisema labda tumefanya vizuri zaidi, tulikuwa sehemu ya 73.8. Wanafunzi wenye uwezo wa kuingia Kidato cha Tano mwaka huu ni wengi zaidi kuliko mwaka jana. Mwaka jana tulikuwa na wanafunzi 2,981, mara hii ni 3,033. Matokeo hayo kwa kweli sio mabaya. Lakini nakubali tunazo changamoto na sasa wizara inajipanga kupambana na hizi changamoto ya kuwemo katika orodho ya mwisho, sio mbaya lakini ya kuwemo katika orodho ya mwisho. Hili tumejipanga na hivi sasa wataalamu wetu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wako katika kuzitembelea skuli hizo, ili tujue hasa kuna tatizo gani, nitazungumza na walimu, wanafunzi na wazazi. Kwahivyo, tunatarajia kwamba changamoto hizi za kuwemo katika orodha ya mwisho zitaondoka, ahsante sana.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa tena kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwanza

niipongeze Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuongeza idadi ya wanafunzi waliofaulu katika Kidato cha Tano mwaka huu.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na uongezeko huo wa elimu wa Kidato cha Tano na kwasababu tunajenga maskuli ya ghorofa katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Moja katika sababu ambayo mimi binafsi naona inarudisha nyuma kidogo elimu ni kutokuwa na madeni kwa wanafunzi wetu ili wapate sehemu fasaha na tulivu za kuweza kusoma nyakati zile baada ya madarasa.

a) Je, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali haioni kama kuna umuhimu sasa kujenga mabweni katika skuli hizi mpya tunazojenga, ili vijana wetu wakae pahali tulivu pa kusoma.

b) Ili kuwaepushia vijana wetu na mabarobaro majiani wakati wa jioni, kwa nini serikali isitie mkazo na lini itafanya mambo hayo ya kujenga mabweni katika skuli zetu hizi mpya.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, minong'ono imezidi, mnanong'ona kiasi ambacho hata watu wa kule kwenye mitambo wanasikia sauti zetu zaidi kuliko sauti ya yule anayezungumza. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafungo ya Amali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako napenda nimjibu Mhe. Mjumbe kama ifuatavyo.

a) Ni kweli kama mabweni yana umuhimu mkubwa sana katika kujenga mazingira bora ya wanafunzi kuweza kujifunza. Kwa kuelewa hivyo hivi sasa Wizara ya Elimu

na Mafunzo ya Amani, inaandaa waraka kupeleka serikalini ili kujenga hoja ya kutaka huduma za dahalia zirudishwe tena katika skuli zetu. Kwa kuanzia katika kufanya hilo na serikali inaona umuhimu wa kuwepo dahalia kwa kweli na kila mtu anaona umuhimu huo. Kwahivyo, waraka huwo unatayarishwa ili kujua taratibu na mbinu za kuweza kurudisha tena huduma za dahalia.

b) Vilevile, Wizara ya Elimu katika majengo ambayo itakayojenga tena inakusudia skuli moja katika Mkoa wa Mjini Magharibi pia nayo kujengwa ikiwa na sehemu ya dahalia. Skuli za dahalia ni muhimu na kweli tunaliafikia na tunalifanyia kazi hivi sasa.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante nimesimia kifungu cha 43(1) - 43(3) Kiongozi wa shughuli ya serikali au waziri yeyote anaweza kutoa kauli katika Baraza kuhusu jambo lolote ambalo serikali inawajibika na baada ya hapo Mwenyekiti wa Kamati inahusika na mjumbe mwengine aliyeidhinishwa na Kamati anaweza kupewa nafasi ya kutoa maoni ya Kamati juu ya kauli hiyo.

Kifungu cha 43(3) hakutakuwepo na majadiliano yeyote kuhusu kauli yoyote iliyotolewa kwa mujibu wa kanuni hii. Lakini Wajumbe wanaweza kwa idhini ya Spika kumuuliza maswali Waziri aliyetoa kauli hiyo kwa madhumuni kuelewa.

Leo hii nimeshuhudia kitendo cha watoto wa miezi 7 - 10 kama sikosei wanatoka nyumba za kulelea watoto Mazizini wakiwa wamebebwa wanapelekwa ama skuli au kitoa cha kulelea watoto wengine inaitwa *Zanzibar baby care*. Ninachokifahamu mimi utaratibu kama nimekosa kwa sababu mimi elimu yangu ni ndogo

nifahamishe miaka mitatu ndiyo mtoto anapelekwa nusury je, nyumba ya kulelea watoto wameshindwa jukumu lao kulea watoto wale, wakati wanalipwa maposho yote stahiki. Nilikuwa nataka kauli ya serikali na watoto ni wawili kama sikosei mmoja anaitwa Yussuf mmoja anaitwa Wahida. Pale ndiyo kituo cha kulea watoto hawa kweli wanakwenda kusoma au wanakwenda kulala kule na gari iliyowapakia ni Nam. Z263EG.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa, Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ningependa kidogo Mhe. Mjumbe atupe ufafanuzi vizuri kwa sababu kifungu 43(1) - 43(3) kinatokana na kauli za serikali hazitokani na kauli za mjumbe. Sasa yeye angesoma kifungu kinachomuhusu kutoa kauli hiyo anayotaka kutoa siyo hichi. Hichi ni cha kauli za serikali Mhe. Naibu Spika. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante nashukuru, Mhe. Jaku Hashim Ayoub nafikiria hoja yako imefahamika na kama alivyosema Mhe. Waziri Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwamba sio kauli za serikali hazitolewi kama hivyo ambavyo unataka wewe. Lakini nafikiri suala lako limefahamika na Mhe. Waziri mpe muda Mhe. Waziri akalichunguza kwasababu sio suala la kutolewa tu hapa nafikiri hiyo itakuwa ni busara zaidi. Sio suala ambalo linaweza *immediately* linaweza kutolewa majibu. Kwahivyo, Waziri anayehusika yupo na atalishughulikia hili.

Waheshimiwa Wajumbe, sasa nimemaliza kwa sasa hivi nampisha Mhe. Mwenyekiti (Mwanaasha Khamis Juma) atakuja kuendelea na shughuli nyengine za Baraza. Ahsanteni.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti alikalia kiti)

HOJA ZA KAMATI

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. sasa naomba nimwite Mhe. Omar Seif Abeid (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Afisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa).

Mhe. Omar Seif Abeid (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Afisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Mwenyekiti, wa Baraza la Wawakilishi kwa niaba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, naomba kuwasilisha muhtasari wa ripoti ya Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu *Allah (S.W)* mwingi wa rehma na mwenye kurehemu, pamoja na kumtakia rehma Mtume wetu, Muhammad *(S.A.W)* kwa kutujaalia, uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana tena katika Mkutano huu wa tisa wa Baraza la Tisa na kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako kuwasilisha Ripoti hii ya Kamati. Hapana shaka yoyote kuwa huu si uwezo wetu bali ni wake yeye *Allah Subhanahu Wataala*, hivyo hatuna budi kusema "*Alhamdulillah"*, na pia kuwaombea wale walio wagonjwa kupata nafuu.

Pia, kwa ruhusa yako nachukua fursa hii kutoa shukrani za kipekee na pongezi nyingi kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, kwa kazi kubwa sana wanayoifanya ya kuiongoza nchi yetu tunamuomba *Allah Subhana Wataala* awape nguvu, hekima na busara kwa kushirikiana na Mawaziri wote na serikali hii, ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo ya kuiongoza nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe, kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu, kuwasilisha Ripoti ya Kamati hii ya kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa kitaifa ya mwaka wa fedha 2017/2018, kwa niaba ya Kamati yetu ambayo mimi ndio mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maneno hayo machache ya utangulizi, sasa naomba nijielekeze katika lengo la kuwepo kwangu hapa. Lakini kabla ya kuendelea na chochote, napenda kutamka kwamba, huu ninaouwasilisha ni muhtasari wa Ripoti ya Kamati. Hivyo, ripoti yote kwa ujumla wake, tayari imeshasambazwa kwa wajumbe, sambamba na muhutasari huu naomba pamoja na ripoti uingie katika *hansard*.

Katika kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi kifungu nambari 108 kifungu kidogo cha (14) ambayo yanasimamiwa na Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mujibu wa kifungu hicho kamati inatekeleza majukumu ya kazi kama ifuatavyo:

i. Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia;

ii. Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza;

iii. Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi ya Wizara husika;

iv. Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha na kufikia malengo;

v. Kuchambua mapendekezo ya serikali kuhusu makadirio ya wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka;

vi. Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika;

vii. Kuchambua ahadi zote za wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo;

viii. Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa na spika.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika utekelezaji wake wa kazi zake imekuwa ikisimamia wizara mbili zifuatazo:

i. Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na
ii. Ofisi ya Rais, na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viogozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka wa fedha 2017/2018, ilifanya kazi zake katika mizunguko mitatu, ikiwa ni jumla ya wiki sita, ambazo zilifanyiwa kazi kama ifuatavyo:

a) Kamati ilifanya kazi zake Unguja kuanzia tarehe 14/08/20 17 hadi tarehe 25/08/2017 kwa mzunguko wa kwanza.

b) Kuanzia tarehe 13/11/2017 hadi tarehe 17/11/2017 Kamati ilifanya kazi zake Unguja na tarehe 20/11/2017 hadi

24/11/2017 Kamati ilimalizia kazi zake kwa Upande wa Pemba kwa mzunguko wa pili.

c) Aidha, Kamati ilifanya kazi zake Unguja kuanzia tarehe 15/01/2017 hadi 26/01/2017 kwa mzunguko wa tatu.

OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Ofisi hii imeundwa na Idara na Taasisi Zifuatazo**:**

i. Idara ya Huduma za Makamu wa Pili wa Rais;
ii. Idara ya Mipango Sera na Utafiti;
iii. Baraza la Wawakilishi;
iv. Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
v. Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Kudhibiti Madawa ya Kulevya;
vi. Tume ya Uchaguzi Zanzibar;
vii. Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar;
viii. Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa;
ix. Tume ya UKIMWI;
x. Idara ya Watu wenye Ulemavu;
xi. Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa;
xii. Ofisi kuu Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yeu kwa ujumla iliweza kufanya kazi zake vizuri kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Hatahivyo, kutokana na ukubwa wa ofisi hii kamati haikuweza kuzifikia baadhi ya Idara. Pamoja na kwamba kamati haikuweza kufikia baadhi ya idara, lakini kamati ilipokea taarifa ya ujumla ya wizara juu ya mpango wa mapato na matumizi wa taasisi hizo na wajumbe wa kamati hii walipata fursa ya kuhoji mambo mbalimbali, na hatimaye kujiridhisha kutokana na majibu ya jumla ya wizara na kamati ilizishauri idara hizo kuendelea kufanya kazi vizuri na kwa bidii, ili kufikia malengo

yaliokusudiwa na kuweka taswira nzuri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

BARAZA LA WAWAKILISHI

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Baraza la Wawakilishi limeweza kufanya kazi za kawaida kama ilivyoeleza katika Katiba ya Zanzibar kifungu cha 88(b)(c) na (d) ambapo shughuli hizo zote kwa mujibu wa maelekezo ya Katiba yetu Baraza lako limekuwa linayatekeleza, lakini pamoja na ufanisi huo Baraza lako bado limekuwa likikabiliwa na changamoto ambazo kamati inaomba kupatiwa ufumbuzi, kama vile kuwepo kwa tatizo la marejeo wa sauti (*echo*) katika ukumbi wa mikutano jambo ambalo halipendezi, na hulipelekea baadhi ya wakati wajumbe na wasikilizaji vikao kushindwa kusikia vizuri mijadala ya vikao. Hivyo basi tatizo ambalo ni la muda mrefu Kamati imeagiza kufanyiwe matengenezo hasa katika Ukumbi mkubwa ili kuondoa tatizo hili. *(Makofi)*

IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SMZ NA SMT

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilipata fursa ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Idara ya Uratibu. Kwa ujumla kamati imeridhishwa na uteketelezaji wa kazi za Idara hii pamoja na mambo mengine iliweza kufanya ziara kuangalia maendeleo na changamoto ya miradi ya TASAF III, kwa Unguja na Pemba pamoja na kupata kwenda kujifunza kwa wenzetu wa Tanzania Bara na kujionea wenyewe jinsi gani wananchi walivyoupokea kwa vitendo mpango wa kujiwekea akiba katika vikundi ambapo kamati yetu ilielezwa namna ambavyo wananchi hao wanavyofaidika kupitia mpango huo.

Kamati pia imefarajika sana kuona namna serikali zetu kupitia mfuko wa maendeleo wa jamii (TASAF) inavyowasaidia wananchi katika nyanja tofauti za huduma za kijamii, kama vile maji, elimu, afya na mazingira kama masuala mengineyo, ambapo pia kamati ilipata nafasi ya kutembelea miradi hiyo na kuona

maendeleo na changamoto zinazokabiliana nazo wananchi na jinsi gani serikali inavyojitahidi kuzitafutia suluhisho la kuzitatua changamoto hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla idara inafanya vizuri katika kuhakikisha majukumu yake yanatekelezwa ipasavyo. Hatahivyo, kamati kutokana na kuwepo kwa baadhi ya changamoto inashauri kuzingatiwa kwa baadhi ya mambo kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaihimiza serikali kuhakikisha kuwa inatoa mchango wake kwa miradi ya *TASAF* kwa wakati kwani kutofanya hivyo kutapelekea kutokamilika kwa wakati miradi iliyokusudiwa kwa walengwa.

Aidha, Kamati imeishauri Idara ya Uratibu wakati wa kuibuliwa miradi ya ujenzi kama ya skuli, ni vyema zaidi kuzingatiwa ujenzi wa skuli za ghorofa, ili kwenda sambamba na uhaba wa ardhi uliyopo na ili kukidhi haja ya mahitaji ya madarasa kwa skuli hizo.

Kamati pia imeshauri Waratibu na Wakurugenzi wa miradi ya *TASAF* kuhakikisha kuwa wanasimamia upatikanaji wa taarifa za ukaguzi wa miradi husika, ili kupatikana kwa ripoti ambayo itawezesha kuelewa mafanikio na changamoto ya miradi.

IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SMZ DAR-ES-SALAAM

Mhe. Mwenyekiti, mingoni mwa majukumu yake ya msingi ya ofisi hii ni kuratibu shughuli za SMZ kwa upande wa Tanzania Bara pamoja na kukuza na kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi wizara za SMZ na zile za Muungano na kukuza na kuimarisha mashirikiano baina ya washirika wa maendeleo na taasisi za kibalozi. Ofisi hii imekuwa ikifanya kazi zake vizuri na kamati

ilifurahishwa na utendaji kazi wa jumla na inashauri ifuatavyo ili ofisi hii iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Kamati, inashauri licha ya kufanyika kwa ukarabati katika baadhi ya sehemu ya jengo la ofisi lakini ukarabati zaidi unahitajika kama kuendelea kupiga rangi kwa baadhi ya maeneo ya jengo, ili liweze kuleta haiba na taswira nzuri ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo kwa Tanzania bara ni ofisi pekee ndio inayotumiwa na Serikali kule Dar-es-Salam.

Pia, kamati inaihimiza serikali kusimamia na kutekeleza mpango wake wa kuwa na jengo bora na la kisasa litakalotumika kwa ajili ya shughuli za Idara ya Uratibu za SMZ na taasisi nyengine ambazo zinafanya kazi kwenye jengo hilo.

Kamati, inaishauri Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ kutafuta utaratibu zaidi kuwezesha kuitangaza ofisi hiyo kupitia maadhimisho ya sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar ya kila mwaka, ili taasisi mbalimbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na SMZ, Balozi na taasisi za watu binafsi ziweze kuitumia ofisi hiyo na kurahisisha shughuli za ushirikiano kati ya taasisi hizo na serikali.

Aidha, kamati yangu inaishauri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kufuatilia suala la upatikanaji wa mgao wa tozo la ukusanyaji wa malipo ya minara, ambalo tayari serikali imeshaanza kulisimamia ipasavyo.

Ofisi ya Uratibu ya SMZ iliyopo Dar-es-Salaam imetekeleza wajibu wake kwa kuratibu ufuatiliaji wa suala hilo, lakini bado suala hilo halijapatiwa ufumbuzi na taasisi zinazohusika za Serikali zetu mbili. Pamoja na kwamba kama nilivyoeleza kwamba tayari serikali inalo na inalifanyia kazi.

Kamati, imeishauri wizara husika kutoa muongozo maalum kwa wizara na taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya umuhimu wa kuitumia Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ iliyopo Dar-es-Salaam, kabla ya maafisa na watendaji wao kuanza kazi zao za kiserikali wanapokuwa huko.

TUME YA KITAIFA YA URATIBU NA UDHIBITI DAWA ZA KULEVYA

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Kitaifa ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ina jukumu kuu la kuratibu mapambano dhidi ya uingizaji, usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya, ambazo ni changamoto kubwa kwa jamii yetu na inaendelea kuathiri vijana wengi ambao ndio nguvu kazi ya taifa. Pia, ina jukumu la kutoa taaluma kwa jamii juu ya athari za dawa hizo za kulevya, tiba pamoja na ushauri nasaha kwa waathirika wa janga hilo.

Tume, inaendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa licha ya kukabiliwa na changamoto kadhaa ambazo kwa kiasi kikubwa kimekuwa ikirejesha nyuma mapambano dhidi ya mtandao huo wa biashara haramu ya dawa za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa changamoto zinazoikabili tume hii ni kama vile upotevu wa vielelezo vya kesi na kukosekana kwa takwimu halisi juu ya idadi ya vijana walioingia na kutoka katika Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia *(Sober Houses)*, ambapo kamati imebaini kwamba vijana wengi wanaokuwepo kwenye nyumba hizo huwa wanajirejea rejea au huwa wanabadilisha nyumba wakati ambapo mwengine hukaa katika nyumba moja na baadaye kuhamia kwenye nyumba nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, ili kusaidia kukabiliana na changamoto hizo kamati yangu inatoa ushauri na maelekezo yafuatayo:

Kamati inaishauri Tume ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya kuwa karibu na taasisi zote ambazo zinahusika na kesi za madawa ya kulevya, ili kuhakikisha kwamba wale wanaojishughulisha na biashara hii haramu ya dawa za kulevya wanachukuliwa hatua zinazostahiki za kisheria, na kwamba tatizo la upotevu wa vielelezo vya kesi za madawa ya kulevya halitokei tena kama ambavyo ikijitokeza hapo awali.

Aidha, kamati imeishauri tume kuwashirikisha kikamilifu Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Masheha na hata mabalozi wa nyumba kumi katika kupata taarifa za watu wanaojihusisha na biashara za madawa ya kulevya.

Pia, kushirikiana na taasisi husika kuhakikisha mazingira bora ya ulinzi bandarini yanaimarishwa ikiwa ni pamoja na kuweka wataalamu na vifaa vya kutosha, ili kudhibiti uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevya kupitia bandari rasmi. Kwa upande wa bandari zisizorasmi kamati inashauri kuwatumia mabalozi wa nyumba kumi na watu wanaokaa karibu na madiko hayo ambao ni rahisi kupata taarifa kwa watu wanaojihusisha na uingizaji wa madawa ya kulevya ambao wanatumia bandari hizo zisizo rasmi. Jambo hili litasaidia kupata taarifa na ndipo itakuwa ni rahisi kujua namna gani ya kuendeleza vita dhidi ya wahalifu hao.

Kamati, imesisitiza pia Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia kwa vijana waliaacha utumiaji wa dawa za kulevya kiliopo Kidimini ambacho kimeshamalizwa kwa sasa kupatiwa samani, ili jengo hilo liweze kutumika kama ilivyokusudiwa.

TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ni Taasisi iliyoundwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar kifungu 119

kifungu kidogo cha kwanza na majukumu ya tume hiyo pia yameelezwa katika Katiba hiyo ya mwaka 1984.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu imeridhishwa sana na utendaji wa Tume ya Uchaguzi. Hatahivyo, kamati yangu imebaini baadhi ya mapungufu au changamoto ambazo zinaikabili tume hiyo na zinahitaji kufanyiwa kazi ambapo miongoni mwa changamoto hizo ni uhaba wa vyombo vya usafiri hasa magari, ukosefu wa jengo ya ofisi za kudumu za wilaya na ukosefu wa ghala la kuhifadhia vifaa, pamoja na kwamba serikali imeshawapatia nyumba ambayo ilikuwa ikimilikiwa na Shirika la Bandari.

Kamati, imeshauri kufanyiwa haraka mchakato wa ununuzi wa gari mbili za tume ambazo zinashughulikiwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, kamati imeagiza kukamilishwa kwa ukarabati wa nyumba iliyokabidhiwa tume na serikali, ili tume iweze kulitumia jengo hilo la kuhifadhia vifaa ambavyo Tume ya Uchaguzi imevihifadhi kwenye ghala ambalo si lake liliopo Kikwajuni.

WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, imeridhishwa sana na utendaji wa Wakala wa Serikali wa Uchapaji. Kimsingi wakala inaonekana kupiga hatua katika ushindani wa biashara ya uchapaji kwa kuimarisha huduma zake ambazo kwa sasa zimekuwa zikivutia wateja wengi. Wakala imeweza kununua mitambo ya kisasa ya uchapaji pamoja na kuimarisha huduma ikiwa ni pamoja na kuanzisha bohari yake ambayo inatarajiwa kutoa huduma kama duka la vifaa vya kuandikia yaani (*stationary*) kwa watu binafsi na taasisi za serikali.

Mbali na jitihada zinazochukuliwa na wakala bado kamati imebaini changamoto kadhaa zinazoikabili taasisi hiyo kama ifuatavyo: Upokeaji wa kazi za machapisho ni mdogo hususan katika taasisi za serikali, ukosefu wa jengo la kudumu la wakala.

Katika kukabiliana na changamoto hizo, kamati imeshauri wakala kuendelea kutafuta soko la nje, ili kuweza kuongeza mapato ya serikali. Kamati pia imeagiza kuharakishwa ujenzi wa Bohari ya Wakala, ili kuweza kutoa huduma za uuzaji wa vifaa vyao (*stationaries*) kwa taasisi za serikali na binafsi.

Kamati, imeishauri serikali kuweka msisitizo zaidi kwa wizara na taasisi zake zote sambamba na kuzishajihisha sekta binafsi kumtumia wakala huyo, ili kuweza kusaidia jambo ambalo linaongeza ufanisi kwa kiwanda hicho.

KAMISHENI YA KUKABILIANA NA MAAFA

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilitembelea Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa na kujionea jinsi kamisheni ilivyojipangia mpango endelevu wa kujenga uwezo kwa jamii katika kukabiliana na maafa, jambo ambalo limepelekea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu. Licha ya kuwa kamisheni inatekeleza majukumu yake kwa ubora wa hali ya juu, kamati imebaini changamoto mbalimbali zinazoikabili kamisheni hiyo ambazo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi na miongoni mwa changamoto hizo ni ukosefu wa jengo la ofisi ambapo kwa sasa kamisheni inatumia jengo la Kituo cha Huduma za Dharura.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inapongeza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuweza kuanzisha Akauti Maalum kwa ajili ya kupokea michango ya kukabiliana na maafa yanapotokea. Aidha, kamati inaishauri ofisi kuwa kuna umuhimu wa kuwa na maghala

maalumu ya kuhifadhia vifaa vya maafa, ili viweze kuhifadhika vizuri na kutumika wakati wa maafa yanapotokea.
Mhe. Mwenyekiti, vilevile, kamati imeiagiza kamisheni kuharakisha kuandaa muundo pamoja na Kanuni ya Sera Nam. 1 ya Sheria Nam. 1 ya mwaka 2015 ya Kupunguza na Kukabiliana na Maafa. Ili taasisi hiyo iweze kufanyia kazi kwa ufanisi. Kamati imeiagiza kamisheni kufanya uchunguzi kwa kupitia sheria inayotoa vibali vya uvuvi, ili kuweza kukabiliana na maafa yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya wavuvi hao jambo ambalo linaonekana kwamba baadhi ya wavuvi wanaotumia vifaa hivyo wana taaluma ndogo ya matumizi ya kifaa hicho na kusababisha miongoni mwao kupotekeza maisha na wengine kupata ulemavu wa maisha.

TUME YA UKIMWI ZANZIBAR

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika mizunguko yake ilipata kuifikia Tume ya UKIMWI na kupata maoni ya watendaji ambapo pamoja na mambo mengine kamati ilielezwa mambo mbali mbali ya kimaendeleo na changamoto ambazo tume imekuwa ikikabiliana nazo.

Katika utekelezaji wa majukumu yake Tume ya UKIMWI inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa watoa huduma za afya, uchache wa vifaa tiba, vifaa vya uchunguzi katika utoaji wa huduma za afya ya uzazi hasa katika utoaji wa huduma za saratani ya kizazi na kasi ndogo ya mabadiliko ya tabia katika jamii.

Mhe. Mwenyekiti, kufuatia changamoto hizo, kamati imeishauri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutokana na uzito wa usimamiaji wa suala la UKIMWI ni vyema ofisi kuipatia kasma yake ya kibajeti tume hii, ili iweze kutekeleza majukumu yake kama ipasavyo.

Kamati imeishauri tume kuendelea kusimamia mazingira ya masuala ya UKIMWI katika sekta za serikali na zile za binafsi kama sheria na miongozo ya nchi ikiwemo Sera ya Mkakati wa Sheria ya VVU na UKIMWI na miongozo inayohusiana na usalama na afya sehemu za kazi inavyoelekeza. Aidha, kamati imeiagiza tume kuhakikisha kuwa inaimarisha jitihada za ufuatiliaji wa taarifa za maambukizi ya UKIMWI katika ngazi za chini, ili kuweza kupata taarifa sahihi zisizogongana na maeneo mengine ya ufuatiliaji.

Mhe. Mwenyekiti, kamati pia inaishauri tume iendelee kuihamasisha jamii kufanya uchunguzi wa saratani ya kizazi mara kwa mara hasa kwa watu wanaoishi na VVU, ambao wamo katika hatari ya kupata saratani hiyo, pamoja na kuhamasisha mabadiliko ya tabia katika jamii kuweza kujikinga na maambukizo ya UKIMWI.

IDARA YA WATU WENYE ULEMAVU

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli idara hii imekuwa ikifanya shughuli zake vizuri na inastahili pongezi katika kuhakikisha haki na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu zinapatikana. Pamoja na utekelezaji wake mzuri ambao umeonesha mabadiliko makubwa na kutoa matumaini kwa watu wenye ulemavu. Lakini idara hii kama taasisi nyengine haikukosa kuwa na changamoto kutokana na kuwa inaendeleza kusimamia shughuli zake za siku hadi siku, ambapo baada ya kamati yetu kutembelea na kukutana na watendaji, kamati ilibaini kwamba zipo changamoto ambazo ni vyema na busara zikatafutiwa ufumbuzi.

Changamoto hizo ni kama uhaba wa bajeti ambao ni kikwazo katika utekelezaji wa kazi zake, ili kufikia lengo kama walivyojipangia. Kuwepo kwa uhaba wa vyombo vya usafiri,

ukizingatia kwamba shughuli za idara hii zinahitaji ufuatiliaji wa mara kwa mara, kama vile kufuatilia kesi katika Mahakama mbalimbali, lakini pia kuwafuatilia waathirika mbali mbali wanaofanyiwa vitendo vya udhalilishaji. Changamoto nyengine ni kesi za udhalilishaji zinazogusa watu wenye ulemavu kukosa nguvu na kuwa na nguvu ndogo za watendaji wanaofuatilia kesi hizo na kukosekana kwa mkalimani wa lugha za alama.

Mhe. Mwenyekiti, kufuatia kuwepo kwa changamoto hizo, kamati imeishauri wizara kutoa kipaumbele maalumu cha kibajeti na ajira kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Aidha, kamati imeishauri wizara kuona umuhimu wa kuliwekea Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu kasma yake badala ya Baraza hilo kuendelea kutegemea bajeti ya idara ambayo bado haijitoshelezi pamoja na kuwawazesha wanasheria wanaosimamia kesi wa idara hii, ili kuzisimamia vyema kesi za udhalilishaji hasa kwa watu wenye ulemavu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeona kuna umuhimu pia wa idara kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kufanya utafiti, ili kuweza kuelewa takwimu na idadi ya walimu hasa wenye taaluma za watu wenye mahitaji maalum, ili waweze kusaidia kuwaendeleza kielimu watu wenye mahitaji maalum.

IDARA YA SHEREHE NA MAADHIMISHO YA KITAIFA

Mhe. Mwenyekiti, idara hii imeendelea kutekeleza kazi zake kwa ufanisi na kwa namna ya pekee, kamati hii inatoa pongezi kwa Mhe. Balozi Seif Ali Iddi ambaye ndiye Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Sherehe kwa kufanikisha maadhimisho ya kutimiza miaka 54 ya Sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2018 kwa mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, licha ya ufanisi ilioupata idara hii bado inakabiliwa na changamoto kama vile uhaba na uchakavu wa vifaa; yakiwemo mashamiana yanayotumika katika sherehe za kitaifa. Hivyo, kamati inaishauri serikali kutafuta namna ya kupata fedha kwa ajili ya kununua vifaa vipya na vya kisasa ambavyo vitatumika katika shughuli na sherehe mbalimbali za kitaifa.

OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS – PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa ofisi hii kwa Pemba, ofisi inafanya kazi vizuri na kuisimamia ipasavyo utekelezaji wa bajeti kwa taasisi zote zilizo chini yake. Kwa upande wa Pemba, kamati ilifika na kujionea utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo iliyo chini ya *TASAF*na kuanza matayarisho ya awali kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na mambo mengine.

Kwa upande wa changamoto kamati imebaini changamoto kuu katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba ni kukosekana kwa nyumba ya kudumu kwa ajili ya makaazi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais anapofanya ziara zake Kisiwani Pemba. Kama nilivyokwishaeleza pamoja na changamoto ya kuwepo kwa ufinyu wa nafasi za kufanyia kazi katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeihimiza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Pemba kukamilika kwa utaratibu wa kuanza kwa ujenzi wa nyumba ya makaazi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais iliyopo Pagali, Wilaya ya Chake Chake, ili ujenzi huo uweze kufanyika kwa wakati na kumuwezesha kiongozi huyo kuwa na sehemu maalum ya kupumzikia akiwa Kisiwani Pemba. Vilevile, kamati imeishauri Ofisi ya Makamu wa Pli wa Rais kuzingatia ushauri

wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa kujenga jengo la ziada ambalo litakidhi mahitaji ya ofisi hiyo kwa Pemba.

HALI YA KIFEDHA KWA JUMLA KWA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS KATIKA KIPINDI CHA JULAI-DISEMBA, 2017/2018

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai-Disemba, 2017 Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na taasisi zake imeweza kuingiziwa jumla ya fedha bilioni 15,434,739,762 ambazo ni sawa na asilimia 99 kati ya shilingi 15,577,894,526 ilizopanga kutumia kwa kazi za kawaida na mshahara. Aidha, ofisi imeweza kuingiziwa jumla ya shilingi 2,730,186,626 sawa na asilimia 45 kati ya shilingi 6,099,929,378 kwa kazi za maendeleo. Kamati inachukua fursa hii kuipongeza sana serikali kwa kuipatia idara hii kiwango hicho cha fedha ambazo zimeweza kufanikisha utendaji bora wa ofisi hii.

Pia, kamati inachukua fursa hii kuipongeza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa usimamizi wake bora katika majukumu yake. Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ukusanyaji wa mapato Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa kwa kipindi cha Julai-Disemba, 2017, imefanikiwa kukusanya shilingi 7,485,000 sawa na asilimia 47 ya makadirio ya malengo ya ukusanyaji.

OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inaundwa na Idara na Taasisi zifuatazo:

i) Ofisi ya Faragha ya Mhe. Rais;
ii) Idara ya Huduma za Rais;

iii) Idara ya Mawasiliano na Habari Ikulu;
iv) Ofisi ya Baraza la Mapinduzi;
v) Kitengo cha Sera, Ufuatiliaji na Tathmini;
vi) Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi;
vii) Idara yaUendeshaji na Utumishi;
viii) Idara ya Mipango Sera na Utafiti;
ix) Idara ya Usalama wa Serikali (GSO) na
x) Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Pemba.

OFISI YA FARAGHA YA MHE. RAIS

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Faragha ya Mhe. Rais ina majukumu ya kuratibu na kusimamia shughuli zote za Mhe. Rais pamoja na kufuatilia utekelezaji wa ahadi zake kwa lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma zilizo bora na kuweka ukaribu baina ya wananchi na serikali yao hasa kwa Kiongozi wetu Mkuu ambaye ni Rais wa nchi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa wakati wote ofisi inaendelea kutelekeza majukumu yake kwa ufanisi kama ilivyojipangia. Kimsingi, kamati imeridhishwa sana na utendaji wa Ofisi ya Faragha ya Mhe. Rais kwa kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa ahadi za Mhe. Rais pamoja na kuhakikisha shughuli zote za ofisi hiyo zinatekelezwa na kukamilika kama zilivyopangwa licha ya kuwepo kwa changamoto ndogo ndogo ambazo zinakabiliana nazo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa changamoto inayoikabili ofisi hii ni pamoja na kuwepo kwa athari kubwa za mmong'onyoko wa ardhi karibu katika nyumba zote za Ikulu. Kwa mfano, nyumba ya Ikulu Migombani, Kibweni, Bwefumu na Mkokotoni kwa

Unguja na Mkoani kwa Pemba. Kamati imeona suala hili linahitaji hatua za dharura na za haraka ili kulipatia ufumbuzi.

IDARA YA MAWASILIANO IKULU

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mawasiliano Ikulu ni idara muhimu ambayo miongoni mwa majukumu ni kumuunganisha Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na wananchi wake anaowatumikia kwa kuweka bayana shughuli mbali mbali anazozitekeleza Mhe. Rais kwa lengo la kuwafikishia maendeleo wananchi wote.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi hii mbali ya utekelezaji mzuri wa majukumu yake, lakini inakabiliwa na changamoto ya muda wa utoaji na urushaji wa habari katika vipindi vya redio na televisheni vya hotuba za Mhe. Rais kuwa sio rafiki kwa wananchi wengi kuweza kupata taarifa hizo zinazorushwa katika vipindi hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inashauri kuandaa utaratibu wa kupanga muda muafaka wa kurusha vipindi vya redio na televisheni vya hotuba ya Mhe. Rais hasa ule muda ambao watu wengi wanakuwepo majumbani baada ya kazi. Kamati imependekeza kukaa pamoja na *ZBC* Redio na Televisheni kuzingatia muda huo kwani muda wanaotoa taarifa hizo huwa wananchi wengi hawapati kuzisikiliza hotuba za Mhe. Rais hasa wananchi walioko vijijini ikiangaliwa kwamba wao muda mwingi wanakuwa hawasikilizi redio isipokuwa kwa muda wa jioni au usiku.

OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI

Mhe. Mwenyekiti, kamati imepata fursa ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, ambayo kwa kiasi kikubwa imekuwa ikitekeleza majukumu yake

bila kuwepo changamoto za kibajeti ambazo zingekwaza utekekelezaji wa majukumu yake kinyume na taasisi nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imebaini baadhi ya changamoto ziliopo kwenye ofisi hii kwa sasa, ni kukosa eneo la kutosha lenye nafasi kwa ajili ya uwekaji wa maktaba inayokusudiwa kutengenezwa katika Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, ili iweze kutumika kwa Waheshimiwa Mawaziri wakati wa utekelezaji wa majukumu yao. Kihalisia Ofisi ya Baraza la Mapinduzi ambayo ni moja kati ya ofisi muhimu katika Ofisi ya Rais, ofisi hii ina jukumu kuu la kuandaa vikao vya Baraza la Mapinduzi na kamati zake za Makatibu Wakuu na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeshauri kulipatia ufumbuzi suala hilo na wizara ihakikishe kuwa inatafuta eneo jengine litakalotumika kwa ajili ya Ofisi za Baraza la Mapinduzi na kupata ukumbi kwa ajili ya mikutano ya kamati zake. Kwa hatua za awali, ofisi zilizopo zifanyiwe ukarabati na kutiwa rangi ili ziendelee kutumika hadi zitakapopatikana ofisi nyengine.

KITENGO CHA SERA, UFUATILIAJI NA TATHMINI

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya saba imedhamiria kuimarisha utendaji kazi kwa viongozi na watendaaji wake pamoja na mambo mengine iweze kutoa huduma bora kwa wananchi na kuwaletea maendeleo endelevu. Hivyo, pamoja na hatua nyengine muhimu ilizozichukua, imeamua kuanzisha kitengo maalum cha ufuatiliaji na tathmini katika Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, ili kifanye tathmini ya kina ya utendaji na uwajibakaji katika wizara mbali mbali na taasisi za umma. Kamati inampongeza sana na kwa dhati Mhe. Rais na Mwenyekiti Baraza la Mapinduzi kwa kukianzisha kitengo hicho na kumteua Balozi Ramia kukisimamia kitengo hicho. Kamati imefurahishwa sana na jambo hilo kwani imeona kwamba kuanzishwa kwa

kitengo hiki kutasaidia utendaji bora wa kazi wa wizara na taasisi zake. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Kitengo cha Sera, Ufuatiliaji na Tathmini kimeanzishwa kwa madhumuni ya kupata taarifa muhimu za utekelezaji wa mipango, mikakati na Sera za Serikali kwa lengo la kujua na kujipima ufanisi wa shughuli zilizotekelezwa na kupima jinsi rasilimali fedha zinazotolewa endapo zimetumika ipasavyo na kama zimetoa mwelekeo mzuri kama ilivyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, licha ya kuanzisha kwa Kitengo Maalum cha Ufuatiliaji na Tathmini katika Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, ili kiweze kufanya tathmini ya kina ya utendaji na uwajibakaji katika kutekeleza majukumu yake mbalimbali ya kazi kwenye taasisi za umma. Kitengo kinakabiliwa na changamoto ya kutokamilika kwa muundo maalum wa kitengo na kutokuwa na wafanyakazi wa kutosha ambao wanawahitajika, ili kitengo hicho kiweze kufanya kazi zake vizuri na kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaishauri wizara kuhakikisha kuwa katika bajeti ya 2018/2019, Kitengo hiki cha Ufuatiliaji na Tathmini kinapangiwa kasma yake, ili kiweze kuwa na nguvu ya ufuatiliaji na kufanya tathmini ya maendeleo ya mipango mbali mbali ya serikali. Vilevile, kamati imeishauri wizara kusimamia uharakishwaji wa uandaaji wa muundo husika wa Kitengo cha Sera, Ufuatiliaji na Tathmini. Pia, ihakikishe kuwa wizara inakipatia kitengo watendaji wenye uwezo na uzoefu, ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi kabla ya bajeti 2018/2019 kwa lengo la kitengo hicho kiweze kufanyakazi kwa mujibu wa utaratibu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo kamati imeshauri wizara kuhakikisha kuwa Kitengo cha Sera na Ufatiliaji na Tathmini kinatoa ripoti ya utekelezaji wa kazi zake katika kipindi cha awamu ya mwisho ya kazi za Kamati ya Kusimamia Ofisi za

Viongozi Wakuu wa Kitaifa, ili kamati nayo yako iweze kukishauri kitengo hicho.

IDARA YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA URATIBU WA WAZANZIBARI WANAOISHI NJE YA NCHI

Mhe. Mwenyekiti, idara hii ina dhamana ya kuhakikisha kwamba wa Zanzibar wananufaika na uhusiano uliopo baina yake na jumuiya za kikanda na kimataifa. Aidha, idara inawaunganisha Wazanzibari walio nje ya nchi kwa dhamira ya kuwaweka karibu na kufahamu maendeleo ya nchi yao na waweze kusaidia katika nyanja mbalimbali za maisha ikiwa ni pamoja na shughuli za kiuchumi na kijamii.

Pamoja na mambo mengine idara hii ni miongoni mwa idara muhimu sana katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti Baraza la Mapinduzi na kwamba inatekeleza majukumu yake vizuri sana, lakini katika kutekeleza majukumu hayo inakabiliana na baadhi ya changamoto za kuchelewesha kupata taarifa za vikao vya mashirikiano baina ya Zanzibar na Tanzania Bara.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeshauri Idara ya *Diaspora* kuhakikisha kwamba fursa za kiuchumi na kibiashara zitokanazo *Diaspora* kwa Tanzania zinasimamiwa na kuendelezwa vizuri kwa maslahi ya wananchi wetu wa Zanzibar, pamoja na kuwashajihisha wana *Diaspora* wa kikanda kujikusanya pamoja ili wajione kama wana *Diaspora* wengine na kuweza kutoa michango yao mikubwa katika fursa za kiuchumi na kibiashara hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imeishauri kuwa na mfumo wa takwimu (*data base*) wa utoaji wa taarifa ili iweze kuwafikia na kuwatambua kiurahisi wana-*Diaspora* wote wa kikanda pamoja

na kutanua wigo kwa kuwatumia Wana-*Diaspora* wa Zanzibar, ili waweze kutangaza utalii wa Zanzibar na kuweza kukuza maendeleo ya kiuchumi ya nchi yetu. *(Makofi)*

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Idara hii ina jukumu la kuratibu na kusimamia Sheria, Kanuni za Utumishi na Kusimamia Shughuli za Uendeshaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Menyekiti, katika kuhakikisha utekelezaji mzuri wa idara hii, kamati imeiagiza idara hii kuhakikisha kuwa inaandaa utaratibu endelevu wa kupima afya za wafanyakazi kila baada ya kipindi cha miezi sita, pamoja na kuandaa programu ya kutoa taaluma ya ufahamu juu ya maradhi yasiyo ya kuambukiza kwa watumishi ili waweze kupata uelewa juu ya afya zao ikizingatiwa kwamba, miongoni mwa watumishi wa wizara hii wanawahudumia viongozi wetu wakuu wa nchi. Aidha, kamati imeagiza idara kuandaa mpango wa urithi wa nafasi za kazini (*Succession Plan*), ili endapo mkuu wa ofisi amefikia muda wake wa kustaafu kusiwe na nafasi tupu kutokana na kukosekana kwa mtu mwenye sifa za kushika nafasi hiyo.

IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango Sera na Utafiti ina jukumu la kuratibu utekelezaji wa shughuli za Mipango, Sera na Tafiti za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kimsingi, inatekeleza majukumu yake kama ilivyojipangia.

Katika kuimarisha utendaji wa ofisi hii, kamati inashauri kuhakikisha kuwa kunakuwa na matokeo ya utafiti kwa wananchi juu ya fursa za masoko katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Pia, kutoa taarifa za Mpango wa Kupunguza Umasikini nchini

(MKUZA), ili jamii iweze kuuelewa mpango huo na kuondokana na umasikini. Aidha, idara imeshauriwa kuimarisha mashirikiano na vyuo vikuu katika masuala hayo ya kiutafiti.

OFISI YA USALAMA WA SERIKALI (*GSO*)

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Usalama (*GSO*) ni idara yenye jukumu la kimsingi na kusimamia masuala yote ya usalama wa serikali kwa ujumla wake. Kamati, katika utekelezaji wa kazi zake imepata fursa ya kutembelea idara hii na kuangalia utendaji wa kazi zake za kila siku, kwa ujumla imeridhishwa na utendaji kazi wa idara hii.

Pamoja na utendaji wake wa kazi, idara hii inakabiliwa na changamoto ikiwemo suala la uchakavu wa jengo lililokuwa linatumiwa na idara hiyo, upungufu wa vitendea kazi na kukosekana kwa eneo maalumu lenye usalama kwa ajili ya kuhifadhia nyaraka muhimu za serikali ambazo hutunzwa na idara hiyo.

Ushauri. Kamati, imeshauri kufanyiwa marekebisho zaidi katika Ofisi ya '*GSO'*, ili kuondokana na hali ya uchakavu wa jengo na kuwawezesha wafanyakazi kufanyakazi zao katika mazingira bora, mazuri na yenye usalama zaidi. Aidha, katika katika kuimarisha ufanisi wa kazi zake idara hiyo, kamati imeshauri kufanyiwa marekebisho ya sheria inayohusiana na uwepo wa Idara ya Usalama wa Serikali (*GSO*) Zanzibar, pamoja na kwamba jambo hili limekuwa likizungumzwa mara nyingi, ambapo ni moja kati ya sababu na changamoto zinazoikabili idara hiyo kwa hapa Zanzibar.

OFISI YA RAIS NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI- PEMBA

Mhe. Mwenyekiti, ofisi hii inajukumu la msingi kushughulikia Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa upande wa Pemba**.** Ofisi inaendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu licha ya kuwepo kwa changamoto zinazoikabili ofisi hii.

Mhe. Mwenyekiti, kamati ilitembelea maeneo mbali mbali katika Ikulu ya Mkoani na kubaini kuwepo kwa changamoto kubwa inayotokana na athari ya mmong'onyoko wa ardhi unaosababishwa na mvua, licha ya kuwepo kwa juhudi za kujenga ukuta huo wa mawe ambao utasaidia kwa kiasi kikubwa kuzuia hali hiyo ya mmong'onyoko wa ardhi katika Ikulu hiyo ya Mkoani. Kimsingi, kuendelea kwa mmong'onyoko huo kutasababisha athari kubwa ikiwemo kubomoka kwa majengo yenyewe katika Ikulu ya Mkoani.

Kamati, imeshauri ofisi kuhakikisha kuwa ujenzi wa ukuta katika Ikulu ya Mkoani unaendelezwa kwa hatua za awali huku kukitafutwa njia bora za kitaalamu, ili kunusuru majengo ya Ikulu kutokana na hali ya mmong'onyoko unaoendelea hivi sasa.

Hata hivyo, kutokuendelea kwa ujenzi huo kunatokana na uhaba wa fedha ambapo jumla ya shilingi milioni thelathini ambazo zilitolewa na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji kwa ajili ya kusimamia ujenzi huo, lakini hadi wakati kamati ilipotembelea eneo hilo ujenzi huo ulikuwa bado haijafanyika. Pamoja na mambo mengine ambayo yanaonekana kwamba ni athari ambayo yangeweza kujitokeza.

Kamati, inaiagiza Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhakikisha kuwa ujenzi wa ukuta huo unaendelezwa pamoja na kutafuta njia mbadala kama tulivyotangulia kuzieleza za kitaalamu, ambazo zitatumika kulinusuru jengo hilo la Ikulu na hali ya mmong'onyoko uliopo hivi sasa.

HALI YA KIFEDHA YA JUMLA KWA OFISI YA RAIS MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI KATIKA KIPINDI CHA JULAI-DISEMBA, 2017/2018

Katika Kipindi cha Julai-Disemba, 2017 Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi iliweza kuingiziwa jumla ya fedha shilingi bilioni 1,665.5 kwa Fungu A01 na TZS 1,178.7 milioni kwa matumizi ya kawaida na TZS.317.0 milioni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kwahivyo, kamati kutokana na uingizwaji huo wa fedha, kamati inaipongeza sana serikali kwa kuipatia ofisi hii muhimu idadi ya fedha hizo ambazo zimeiwezesha wizara hii kufanya kazi zake kama ilivyojipangia.

Katika, kuimarisha utekeleza mzuri wa majukumu yake kila idara zinazosimamiwa na wizara hii. Kamati yetu imetoa maoni, ushauri na maagizo mbali mbali ambayo tunaamini yakitekelezwa yataweza kusaidia utendaji kazi ulio bora katika taasisi zetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano wao mkubwa uliopelekea leo hii kusimama mbele yako na kuwasilisha Ripoti hii ya mwaka 2017/2018. Bila ya ushirikiano huo, kamati hii isingeweza kufanikisha ripoti hiyo. Wajumbe wenyewe ni kama wafuatavyo:

1.	Mhe. Omar Seif Abeid	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdallah	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Mjumbe
4.	Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Mjumbe
5.	Mhe. Mussa Ali Mussa	Mjumbe
6.	Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	Mjumbe

7. Mhe. Ame Haji Ali Mjumbe

Aidha, kamati inaratibiwa na makatibu wawili ambao ni:

1. Ndg. Karima Abdul Wahab
2. Ndg.Talib Enzi Talib

HITIMISHO

Kwa mara nyingine, napenda kuchukuwa fursa hii kukushkuru kwa dhati wewe Mhe. Mwenyekiti kuniruhusu kuwasilisha Ripoti hii ya Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa mbele ya Baraza lako tukufu. Pia, nawashukuru Wajumbe wote wa Baraza hili kwa ustahamilivu wao na usikivu wao wa hali ya juu kwa muda wote niliokuwa hapa nikiwasilisha Ripoti hii.

Nawaomba, Waheshimiwa Wajumbe wote waijadili, waichangie na hatimae waipokee ripoti hii. Sambamba na hilo tunachukua fursa hii kwa niaba ya kamati yangu kutoa shukurani kwa Mawaziri, na Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote wa ofisi zilizo chini ya kamati yetu kwa mashirikiano yao waliotuonesha wakati wa utekelezaji wa kazi zetu ambazo zimesababisha kufanya kazi zetu kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba kutoa hoja ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa ripoti yako. Waheshimiwa Wajumbe ripoti imetolewa na imeungwa mkono majadiliano yanaendelea. Mchangiaji wetu wa mwanzo wa ripoti hii naomba nimwite Mhe. Ali Suleiman Ali,

atafuatiwa na Mhe. Shehe Hamad Mattar na Mhe. Simai Mohamed Said ajiandae.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako hili kuchangia Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Mwenyekiti pamoja na wajumbe wote wa kamati hii kwa kazi zao nzuri walizozifanya hadi kutufikia ripoti hii, ambayo ina umuhimu wake juu ya kuendeleza shughuli mbalimbali au kusimamia vizuri viongozi wetu wakuu wa kitaifa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Katibu Mkuu Kiongozi, Mawaziri wake wote wawili wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, tuseme tu kwamba kwa jumla nawapongeza wafanyakazi wote wa wizara hizi mbili, hasa tukizingatia kwamba viongozi wetu hawa ndio wadau wa kwanza wa kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri katika kuhakikisha shughuli zetu, hazipotezi na wala hatuna kasoro katika mafanikio yake.

Mhe. Mwenyekiti, hizi wizara mbili ambazo zimesomwa hapa zina mambo mengi, lakini mimi nitasema haya nitakayosema. Lakini, kwa jumla nimepongeza wizara zote na taasisi zake, ile nitakayokuwa sikuigusa wajue nimewapongeza kwa kazi zao nzuri kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, tunajua katika kufuatilia shughuli za kamati tunakumbana na mambo mengi na mambo yale huwa ni changamoto ambazo zinataka kupata maelekezo au ushauri, ili wenzetu wende vizuri zaidi. Nitaanza ukurasa wa 9 Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana kamishna anayehusika kwa kazi zake nzuri ambazo kwa muda mfupi aliyokaa tumehakikisha kwamba kuna mabadiliko makubwa ya kazi zake. Mimi husema katika maisha ya binadamu usiseme na wewe kaa, bajeti ya maafa, lakini kiutaratibu unatakiwa lazima liwekwe fungu la dharura ili inapotokea dharura litumike kwa yale maafa yaliyotokea. Tunamuomba Mwenyezi Mungu asiyalete maafa katika nchi yetu, kwasababu yakitokea ni taharuki na tunapata shida sana katika maeneo mbalimbali. Ushauri wangu Mhe. Mwenyekiti pamoja na juhudi nzuri anazoendelea nazo mwenzetu huyu na watendaji wake, niseme kwamba kuna mambo anakwenda katika vyombo mbalimbali mpaka taasisi za mapolisi na majeshi anafika kuelimisha athari za maafa katika nchi yetu, linapotokea hili huwa ni janga la kitaifa halina mwenyewe.

Kwahivyo, naomba tu, kuna mambo yameelekezwa humu lakini natoa ushauri wangu kabisa, yanapotokea maafa hasa siku za mvua za masika. Mhe. Mwenyekiti, wewe shuhuda tuko mpaka mmoja, Jimbo la Chukwani na Jimbo langu la Kijitoupele, kuna athari kubwa zinatokea katika maeneo yetu hususan sehemu ya Ziwamaboga. Hapa pahala panatupa shida sana na adha kubwa sana na mkusanyiko wa maji ya pale ndio huenea sehemu mbalimbali baadhi ya wakati Mwenyezi Mungu atuepushie hutokea maafa kwa watoto wetu. Kwahivyo, namuomba sana mwenzetu huyu kamishna kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti baada ya shughuli zetu za Baraza tukimaliza tuko tayari tumualike aje afanye ziara aangalie kero na taharuki inapotokea siku za mvua watu wanaoathirika katika maeneo yetu.

Kwakweli, kwa upande wangu eneo langu hilo lina matatizo makubwa, ukienda Kijitoupele, kwa Ngulangwa na kwengineko. Kwahivyo, ningemuomba maeneo haya ya Tomongo na kwengine aje tuyatembelee ili aone. Kwasababu ni vyema Mheshimiwa ukaweka kinga mwanzo kuliko kutokea maafa ukaja ukahangaika baadae, kinga yenyewe nafiki ni taaluma na yeye kuona yale mazingira yaliyokuwepo anaweza kuwapa taaluma wale wananchi wakaelewa juu ya umuhimu wa kutafuta hifadhi ya usalama katika maeneo mbalimbali.

Mhe. Mwenyekiti, tumeelezwa hapa katika ukurasa wa kwanza katika changamoto namba 1, naomba ninukuu kama ilivyo inasema kwamba:

"Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa katika utekelezaji wa kazi zake imekuwa inakabiliana na changamoto mbali mbali zikiwemo:

(i) Inategemea fedha za maendeleo kutoka kwa wahisani ambako kunapelekea shughuli zilizopangwa kutokamilika kwa wakati".

Mhe Mwenyekiti, niseme tu kwamba kweli panapotokea maafa haya huwa tuna shida nyingi sana na kamisheni hii huwa ina harakati nyingi za kuhakikisha kwamba matatizo yaliyotokea anahangaika kufa na kupona. Kwahivyo, muhisani ana hiari yake, lakini fedha za bajeti zimesema hakuna bajeti ya maafa. Sasa liweko fungu ambalo la dharura ikitokea itakuwa ndio fedha hizo zitumike kwa wale wahanga wanaopata maafa yale wasaidiwe.

Nimesema tu ufinyu wa bajeti ndio huo unaosababisha kwenda kwa wahisani na wahisani wana hiari yao. Kwahiyo, nimuombe sana Mhe. Waziri wa wizara hii kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti

hilo alishughulikie kwasababu bila ya kufanya hivyo tutapata shida siku hadi siku.

Pia Mhe. Mwenyekiti, nimshauri sana Mhe. Waziri kwamba katika changamoto hizo zilizoelezwa ukosefu wa jengo. Ofisi ni kitu muhimu sana na akiwa na ofisi yake katulia itakuwa ni nafasi nzuri ya kufanya shughuli zake kwa wakati unaofaa. Hivyo, na hili pia liangaliwe kwa maslahi ya ufanisi katika kazi zake.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nitalozungumza hapa ukurasa wa 10 Idara ya Watu wenye Ulemavu. Mhe. Mwenyekiti, tunaamini kwamba wenzetu hawa nao wamo katika umoja wao na ulemavu hauna mmoja, sote ni watarajiwa wa ulemavu kwa Mwenyezi Mungu anavyojua mwenyewe. Kwahivyo, niseme tu kwamba wenzetu hawa naomba kushauri katika changamoto zilizowekwa hapa uhaba wa bajeti na huu uangaliwe. Kutokana na hali hiyo, naomba sana bajeti yao iangaliwe kwa hali na mali kwasababu kama hatukuwawezesha bado watakuwa katika kupata shida.

Wenzetu Umoja wa Watu wenye Ulemavu wana mahitaji mengi, kuna ulemavu wa aina mbalimbali wanaotaka vigari, wanaotaka vitendea kazi vyengine, wanaotaka miwani, yaani kila mtu na alivyojaaliwa. Lakini niipongeze idara hii kwasababu Mkurugenzi wake nilimuona juzi nikampongeza sana japo kimoyomoyo ni mtu hodari kwa shughuli zake, ni mtendaji mzuri nimemlea mwenyewe nilipokuwa Mikunguni ni Mkurugenzi Mtendaji mzuri ana imani ana moyo mjasiri msichana wetu huyu. Kwahivyo, tumpe kila uwezo afanye kazi zake vizuri. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, natoa ushauri pamoja na juhudi hizo, tunao walemavu wengi katika majimbo nasemea katika Jimbo langu la Kijitoupele nitaomba ikiwa yeye mwenyewe au watendaji wake mara baada ya tukimaliza Baraza hili, namuomba sana Mhe. Waziri nimpate Mkurugenzi au watendaji wengine niwakusanye

walemavu wangu, ili awajue takwimu yao wako wangapi na nitamuhakikishia tu kwamba wote waliokuwepo wanataka huduma mbalimbali, hususan wako wengine kwenda hawawezi na mambo mengineyo ambayo yanawatokea wako kitandaji. Kwahivyo, hilo nampongeza kwa kazi nzuri.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti liko jengine ambalo limenisikitisha namba 3 ukurasa wa 11 Kesi za Udhalilishaji za Idara ya Watu wenye Ulemavu. Mhe. Mwenyekiti, suala hili ni zito nalilia sana Wizara yangu ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwasababu ndio mlengwa katika mambo kama haya. Lakini nasema tu kwamba udhalilishaji hauchagui.

Kwa maana hiyo, naomba wasaidiwe kwa hali na mali juu ya tatizo hili la udhalilishaji ambalo tunalipiga vita. Bahati nzuri tumepitisha sheria jana hapa lakini tunamgojea Mhe. Rais muda wake ukifika aiweke saini, ili itumike haraka kwasababu udhalilishaji unaumiza akili, unamuviza vichwa hatujitambui wengine kwa ile imani. Jana pia tumesikia wabakaji wamewabaka watoto hata sijui aah! Haisemeki Mhe. Mwenyekiti.

Halafu chengine Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri kwa bahati nzuri katika Kamati yangu ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii tunaye mkalimani anamsaidia sana Mhe. Zaina Abdulla Salum anafanyakazi hapa hapa usiku na mchana kila tunapokwenda na yeye yupo. Mhe. Mwenyekiti, sifichi kaomba uajiri kupitia sehemu ya watu wenye ulemavu. Namuombea sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, huyu msichana apewe kazi hiyo atatusaidia Barazani atamsaidia Mhe. Zaina Abdulla Salum atasaidia na watu walemavu wengine. Lakini baada ya ile kuwa akeshapata ule uajiri wake wa uhakika tutakuwa nae bega kwa bega katika kufanya kazi zake. Namuombae sana Mheshimiwa huyu afikiriwe.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nitalizungumzia ni kuhusu Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ na SMT na Muungano. Mhe. Mwenyekiti, wenzetu hawa wanashughulika na mambo mbalimbali hasa miradi ya *TASAF*. Kwakweli, nazipongeza serikali zote mbili kwa juhudi nzuri walizoziweka na utekelezaji wake unakwenda vizuri. Lakini natoa ushauri na hayo mambo ambayo kwa kuwa sisi watu wetu tunao katika maeneo yetu walengwa kama ilivyosema ripoti hii, walengwa halisi hawapati faida hii, kuna watu masikini sana Kaya masikini hawana uwezo, hawana kitu wanaachwa katika baadhi ya maeneo, watu wenye nguvu zao wanaweza kwenda kujituma pahala popote wanachukuliwa. Kwahiyo, naiomba wizara kupitia idara yetu hii waangaliwe watu hao, ili wenye haki za kupata haki zao wapate kwasababu hili ni changamoto kwa watu wetu ambao hawana uwezo lakini pa kwenda hawana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jengine nitakalolizungumza hapa Afisi ya Utaratibu wa Shughuli za SMZ Dar-es-Saalam. Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mkurugenzi nawapongeza na watendaji wake. Sisi tunaobahatika kwenda kwenye kamati hatujapata shida tunapofika pale anatusaidia kuanzia ziara yetu mwanzo mpaka mwisho. Kwahivyo, naomba Mhe. Mwenyekiti hapa pana matatizo kidogo jengo letu linasema uchakavu. Kweli jengo lile kama la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Afisi ile haistahiki ukienda wamejipana nafasi hawana. Lakini nasema tu kwamba mwezetu huyu Mkurugenzi na Watendaji wake wanafanyakazi nzuri wanatusaidia kwa hali na mali.

Kwahiyo, nimuombe sana Mhe. Waziri waangaliwe hawa kutokana na shughuli zake hizi nzuri ambazo anatusaidia usiku na mchana. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti niseme kuna matatizo ambayo yanajitokeza katika afisi ile bado kuna wafanyakazi wetu wa *ZBC* wanapata shida kidogo, katika jengo hawapati shida katika kazi zao wanapata shida kwa ufinyu wa lile jengo.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali kama tuko tayari tumepata maeneo mazuri bora tutafute Afisi ya Faragha kubwa zaidi kwamba watendaji wetu wa SMZ wawe kitu kimoja katika maeneo yale lakini wanafanyakazi kwa vizuri bila ya matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine nitalolizungumza hapa nimesema tu kwa jumla kwamba mimi sina matatizo makubwa sana kwa wizara hii na Afisi ya Mhe. Rais nimeipongeza mapema sina mazungumzo makubwa sana, lakini ni sehemu moja tu.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 25 Idara ya Usalama kwa Serikali *GSO*. Katika dunia yoyote Mhe. Mwenyekiti, kitengo hichi ni muhimu sana na kitengo hichi kinaitwa kitengo cha Hifadhi yaani kitengo salama kabisa. Kwahivyo, mimi naomba tu kwamba baada ya shughuli zao na tunategemea wenzetu hawa wana kazi nzito na kazi zao nazielewa mimi kwa sababu na mimi nilipatia huko huko kunako uaskari, inataka lazima uwe na mazingira mazuri ambayo mazingira yake ni salama zaidi kwa kazi zao. Kwakweli, kama nilivyosema hapa kwamba kuna mapungufu kidogo, upungufu wa bajeti, hili liangaliwe. Naiomba sana wizara liangaliwe, ili wenzetu wafanye kazi zao vizuri zaidi.

Lakini naomba mbili, uchakavu wa jengo lao wanalolitumia. Vilevile, liangaliwe kwa sababu wapate pahala pazuri na hasa nikisema tu kwamba katika kipindi cha awamu hii ya Mhe. Dkt Ali Mohamed Shein Mungu amjaalie sana maisha yake na ampe uwezo zaidi mbele anakokwenda na fikra zake nzuri. Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar imebadilika sana kwa majengo ya serikali, Afisi za Serikali zimepata majengo mazuri zina hifadhi nzuri na zinaeleweka ulimwenguni kwa sababu kila anaekuja akiikuta wizara fulani kama ya Katiba na Sheria mfano anababaika mtu hajui aanzie wapi. Ukienda majengo mengine unayakuta mazuri, ukinda kwa Mwanasheria mazuri mfano na kwengineko.

Kwahivyo, nawaomba wenzetu hawa wapatiwe Afisi ambayo inakwenda na wakati tuliokuwa nao. Lakini pia vitendea kazi ni kitu muhimu sana, bila ya vitendea kazi Mhe. Mwenyekiti, watakuwa hawana uwezo wa kufanya yao. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nazipongeza wizara zote mbili nampongeza Mwenyekiti wa Kamati, nawapongeza wote, nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutuweka vizuri, nampongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kutuelekeza vizuri na kuwaelekeza mawaziri wote na sisi Wawakilishi kwasababu hichi ni chombo ambacho anatuongoza yeye mote humu.

Kwa hivyo, tumpongeze, tumpe nguvu na naomba wenzangu waichangie ripoti hii kuzipa nguvu wizara hizi kuu kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu na watu wetu. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ali Suleiman Ali kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Shehe Hamad Mattar akifuatiwa na Mhe. Simai Mohammed Said na Mhe. Machano Othman Said ajiandae.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwanza kunijaalia afya njema na wewe nikushukuru kuweza kunipa nafasi hii na namuomba Mwenyezi Mungu aniwezeshe niweze kuchangia vyema na hatimae na mie niunge mkono ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya wote kwanza kama nilivyotanguliza kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumtakia Mtume wetu (*SAW*) Rehema na Amani ziwafikie na katika ripoti hii niendelee kuwapongeza Kamati inayosimamia Afisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi. Kazi iliyofanywa humo ni

kubwa sana ripoti nimepata muda wa kuipitia vizuri kwanza naunga mkono mia juu ya mia kabla sijaendelea. (*Makofi*)

Kuunga mkono kwangu, nitaongeza nyama tu kidogo kwa baadhi ya mambo lakini ripoti ni nzuri imegusa kila pahali wamefichua mambo mengi. Kwahivyo, tutegemee wizara zetu hizi zitakuja kuleta majibu na maelekezo ambayo yametolewa kuyafanyia kazi.

Vilevile, niwapongeze viongozi wakuu ambao wanasimamia wizara hizi akiwa ni Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Idd na akifuatiwa na waziri wake Mhe. Mohammed Aboud Mohammed pamoja na Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambayo kuwa Waziri wake ni Mhe. Issa Haji Ussi Gavu simsahau kiongozi mkuu ambaye kuwa ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt Ali Mohamed Shein. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti hii mimi naenda moja kwa moja katika ukurasa namba 9 unaozungumza masuala ya Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa. Kwakweli, nimeisoma ripoti hii na kuona kuna mambo muhimu sana. Kwanza ningeomba waziri atakapokuja baadae kutoa taarifa hii atupe hasa hii tafsiri ya maneno hii ya "maafa". Hii neno maafa maana urefu wake ni ipi pengine atakapokuja na wananchi wataelewa ni lipi maafa na lipi janga na wao wakaweza kujijua winapotokezea wakajua hili lin muelekeo upi.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kutoa mchango wangu katika suala zima la hii kamisheni katika ukurasa wa kwanza unaposema kwamba kamisheni imepanga mipango ya kukutana na jamii katika kuekeleza hatua nzima inapoona kwamba inafanya vipi shughuli zake. Pamoja na malengo yake yaliyojipangia kamisheni nashauri hivi katika kutoam taarifa ni vipi wananchi waweze kuitumia kamisheni hii basi taarifa itumike kwa vyombo vya

habari, redio na *television* kama inavyoendelea lakini pamoja na masheha.

Mhe. Mwenyekiti, hawa masheha ambao kuwa tunawapa taarifa na taaluma wasibakie nazo vifuani mwao. Hawa Masheha ni watu muhimu sana katika majimbo yetu ambayo wataweza kukaa na wananchi wao kwa makundi wanayoyajua wao kuipa taaluma hii. Kwasababu inapotokezea janga au maafa mwananchi atajua nini nifanye, baada ya kukaa akaduwaa katika sehemu huku ana msiba wa mambo yametokezea hajui afuate wapi na aende wapi. Mhe. Mwenyekiti, hili naomba sana masheha wale ambao wanapewa taaluma zao kutoka kwa wizara husika au kamisheni na wao wasibakie nae waipeleke kwa wananchi wao.

Lakini jengine niendelee katika suala zima la changamoto walizozionesha hapa changamoto zipo na mimi kwa kweli nazikubali changamoto zilizopo hapa.

Changamoto ya kwanza inategema fedha za maendeleo kutoka kwa wahisani. Mhe. Mwenyekiti, hili ni janga linapotokezea au maafa yanapotokezea kwakweli hayasubiri muhisani ni vyema sana suala hili tukalipa umbele sisi wenyewe kwanza kwa kutenga fedha maalum kama vile tunavijiwekea majumbani kwetu kwamba piga uwa lakini kiasi fulani zibakie angalau ikitokezea mtoto kuumwa au ikitokea dharura tuweze kuzitumia. Sasa na sisi serikali ni vyema tuweke mfuko wetu maalum baada ya kutegemea wahisani, wahisani hata wakija watakuja kusaidia wanasema watu "ukingoja maiti unangoja ukilia".

Kwahivyo, na sisi tutumie fursa hii kujitengea sehemu yetu wenyewe kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali hii ikae kwa kusubiri itakapotokezea haikutumika kwa mwaka ule basi itaendelea kwa mwaka mwengine. Hili jambo nashauri sana katika changamoto zilizipo hapa.

Vilevile, suala la ufinyu wa bajeti. Suala la ufinyu wa bajeti ni vyema kwamba Wizara ya Fedha katika kupanga mipango yake nayo ndio vile vile inakaribiana na eneo lile lile la kutenga fedha maalum. Suala zima la ukosefu wa afisi ambapo kwa sasa kamisheni inategemea jengo la Kituo cha Huduma za Dharura. Afisi ni muhimu sana Mhe. Mwenyekiti, kwani kuwepo kwa afisi au jengo ambalo kuwa Kamisheni itakuwa na mamlaka wa kuweza kulitumia na kwa upana ndipo shughuli hizo ambazo zitaweza kuratibiwa mara baada ya mara zitakapotokezea.

Mhe. Mwenyekiti, changamoto ya nne iliyopo hapa kuchelewa kupata *vote* suala la *vote* kwa vile tumeamua kuiweka kamisheni kwani kuna ugumu gani Wizara ya Fedha kuweza kuipa *vote* hii. Mimi nashauri kwamba kwa vile tumeshaipa nafasi ya ukamisheni hii ni eneo kubwa basi nashauri sana Wizara ya Fedha na Mipango iweze kutoa *vote* na wao wapewe fedha waweze kujiendesha na watu wa mahesabu wapo wengi hapa tuwaajiri waweze kutumia kamisheni hii ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye ushauri ambao kubwa wametoa kamati na mimi naongeza katika ushauri, kamati inashauri masuala mazima ya kupatiwa sehemu ambayo inapotokezea majanga kuweza kupata maeneo muhimu ya kuweza kuyatumia. Kwakweli suala la maeneo ya kuweza kulitumia ni muhimu sana katika inapotokezea majanga katika nchi yetu. Lakini hii inatuwia vigumu pale tunapojenga kiholela leo utakuta ni sehemu chache ambazo kuwa kutokana na ujenzi wa kiholela huwezi kusema kwamba leo imetokeza janga la moto au la upepo tuwachukuwe wahanga hawa tuwaweke maeneo ya karibu inabidi tupate tabu sana sana. Kwahivyo, serikali katika mipangilio yake ni vyema katika maeneo ya wazi waendelee kuyadhibiti, baada ya kuwa wengine wakiyanyemelea wakianza kuyajenga majumba yao. (*Makofi*)

Nashauri sana katika eneo hizi za majengo au Afisi za Kamisheni hizi zinazohusiana na maafa ziweko katika kila mkoa kwa kuanzia tuanzie kila mkoa angalau kuwe na afisi zake zinazohusiana na maafa na baadae tutakuja hali itakaporuhusu tushuke katika wilaya hadi shehia. Lakini, linapotokezea jambo hili tuwe wepesi kulifatilia baada ya kungojea kamisheni mpaka ifike. Ni vizuri sana kuwa na maeneo yetu ofisi hizi katika ngazi za mikoa kama hazipo nashauri sana ziwepo.

Mhe. Mwenyekiti, niende sehemu ukurasa wa 10 sehemu Idara ya Watu wenye Ulemavu. Naomba kuchangia kwenye sehemu hii kuhusu changamoto zilizopo. Hapa wameonesha changamoto mbili. Mhe. Mwenyekiti, naona niongeze changamoto nyengine iliyopo hapa kuhusu vifaa vya watu wenye ulemavu. Watu wenye ulemavu wanakuwa ni wengi siku hadi siku na sote ni walemavu watarajiwa, kwa kweli katika Mkoa wangu wa Kaskazini Pemba hawapungui watu 2300 na kuendelea kwa takwim za haraka haraka hao ni walemavu waliomo katika Mkoa wa Kaskazini Pemba, na ukiangalia watu hawa wanhitaji mahitaji mbalimbali zikiwemo baskeli za maringi matatu, miguu ya kuendea, wengine hawana macho, wengine wanahitaji viungo muhimu hawana.

Kwahivyo, niombe sana wizara inayohusika pale inapofanya juhudi kutafuta vitu kama hivi basi wavigawe mpaka Mikoa yetu y Kaskazini na Kusini Pemba isiishie Makao Makuu tu Zanzibar. Vitu hivi niombe inapotokezea vifaa kama hivyo tunaomba kwa wenzetu wahisani wafanye juhudi kubwa kuvitafuta vitu hivi wasingojee mpaka watunukiwe wajaribu kuwaomba wenzetu ambao kuwa wana uwezo vitu kama hivi. Kwasababu tunajua kwamba baskeli ya maringi matatu ni ghali kwa masikini mnyonge hawezi haipungui shilingi laki nne baskeli moja.

Mhe. Mwenyekiti, ninazo kumbukumbu katika jimbo langu ndani ya nyuma mmoja kuna walemavu wanafika wanne ndani ya nyumba moja ataweza mtu masikini kama huyo baba mlemavu, watoto walemavu ataweza kuhudumia vipi. Kwahivyo, kweli kama itakuwepo vyombo kama hivi katika taasisi hii itaweza kutusaidia sisi Waheshimiwa kule katika majimbo yetu kuona kwamba tunatekeleza vipi kero zao majimboni mwao.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika suala zima la Baraza la Wawakilishi. Katika ripoti hii imeelezwa hapo kuna changamoto tunaoneshwa hapa ni changamoto moja tu iliyopo kuwepo kwa marejeo ya sauti katika *echo*. Hili ni tatizo kubwa sana na kwa muda mrefu toka tuingie katika Baraza hili linazungumziwa hili. Lakini kuna suala zima la miundombinu, tumekuwa tukizungumza suala la miundombinu ya watu wenye ulemavu haipo.

Naomba sana hili suala lipewe kipaumbele. Leo hapa watu wenye ulemavu wakiwa wanataka kuingia Barazani ni shida wakiwa wamekuja kusikiliza Baraza ni shida. Kwahivyo, suala hili tuliangalie kwa upeo kwa nguvu kubwa sana tuone kwamba tunalitelekeza vipi katika Baraza letu la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika masuala mazima la Idara ya Sherehe ya Maazimisho ya Kitaifa. Hapa niipongeze sana Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais pamoja na vyombo vyote ambavyokuwa vimeshirikiana na kamati zake katika kufanikisha Sherehe za miaka 54 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ambayo kuwa yamefanyika hapa *January* iliyopita. Vilevile, niwapongeze viongozi wakuu ambao kuwa wamesimamia shughuli hizo. Lakini, hapa nina ushauri, sherehe hizi tunazofanya kila mwaka kwanza suala zima la kuwanze viongozi wakuu wa kitafa liendelee kuwepo kila mwaka lakini suala zima la kufanya sherehe zile kubwa basi naona tufanye rai kuzipunguza.

Tufanye kila mwaka kuna suala la kuazimisha tunaweza kufanya shughuli nyengine mbalimbali ndogo ndogo, lakini kama miaka miwili mwaka wa tatu tukaweza kufanya shughuli kubwa kama vile wenzetu tunaona baadhi ya nchi zinafanya.

Shughuli hii itakuwa ni kubwa itabeba mambo mengi watu wataweza kujionea na kumbukumbu mbalimbali pale tutakapoifanya baada ya miaka mitatu, kwa nini nikasema hivyo, kwasababu sherehe ni sherehe hakuna sherehe ndogo inabeba fedha nyingi sana fedha hizi ambazo kuwa tungeweza kuzifanyia kila mwaka miwili hii tungeweza kuondoa matatizo yetu katika majimbo ambayokuwa yana matatizo mengi kuhusiana na maji na mambo mengine. Kwahivyo, natoa ushauri sana serikali suala hili tuliangalie kufanya baada ya mwaka wa tatu ndio tukafanyua sherehe kubwa.

Mhe. Mweyekiti, niende katika suala zima la Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika suala zima la ushauri uliopo kupatiwa ofisi iliyoko Pemba, ofisi iliyopendekezwa hapa kwamba Ofisi ya Rais Katiba Sheria na Utawala Bora iliyoko Pemba kupewa katika sehemu watu wa Makamu wa Pili wa Rais. Kwakweli, ushauri wangu nasema ofisi ambayo kuwa inahitajika kupewa watu hawa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuuongeza maeneo basi wapewe katika majengo pacha matatu pale ya Gombani.

Kwa vile ofisi zile mwanzo zilitakiwa zijengwe ghorofa mbili lakini zikaongezwa tena ghorofa tatu, basi itafutwe sehemu katika jengo hili ambayo itakuwa na hadhi ya ofisi kama hii iweze kupata nafasi pale. Kwasababu jengo hili la Katiba na Sheria na Utawala Bora lilioko hivi sasa wenyewe ni bovu. Tukiaanza kuwaweka mule suala la kulitengeneza tutacherewa sana ni vyema tuweze kuwaweka jengo jipya katika majengo pacha yale tutafute sehemu moja iliyo nzuri ambayo itakuwa na hadhi na ofisi

yenyewe tuwaweke hata kwa muda baadae kama tunataka kutumia ofisi iwe tayari imeshafanyia matengenezo makubwa huu ni ushauri wangu.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu ushauri mwengine kamati imeshauri Wakala wa Serikali wa Uchapaji kujenga miundombinu bora katika ofisi zake za Pemba, ili kuiwezesha taasisi hiyo kufanya kazi kibiashara na serikali kupata mapato zaidi katika eneo hili. Ni kweli ofisi ya uchapaji iliyopo Pemba ya uwakala wa uchapaji haiku vizuri sana na mimi naifahamu ni vyema itafutiwe sehemu nyengine, ili iwekwe katika hali nzuri iwepo kibiashara zipo shughuli ambazo ingeweza kufanya kibiasha na serikali ikaweza kupata mapato kama vile inavyopata hapa Zanzibar.

Niombe sana serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais katika kitengo hichi cha uchapaji nacho wakeweze kukifanya kiweze kutia tija katika ofisi yetu iliyopo Pemba. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naendelea tena kuunga mkono mia juu mia kwa mchango wangu huo na maoni yangu hayo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Shehe Hamad Matar kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe, naomba niwakumbushe kuwa hoja iliyokuwepo menzani ni hoja ya kamati na sio ya serikali. Kwahivyo, naomba sana Waheshimiwa Wajumbe na hoja hii Serikali kwa leo haitatoa majibu mpaka katika mkutano wa mwezi wa Septemba nilikuwa naomba niwakumbeshe hilo. Sasa naomba nimwite Mhe. Simai Mohammed Said atafuatiwa na Mhe. Machano Othman Said na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf ajiandae.

Mhe. Samai Mohammed Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwa kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika ripoti hii ya Kamati

ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza hili la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze pia kwa kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu wao ndio ikiwa mimi ni sauti yao mtetezi wao, msemaji wao katika chombo hichi, basi na mimi niseme pia nitaendelea kuwapenda na kuwajali na kufanya kazi yangu kwa kadiri ninavyoweza katika kutimiza wajibu wangu katika Baraza la Wawakilishi kwa mujibu ya Katiba ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwanza ofisi zote mbili hizi ni ofisi kweli kuu kabisa na zinatuongoza katika maeneo mengi wananchi wa Zanzibar, lakini pia zinatupa dira na mwanga kwa maeneo ambayo wapi Zanzibar inataka iende na wapi tufike. Kwahiyo, nianze kwa kumpongeza sana Mhe Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri ambayo amekuwa anaifanya katika kuwaongoza wananchi wa Zanzibar, pia kwa kuleta hali ya amani, umoja, upendo, utulivu katika visiwa vyetu kwa njia moja au nyengine pia kuimarisha umoja na Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Lakini pia nichukue nafasi hii pia kumpongeza jembe letu Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi, kwa kazi nzuri pia naye anayoifanya ya kusimamia serikali pamoja na kusaidiana na kushirikiana pamoja na wizara zote husika na *Inshallah* Mwenyezi Mungu anampa umri mkubwa pamoja na afya njema ili aweze kuyafanya yote. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja nitakwenda kwenye mchango wangu, nitajitahidi sana kupunguza pongezi, kwasababu naamini pongezi ambazo zitakazotolewa na mimi tayari nishazitoa zitakuwa tayari zinakuwa zina umoja. Mhe. Ali Suleiman Ali amepongeza sana kwa hivyo, basi nitakaa katika mgongo wake

kwa pongezi zile na mimi naziunga mkono zote. Sasa nitakwenda kwenye hoja ambayo ipo mbele yangu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niishauri serikali pamoja na Ofisi ya Rais, na Mhe. Waziri ambaye anasimamia katika Ofisi ya Rais kuwa mara nyingi tunasikia Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameteuwa wenyeviti wa bodi au mabaraza ambayo yanasimia kwenda kuyaongoza katika wizara husika.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, ukifuatilia kwa undani katika haya mabaraza au hizi bodi unakuta kuna bodi nyengine hawa wenye viti ambao wameteuliwa na Mhe. Rais wanazidiwa madaraka yao na wajumbe wengine wa bodi. Sasa nataka niishauri serikali pamoja na waziri ambaye anasimamia Ofisi ya Rais yupo hapa, hivyo nitampatia baadaye majina ya bodi ambazo zinanitia hofu na kwamba wajumbe ambao wanashiriki kwa njia moja au nyengine katika bodi hizi, wanang'ang'ania au wanajaribu kuyafunika yale madaraka ambayo mwenyekiti ameteuliwa katika kuishauri wizara au sehemu husika.

Sehemu nyengine, ambayo nataka niizungumzie ni suala la madawa ya kulevya nigusie tu kwasababu nishazungumza sana. Mhe. Mwenyekiti, nataka niishauri serikali katika upande wa *airport* na bandari, kutoka eneo ambapo mgeni anapotua na kuingia na mabegi yake, basi pale pana *camera* anaangaliwa tangu anashuka, anapotembea, anapopekuliwa anapopita *immigration* mpaka anapotoka nje na anapopanda gari. Mhe. Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi, juzi hapa tumepitisha Sheria za Jinai hapa tafauti zetu zote na sheria hizi zitakuwa zinaenda sambamba katika mfumo mmoja hasa katika suala zima la madawa ya kulevya.

Kwahiyo, jambo moja ambalo limepita ni ushahidi wa *electronic* kwa hivyo, hatuwezi kuwa tunaendesha *airport* ambayo mgeni

anatua yupo katika ile *apron* kwenye *terminal II* ambayo imejengwa lakini mgeni anaposhuka begi lake ukuta wa nje upo karibu, anapanda katika basi anachukuliwa anauwezo wa lile begi kuliacha ndani ya basi na ule mzigo ukatolewa nje, huu ni ukweli kabisa. Kwakweli, mabasi wayanoendeshwa kupakia wageni ni mabasi ya kawaida, sasa usalama wa wananchi wa Zanzibar katika kupambana na hili janga la madawa ya kulevya linahitaji pia nguvu ya ziada.

Mhe. Mwenyekiti, zipo njia nyengine ambazo tunatakiwa tuziangalie sana. Kwahivyo, nashauri nasuala ya *camera* sasa iwe siyo tena wimbo wa taifa tufanye tena kwa kazi hii mara moja, ili ambayo yale ambayo Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais anayoyazungumza basi tuweze kumsaidia katika na sisi katika kutekeleza adhma hiyo.

Jengine nataka niulize suala *Diaspora*. Mhe. Mwenyekiti, *Diaspora* tumekuwa tunaimba na tumekuwa tunazungumza kwa muda mrefu sana sasa hivi, lakini leo ni ukweli *Diaspora* hawa Wazanzibaari wanao *Diaspora* ishi nje wakingia *airport* wanalipa viza ikiwa ana *passport* ya Ulaya atalipa dola 50, ikiwa ana *passport* za nchi kama Marekani atalipa dola 100. Lakini huyo *Diaspora* tunamwambia njoo Zanzibar uje kuekeza au uje kutumia utalamu wako lakini hadi leo akitaka kuishi hapa anatakiwa alipe *resident permit*, na hiyo *resident permit* ni dola elfu mbili na hamsini sasa hebu tujiulize kuna tafauti gani baina ya *Diaspora* na yule raia wa kigeni ambae tunataka kutumia utaalumu wake kuja kuishi Zanzibar.
Kwahivyo, aidha tuamue moja *Diaspora* tuwaite ni *Diaspora* lakini pia *non citizen* kwasababu tanawaita tunawatambua lakini hawa bado hatujaweza kuwafikia kuwapa ile hadhi ambayo iliyokuwepo. Hatuwezi kumwambia mtu Mzanzibari tanakutambua lakini anapofika *immigration* analipa dola hamsini ya kuingia ndani inawauma sana.

Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani mtu ambaye ana familiya yake anakuja huku na dola zake laki tano au milioni moja aje kuziekeza Zanzibar tunamwambia alipe dola elfu mbili na hamsini. Sasa kitu gani kinamtofautisha baina ya mwana *Diaspora* na raia wa kigeni anayefanya kazi ya hoteli shamba. Hivyo, ninachokiomba kwanza tuangalie hilo, ili kuweza kuwaondolea kuwaonesha na sisi ndani ya serikali yatu ndani ya nchi yetu kwamba tunawajali na hichi ndicho kitakuwa cha kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, hata binaadamu unapokwenda kuposa huendi saa nne asubuhi unakwenda saa kumi jioni baada ya Laasiri, baba mwenye nyumba ameshakaa, ameshasali, ameshakula chakula chake cha mchana na amepumzika, kwasababu mazungumzo yatakwenda vizuri haiwezekani hawa watu wa *Diaspora* wanakuja hapa Zanzibar, tunawaambia tunawataka waje halafu pia zaidi ukiangalia pia tunahitaji utaalamu wao kuna kasoro kubwa sana tunahitaji hawa tuwatumie katika maeneo muhimu hasa katika masuala ya TEHAMA.

Lakini pia, kuna wakandarasi wazuri sana ambao wanatakiwa waje hapa waunge mkono na kuna mapungufu leo Zanzibar tunaangalia miradi mikubwa inafanyika na hawa Wazanzibari wanaoishi nje wapo na wapo tayari kuja. Sasa sisi tuangalie utaratibu wetu najua kuna mambo tunagusa ndani Jamhuri lakini naamini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mkono mrefu, pale wanahisi kwasababu ukiangalia chumi zetu sisi ni mbili baina ya Zanzibar na Tanzania Bara ni chumi mbili tofauti.

Sisi Zanzibar ni *service oriented* na wenzetu wao wana *ago-business* wana *telecom, banking, mining, oil and gas* pamoja na mambo mengi sana. Kwahivyo, sisi lazima tuangalie pale maeneo ambayo sisi yataweza kutusaidia ambayo tunaweza kuboresha

kwa upande wetu sisi wenyewe, ili tuweze kuwasaidia na hawa Wazanzibari wote tunawowazungumzia wapo tayari.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Mwenyekiti kupitia kwako watakapokuja hapa watusaidie sana hili, katika bajeti yetu ya mwaka huu tuangalie utaratibu mpya wa kuweza kuwasaidia na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iweze kuonyeshea mkono mmoja wa upendo, ili na wao wapate afueni. Aidha, niunganishe nguvu pia ielekezwe katika vikao na mambo yote yanayohusiana na masuala ya Afrika Mashariki na Kati, hasa *EAC* zile faida za wananchi vikao tuletewe pia tupate kueleza zaidi.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu ziara ya Mhe. Rais Arabuni. Mhe. Mwenyekiti, katika jambo lililonifurahisha katika utawala wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika miaka hii minane (8), basi ni hii ziara aliyoifanya katika Falme za Kiarabu alipoenda nafikiria Abudhabi, Ras-el-Khaima, Dubai na Sharja pia katika hizi nchi saba za *UAE*. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein, amepokelewa nafikiria si dhani kama kuna kiongozi wa Afrika au katika Bara la Afrika amewahi kupokelewa katika nchi za kiarabu kama Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwakweli ilikua ni sifa kubwa sana kwa Wazanzibari, halafu kilichonifurahisha zaidi ofisi yake sasa hivi jambo lolote ambalo Mhe. Rais sasa anafanya tunapata katika mitandao ya kijamii, picha *clip* ya *video* na kila mwenendo anaofanya Arabuni tulikuwa tanauona. *(Makofi)*

Halafu pia nimefurahi kitu chengine zaidi mavazi aliyokuwa amevaa amekuwa amependeza amevaa suti nzuri ukiangalia yeye

pamoja na wote waliofatana naye, mmoja aliyenivutia pia ni Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Juma Ali Khatib) nilikuwa namfatilia juu mavazi yake, pamoja na pozi alivyokuwa anakaa utafikiria yeye yupo katika Umoja wa Mataifa. Kwahivyo, nawapongeza viongozi wote waliokwenda katika hii ziara. *(Makofi)*

Vilevile, nataka nizungumze pia Sherehe za Mapinduzi. Mhe. Mwenyekiti, Sherehe za Mapinduzi zimekuwa zinakuwa kwa haraka tena kwa ubora ni nzuri na ushiriki wa wananchi umekuwa ni mkubwa zaidi. Naomba sana katika maeneo yafuatayo tuanze kuyazingatia. Eneo la Maisara au pale katika viwanja ambavyo vinafanyika waanze kuweka *lost and found* kwasababu watoto wanaokuja ni wengi sana pawe na Kituo cha Polisi pia kidogo na kiwe kimetangazwa mapema kabla.

Mhe. Mwenyekiti, pia papatikane huduma za kuweza kujisaidia kwa wananchi ikiwa ni *temporary* au itajengwa *permanent* kwa upande wa baharini kule siwezi kujua, lakini wazingatie hayo yote kwasababu wananchi wanaojitokeza ni wengi sana katika kuunga mkono Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964. Kwakweli, yale yote ambayo yanafanyika pale yanakuwa na mvuto mkubwa.

Aidha, nataka nishauri katika suala zima la *firework* au fash fash. Mhe. Mwenyekiti, fash fash zinakwenda vizuri lakini hizi fash fash sasa tunakwenda nazo zinaweza zikaboreshwa kwa njia pana tu au kubwa zaidi. Mhe. Mwenyekiti, nashauri serikali iangalie upande wa kuanzishwa mfumo wao wenyewe wa kuiagizia kutoka nchi za nje na kuleta utaalamu ambau utakuwa ni bora zaidi, aa! Sasa hivi hizi ni nzuri lakini wananchi wanaanza kuzizoea, ukiangalia rangi zake, sehemu zinazofika, na mazingira yote kwa ujumla basi tunaweza kuja na mfumo mpya kila mwaka ili

manjonjo yakazidi kuongozeka na wananchi wakapata burudani ya kipekee katika kuyaenzi Mapinduzi yetu matukufu.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nataka nende katika masuala ya UKIMWI Mhe. Mwenyekiti naomba sana elimu pamoja na kuwasaidia wananchi kupunguza haya maambukizi yazidi kuimarishwa zaidi, aa! Tusilale, vijana wetu bado wanahitaji nguvu ya kujenga uelewa mkubwa zaidi hasa katika maeneo ya maskuli, mkusanyiko tofauti, na maeneo ya vijijini na mashamba hasa katika kisiwa chetu cha Pemba pamoja na katika Mkoa wetu pia wa Kusini na Jimbo langu la Tunguu.

Kwahivyo, naomba sana kuwe kuna ziara zinafanyika za kila baada ya muda, ili wananchi waweze kuuliza masuali yao ipo wakati mwananchi anaweza kuangalia au kusikiliza taarifa katika vyombo vya habari, lakini wakati mwengine anapopata mtaalamu anakwenda katika vijiji anatulia halafu wananchi wanakuja kuuliza zile taatifa na kujenga uelewa mkubwa zaidi ni vizuri. Hivyo, ni vyema hizi zifanyike kuwe na matembezi aidha kupita na gari katika mwaka katika vijiji *throw of the year* zisifanyike tu kila baada ya mwaka mara moja aa, iwe ni ratiba ambayo wanakwenda maeneo yote.

Eneo jengine nataka nichangie ni Baraza la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Wawakilishi ni zuri jengo letu lakini kwa hali tunalokwenda nalo litakuwa *out of date,* sehemu moja ambayo tuna changamoto ni ya waandishi wa habari. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kama sasa hivi mimi ninachangia hapa inawezekana pengine kuna waandishi wamekaa katika *gallery* kama kwenye lile Bunge la Jamuhuri ya Muungano kule wananiona kwa mbele napigwa picha naonekana na wajumbe wote hata Mawaziri pia, lakini kila ukisoma magezeti hapa au vyombo vya habari unakuta picha zipo kwenye migongo yetu,

kwasababu hakuna njia ya kuwafikia Waheshimiwa Wajumbe au Waheshimiwa Mawaziri wanapochangia.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia mfumo wa ukumbi wetu una changamoto zake. Hivyo, natoa ushauri kutokana na mazingira ya jengo hili serikali itafute njia mbadala pamoja na Ofisi ya Spika, kujenga jengo jipya ambalo litakuwa lina *long term* kama itakuwa ni maeneo yetu kwenye kiwanja chetu cha Fumba na jengo hili linaweza kutumika vizuri sana na serikali katika miaka ya baadae. Ukiangalia lina *parking* za kutosha na ukumbi kama huu unaweza ukatumika, lina vyumba vya ofisi vya kutosha na katika ukumbi mpya utakojengwa basi ninaamini kila Mwakilishi wa Unguja na Pemba atakuwa na ofisi yake ya kuweza kutimiza majukumu yake na kuonana na wananchi na pia kufanya kazi zake za kila siku.

Vilevile, nashauri pia Ofisi ya Makamu wa Pili ya Rais, tukiangalia kwa mazingira yalivyo, ofisi yake sasa inakuwa ni ndogo ukiangalia haina *parking* ya kutosha ina *department* nyingi sana, ukiangalia kama itawezekana kwasababu kazi yangu mimi kama Mwakilishi ni kuishauri serikali. Kwa mfano, wanaweza wakafanya *switch* au kubadilishana baina ya Ofisi ya Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo halafu kama waangalie, kwasababu ukiangalia leo Makamu wa Pili wa Rais akipokea wageni zaidi ya hamsini hawezi kukutana naye katika ofisi yake inabidi ahame. Lakini ukiangalia wizara kama ile pale majengo yalivyo yanaridhisha.

Kwahivyo, tujitahidi sana kuangalia uwezekano wa Makamu wa Pili wa Rais, awe ana uwezo katika mazingira ya jengo lake kuonana na watu wote, ili aweze kufanya kazi kwa utulivu, kwasababu yeye ni kiungo muhimu sana katika nchi yetu na tumuonee huruma kwasababu anafanyakazi nyingi. Kwahivyo, jengo lake linahitaji kuwa na mazingira na maboresho yote. *(Makofi)*

Nikirudi katika Baraza la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, naishauri sana serikali tuangalie kwenda katika mfumo wa *digital*. Leo ukiangalia Baraza letu unapotaka kukaa hapa kufanya *research* yoyote, hatuna uwezo wa kuangalia kwenye simu, hatuna compyuta ya kufanya *research*. Nikitaka kuangalia leo Japan kumetokezea nini sina chochote cha kuangalia hapa. Kwa hivyo, niombe sana kwamba tayari tunaweza kulipeleka Baraza letu likawa katika mfumo wa *digital* ili tuwe na taarifa za kutosha. *(Makofi)*

Nina dakika ngapi. Tano Mhe. Mwenyekiti. Ahsante. Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nichangie

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, muda wako umekwisha naomba umalizie.

Mhe. Simai Mohamed Said: Muda wangu umekwisha. Naomba dakika tano Mhe. Mwenyekiti, nimalizie.

Mhe. Mwenyekiti: Nakupa dakika mbili.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nashukuru. Nakujua mara unanitoa nje. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, maafa. Katika suala la maafa nataka nishauri vitu viwili. Tunapozungumzia maafa tunaangalia katika hali ya tabia nchi, mabadiliko ya hali ya hewa mvua na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, jana nafikiria kuna Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi walifungua Dawati la Afya, ambalo hili litakuwa katika masuala yanasimama katika *Water Board Disease* na ipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwahivyo, naomba sana Ofisi ya Makamu wa Pili walifuatilie sana hili

dawati lifunguliwe Zanzibar, kwasababu tunapoangalia maafa tusiangalie katika masuala ya majanga ya upepo na mvua. Ukiangalia katika maeneo ya mjini sasa hivi kuna panya na paka wengi. Mji wa Uingereza London uliwahi kuchomwa moto kwa sababu ya *plague*.

Kwahivyo, ukiangalia leo masuala kama haya ya panya na takataka nyengine tuhakikishe kwamba elimu inatolewa ya kutosha, usafi unaimarishwa, ili tuhakikishe miji yetu hatupati majanga haya yanayokuwepo. Hata ukiangalia leo mwezi huu wa Januari ukiangalia hali ya hewa ilikuwa ni tofauti na mwaka jana wenye upepo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana pia katika masuala ya Muungano Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tulipata fursa. Namalizia Mhe. Mwenyekiti. Basi japo mawaziri wanaosimamia katika sekta tofauti za Muungano na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuweze kuonana nao. Mimi jimboni kwangu ukiangalia kule nina kambi za jeshi, nitafurahi tukipata kumuona Mhe. Waziri wa Ulinzi, ili kuleta umoja wetu na yale ya kwetu pia waweze kutusikia.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa fursa uliyonipa na nikushukuru kwa muda ulioniongeza, nasema ahsante sana nawashukuru Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikiliza, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nakushukuru Mhe. Simai Mohamed Said kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Machano Othman Said, atafuatiwa na Mhe. Nadir Abdul-latif na Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis ajiandae.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi

Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima mchana huu wa leo na kuweza kuipokea ripoti hii.

Pili Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii kuwa mchangiaji wa nne wa ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi.

Aidha, Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe nafasi hii kumpongeza sana Mwenyekitiwa Kamati Mhe. Omar Seif Abeid pamoja na timu yake yote. Wamejitahidi wameandika ripoti nzuri ambayo imejadilika, lakini pia inaweza ikaleta tija zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ofisi hizi mbili ni ofisi za viongozi wetu wakuu. Kuna Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kabla ya kuzungumza lolote naomba niwapongeze viongozi wetu hawa wakuu wa nchi kwa uchapakazi wao. Kwakweli, ilivyoingia tarehe 30 Mei nafikiri baada ya uchaguzi ule, tulipoapa na kuja Barazani huko nje kulikuwa kuna maneno mengi sana ya wiki, wiki mbili, wiki tatu, lakini hatimaye sasa tumeshapitisha bajeti mbili na tunaelekea kwenda mbele keshokutwa bajeti ya tatu na tunatarajia Chama Tawala CCM kitaendela kuwa kinaongoza mpaka mwaka 2020 kwa awamu hii, tutaendelea na viongozi wetu hawa na bila shaka kila mtu anaona sasa hali ikoje. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nianze na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, pamoja na kumpongeza kwa utendaji wake na wasaidizi wake Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Rais, na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili, Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wao. Lakini ninayo maoni kwa ripoti hii ya kamati, ambapo kwa kupitia mwenyekiti naomba serikali iyafanyie kazi.

Kwanza nianze na Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Mhe Mwenyekiti, ripoti imeeleza vizuri tu changamoto na hali halisi ya tume hii. Lakini nataka niseme kwamba bado nguvu za ziada zinahitajika katika kupambana na madawa ya kulevya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, sisi humu ndani Waheshimiwa Wajumbe mlituchagua baadhi yetu kwenda Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Miongoni mwa changamoto ulikuja Mswada wa Madawa ya Kulevya na wengi wa wajumbe, ukiwacha viongozi, walikuwa na hofu sana na hali ya madawa ya kulevya kwa Zanzibar, na walisema kwamba hebu hii sheria ya huku itumike mpaka huko, lakini wenyewe tulikataa tukasema hili sio jambo la Muungano.

Sasa kwasababu sio jambo la Muungano na kwa kuwa Zanzibar tuna Tume yetu ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya, niombe juhudi zaidi ichukuliwe ili iweze kupambana na madawa. Kwanza bado tunahisi kwamba waletajiwa madawa ya kulevya hawajeweza kudhibitiwa na kukamatwa, wakamatajwi ni watumiaji wa madawa ya kulevya. Lakini hawa wanokamatwa sio wanaoingiza nchini na kama waingizaji wapo, kwa nini hawakamatwi na kama hawapo dawa zisingeingia Zanzibar. Kwahivyo, tunaiomba serikali tunaiamini na tunaipenda serikali yetu, hivyo wajitahidi hili lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwasababu kamati imeeleza kwamba hata vielelezo vya kesi vinapotoea vinakuwaje vipotee, ile sio sindano kwamba shindano ni ndogo imepotea au kifungo, na kwa kuwa tumefikia hatua hii ndio inaonekana Zanzibar ni chochoro ya kupitishia madawa ya kulevya.

Kwahivyo, tunaomba Mhe. Mwenyekiti, Mwenyekiti wa Kamati wamesema na tunaiomba serikali ijitiahidi hivi sasa. Miaka ya

nyumba madawa ya kulevya ilikuwa kama tatizo ndani ya Manispaa ya Mjini Unguja, lakini sasa hivi tatizo hili limekuwa kubwa hata katika majimbo yetu ya shamba lipo, Pemba lipo. Zamani ilikuwa wanaokamatwa na madawa ya kulevya au watumiaji ni wanaume, sasa hivi mpaka wanawake tena ni wengi kweli. Kutokana na hali hiyo, bado tunayo kazi ya kufanya kuhakikisha kwamba tatizo hili linakaa sawa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jambo la pili nataka kuzungumzia Tume ya Uchanguzi. Kwanza niipongeze Tume ya Uchanguzi, kwa miaka yote wamekuwa wanafanya kazi nzuri, wanazo changamoto mwenyekiti kazieleza, maghala yao, vitendea kazi lakini pia maslahi ya wafanyakazi. Hivyo, ni vyema kuangaliwa kwa jicho lolote maslahi ya wafanyakazi ya Tume ya Uchaguzi. Kazi zao ni ngumu sana na za hatari sana, kama zilivyo kazi za watu wengine za hatarishi basi na Tume ya Uchaguzi kazi zao ni za hatari, hivyo maslahi yao yaangaliwe.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali leo tuko mwezi wa Februari mwaka 2018, naomba serikali iamke kwa uchanguzi wa mwaka 2020, maandalizi yaanze tutachelewa kama hatukuanza sasa maandalizi. Mpaka sasa tangu tumalize uchaguzi hakuna uboreshaji wa Daftari la Wapiga Kura tunatarajia lini daftari litaanza. Tukiingia mwaka 2019 maana yake macho yetu yote yako kwenye uchaguzi. Kwahivyo, naiomba serikali iwapatie fedha tume waanze zoezi la daftari, ili tuwe na uchaguzi ulio safi na salama. *(Makofi)*

Nikitoka hapo Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie Wakala wa Uchapaji. Mhe. Mwenyekiti, nikubaliane na kamati kwa mambo mengi waliyoyasema katika idara hii au wakala huu. Lakini pia nizipongeze juhudi za serikali za kuifufua na kuimarisha wakala huu wa uchapaji. Katika miaka ya katikati au

miaka pengine ya mwanzo ya mwaka 2000 mpaka pengine juzi, ili kuwa ni idara ambayo haikuwa na uwezo wa kufanya kazi hata ukipeleka kazi walikuwa hawawezi kufanya kazi, walikuwa hawaaminiki hawana uwezo, kazi zote za serikali zikipelekwa kwenye taasisi binafsi kuchapwa na kununua. Sasa serikali kwa kuona umuhimu pengine wa kutunza siri zake na kufanyakazi kwa bidii, idara imeimarishwa sana na iko vizuri katika vitendea kazi.

Mhe. Mwenyekiti, tuiombe serikali wavitumie vile vifaa, wavitumie kwa kuziomba taasisi na idara za serikali kufanyia kazi zao katika idara ile au wakala ule. Lakini pia sio kupeleka tu kazi, lakini na wale ambao wanafanyiwa kazi pale walipe baada ya kufanyiwa kazi, maana yake upo utaratibu, kama mtu huna fedha unapeleka kwenye wakala wa serikali uchapishiwe, lakini ukipata fedha unakwenda kufanyiwa kazi yako nje sio kwa wakala wa serikali. Kwahivyo, naomba walipe madeni taasisi za serikali kwa wakala huu.

Mhe. Mwenyekiti, na wafanyakazi wa pale waangaliwe maslahi yao na ikiwezekana kuwe na *shift* pale kwasababu wanafanyakazi ngumu, lakini kuwe na posho maalum la wafanyakazi wa wakala pale.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nije katika Idara ya Uratibu. Uratibu wa Shughuli za SMZ, SMT na Muungano, hiyo SMT ndio Muungano yenyewe. Mhe. Mwenyekiti, tunawashukuru viongozi wetu wanao utaratibu wa vikao vya kutatua kero za Muungano, lakini binadamu madamu yuko hai kero haziishi. Sasa na wao wajitahidi zile kero, mimi nafikiria kuwe na utaratibu kama ambavyo tukipitisha mswada hapa baada ya Mhe. Rais kuusaini mswada, Mhe. Spika, atatutangazia kwamba katika miswada iliyopitishwa, mswada fulani umeshatiwa saini na Mhe. Rais, mswada fulani tayari.

Kutokana na hali hiyo, ni vyema kuwepo na utaratibu kwa waziri muhusika au ofisi husika iwe na utaratibu wa kutusomea kero zilizopitishwa na kutatuliwa kwenye Baraza la Wawakilishi kila linapokutana. Kwasababu hofu yangu pengine ndani ya miaka mitano hakuna kero iliyopatiwa ufumbuzi wa kukubaliana kwa makubaliano, kama ipo basi tuambiwe tufahamishwe, ili wananchi kwa kupitia sisi wawakilishi wao waweze kuelewa kero gani imepatiwa ufumbuzi.

Pia katika eneo hili naomba nizungumzie na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ya mwakilishi. Mhe. Mwenyekiti, katika majimbo ya Zanzibar kuna viongozi wawili wakuu sawa sawa, kuna mbunge na Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, wakisaidiwa na madiwani. Changamoto zipo nyingi na mimi nahisi kwamba wakati umefika kwa serikali ya SMZ na SMT kuzungumza ule mgao ulingane kwa wakati mmoja wabunge na Baraza la Wawakilishi, halafu kuwe na juhudi za pamoja ya kuzichanganya zile fedha, ili zitumike kwenye jimbo katika maslahi ya jimbo na wananchi wa jimbo. Hili linaweza kusaidia hata ile tukiambiwa kuna migogoro ndani ya majimbo, kwasababu itakuwa kwa pamoja wamechimba kisima kwa pamoja, wamejenga skuli kwa pamoja na wamejenga hospitali kwa pamoja itasaidia. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa Waheshimiwa Wabunge ambao tumechaguliwa pamoja wameshapata fedha mara tatu. Mhe. Mwenyekiti, na wewe una jimbo, mara tatu wawakilishi wote mara moja, mwananchi wa kawaida hawezi kuelewa, ataona wewe na mbunge mnapewa fedha sawa kwa wakati mmoja wewe hizitumii mbunge amezitumia. Suluhisho la jambo hili, kwasababu fedha zote zinapitia halmashauri, fedha za mbunge zinatakiwa zipite halmashauri fedha za mwakilishi zinatakiwa zipitie halmashauri, kwa nini zisichanganywe zikawa moja tu na kwasababu zote zile ni fedha za wananchi, kwa sababu zile sio fedha za mbunge, sio fedha za mwakilishi, zile ni fedha za

wananchi ambao wako huko mitaani. Kwahivyo, nilikuwa nashauri jambo hili nalo litizamwe vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoka hapo naomba niizungumzie hii Ofisi ya Rais na Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Mwenyekiti, nilianza kwa kuwapongeza viongozi wetu, nataka niendelee kuwapongeza. Nchi imetulia na ina amani na ina amani kwasababu tuna kiongozi mzuri na anatuongoza vizuri, lakini pia sio kutuongoza vizuri tu, anajenga uchumi mzuri kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Kwakweli, lazima na nafikiri wajumbe wote humu hatuna mashaka na jinsi nchi inavyokwenda, tunampongeza Mhe. Rais na tunampongeza ndugu yetu Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, hao ndio watu wa Ikulu na wengine wapo hapa, kuna Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Said Soud Said), Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Juma Ali Khatib) pamoja na Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya) pia ni Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum hawa ni MBM, wote wako katika ofisi hii ya Mhe. Rais. Sasa kazi inafanyika vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenzangu Mhe. Simai Mohamed Said, kasema kurugenzi, kaisifu sana, lakini pamoja na kusifiwa nahisi kwamba nguvu zaidi ziimarishwe kwenye Kurugenzi ya Mawasiliano Ikulu, bado hatujafikia kiwango ambacho tunaweza kusema sasa hii ndio Kurugenzi ya Rais Ikulu. Kwakweli, kama tunafuatilia juzi kuna Mhe. Mbunge mstaafu wa Jamhuri ya Muungano mgonjwa wenyewe wanamuita Papaa huyo alikuwa maarufu Bungeni. Lakini *clips* Rais kaiona moja kwa moja kamsaidia. Kwahivyo, kurugenzi ni muhimu katika mawasiliano ya umma na Mhe. Rais, ili aweze kutekeleza vizuri shughuli zake za maendeleo. Matarajio yetu ni kwamba haiko ilivyokuwa

imeimarika, lakini nafasi ya kuimarisha zaidi kurugenzi ipo. Kwa hivyo, naomba nalo hili lichukuliwe kama moja ya changamoto.

Vilevile, nizungumzie kifungu alichozungumzia mmong'onyoko kwenye Ikulu zaidi ya Kibweni. Ikulu ya Kibweni ni kweli Mhe. Mwenyekiti, lakini ombi langu mimi itakapofanyiwa ukarabati wa mmong'onyoko pale uwe mradi na ufike mpaka kwenye kikosi cha KMKM, kwasababu kwa eneo lote lile lina mmong'onyoko. Tuwe na mradi kama ilivyokuwa Forodhani ili na kule nako tukunusuru, tuinusuru skuli ile ya kihistoria na tukinusuru Kikosi chetu cha KMKM pale kisipotee katika hali ambayo iko sasa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie mchango wangu kwa leo kwa kuzungumzia Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nchi za nje. Mhe. Mwenyekiti, hapa nazungumzia jambo dogo lakini nahisi ni vyema nilizungumze. Zanzibar ni kisiwa cha utalii na tunapokea wageni wengi, na Zanzibar sasa hivi tunajenga *terminal III*, Mwenyezi Mungu akipenda karibu itamalizika.

Zanzibar hii watu wa nje wengi watalii na watu wengine, wafanyabiashara na wafanyakazi wa serikali wa kimataifa viongozi wangelipenda sana kufika Zanzibar na kufanya shughuli zao za kimaendeleo, tatizo hatuna ukumbi wa mikutano wa kimataifa. Kutokana na hali hiyo, naomba sana kwa mahusiano yetu na nchi zetu nyengine rafiki, hebu tuwaombe watujengee na ukumbi wa mikutano wa kimataifa hapa Zanzibar.

Kwakweli, naamini tukijenga ukumbi wa kimataifa hapa inaweza kuwa moja ya pato letu kubwa sana linatokana na ukumbi huu, sasa hivi Zanzibar ukitaka mkutano serikali ama Bwawani au ukumbi wa zamani wa Baraza la Wawakilishi huwezi kufanya Ukumbi wa Mikutano ya Kimataifa, Bwani yenyewe Salama

imekufa imebakiwa na Baraza la Wawakilishi ama baadhi ya sehemu za hoteli nyengine ambazo pia hazina kumbi za kufanyia mikutano ya kisasa katika maeneo haya.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwamba hapo watakapokuja kutoa majibu ya hizi ripoti za kamati, serikali ijali sana kuangalia kwamba tunakoelekea tutakuja kutakuwa na mahitaji makubwa ya mikutano ya kimataifa Zanzibar. Kwa hiyo, hivi sasa hatupati kwasababu hatuna kumbi hata ile mikutano inayofanyika Arusha, Dar-es-Salaam hivi sasa mengine ingeliweza kuja Zanzibar kama tuna kumbi za mikutano. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nimalizie kwa kuwashukuru Mwenyekiti mwenyewe wewe, Mwenyekiti wa Kamati lakini pia na Viongozi wetu na Mawaziri wenye kushughulikia Ofisi hii naomba nimalizie hapo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Machano Othman Said kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, atafuatiwa na Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis na kama muda utaruhusu Mhe. Hamza Hassan Juma ajiandae.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: *Bismillahi Rahman Rahym,* Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na mie kuweza kuchangia ripoti ya Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Kwanza tumshukuru Mwenye Mungu sote kuwa wazima, lakini jengine niwapongeze sana niwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Chaani nawasalimia sana.

Kabla ya kuanza kuchangia ripoti hii mimi nitaanza Ofisi moja kwa moja ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi halafu nitaenda kwenye Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwanza nimpongeze sana Mhe. Rais Dkt. Mohamed Shein na Mwenyekiti

wa Baraza la Mapinduzi kwa jitada zake anazochukua ufanyaji wake wa kazi na hekma zake katika kuongoza nchi. Vilevile, pongezi zangu zitaenda mbili binafsi kutoka kwangu mimi kwake yeye ikiwemo moja ya kuweza kwenda kunifungulia rasmi Soko langu la Kinyasini la wananchi wa Jimbo la Chaani ambako mimi mwenyewe nilikuwa sipo niko nje ya nchi matibabuni, lakini nimeona kwa njia ya mitandao nampongeza, nimefurahi sana na wananchi wamefurahi sana kwa ufunguzi wa Soko la Kinyasini. *(Makofi)*

Aidha, pongezi yangu ya pili nimpongeze sana nilipokuwa sipo nchini kwa kuweza kuona sherehe kubwa alizowapokea vijana wetu wa *Zanzibar Heroes* pamoja na kuwapati fedha taslimu kila mmoja shilingi milioni 3 pamoja na kiwanja kila mmoja. Naweza kuthubutu kusema kwa hesabu nilizo zifanya mimi kwamba *amount* ile yote ikijumlisha ya sherehe alizozifanya Ikulu, Viwanja alivyovitoa kwa mujibu wa dhamani ya sasahivi pamoja na fedha taslim basi zime *over* shilingi milioni mita tisa kwa hesabu zangu mimi. Kwakweli, ni jambo ambalo la kupongezwa Mhe. Rais na hii hesabu nasema tena ni yangu nimefanya mwenyewe hesabu asije akaja nambia mtu hesabu imetoka wa wapi, hesabu imetoka kwa Nadir, ikiwa kuna lolote nije niulizwe mimi hiyo ni tathmini yangu binafsi, nampongeza sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitapongeza uongozi mzima kwa ujumla kuanzia Mhe. Waziri mwenyewe, viongozi wote wanaofuatia pamoja na watendaji wote wa Ofisi Rais na Mwenyekiti wa Baraza ka Mapinduzi kwa utendaji wao mzuri, mambo yao yanakwenda vizuri na tunaridhika kusema la ukweli hakuna tatizo, japo kuwa hakuna binaaadamu alokamilika *ofcourse* yatakuwepo mambo moja mawili ambayo ya kibianaadam wenyewe wataangalia vipi vya kujirekebisha

kwasababu hakuna mkamilifu isipokuwa Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Jambo langu kubwa nilalotaka kulizungumza kwenye ofisi hii, jambo la mwanzo kwa watu wa mawasiliano kikweli sasa hivi mimi kama nilivyozunguza mambo yote niliyompongeza nipo nchini India matibatulakini niliona *up to date* Mhe. Rais yupo kwenye eneo. Lakini nipo India naona Mhe. Rais anafungua nini anaongea nini na picha zinatumwa ni jambo ambalo zuri sana kwa sisi viongozi kwasisi viongozi na sisi tunapata kuona na kutuma hata kama hatuko nchini.

Vilevile, naomba kuzungumzia suala la mambo ya Usalama ya Ikulu pamja na watu wanaohusika na kumleta Mhe. Rais kwa kweli nawapa pongezi sana, wanampa hadhi ya hali ya juu ulinzi wa Mhe. Rais uko vizuri. Mambo yanaridhisha *protocol* iko safi kabisa hata kwa *system* ambayo tunayokwenda nayo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kulizungumzia Idara ya Uhusiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi. Mhe. Mwenyekiti, suala hili nilimuuliza Mhe. Waziri mimi ninavyo fahamu mimi kitu kimoja ndani ya Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar Mhe. Rais anayo mamlaka yake anaweza akaamua vitu kama yeye kwa mujibu wa nchi ya Zanzibar. Kwahivyo, niliomba kwakuwa Wazanzibari wote ambao ni *diasporas'* wapo nje ya nchi na wanatambulikana wale hawakwenda nje ya nchi kwamba wamekataka hawajakataa Utanzania au Uzanzibar walikwenda nje ya nchi kutafuta maisha, Serikali ya Zanzibar, ya Mapinduzi ya Zanzibar haiwezi kuwajiri wananchi wote Wazanzibari hata *private sectors* hawawezi kutoa ajira kwa wananchi wote wao, kwa imani yao na fedha hata hawajaazima serikalini wala kwa Mhe. Nadir walitafuta wenyewe wakaenda kukopa wakaazimwa wakasafiri, wakaenda kutafuta maisha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano leo tuangalie Unguja nzima hii hasa maeneo ya Mbweni asilimia sabiini imejengwa na wana *diasporas* nyumba unazokuta nzuri nyingi hapa wenye wapo nje ya nchi Wazanzibari ndugu zetu wazee wetu, kaka zetu, mama zetu wamepigwa na baridi wanakosha nguruwe wengine wanakosa magari, siku za baridi tuzungumze ukweli. Kwakweli, wengine wanasafisha mpaka makaro wako Wazanzibar, hii ni hali halisi nishakwenda nishakutana siongei kitu nabahatisha, nishatembea *Europe* sana nishaonana na watu tofauti, wanaofanya kazi za makaro wanaosafisha siku za baridi wao ndio wanakwenda kufanya kazi, hali ngumu.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mamlaka alokuwa nayo, afanye jitihada zake awaruhusu Wazanzibari wale awatambue, waweze kumiliki ardhi wenyewe Unguja sizunguzi mimi Tanzania Bara nazungumza Unguja mamlaka hayo Mhe. Rais anayo waweze kumiliki ardhi, nyumba zao kwa majina yao na vile vile *ID* ya Zanzibar wapewe, hata kama itaandikwa *diaspora* lakini *ID* Zanzibar wapewe.

Mhe. Rais suala hili analiweza, sikusema wapewe *Passport*, nimesema wapewe *ID* ya Uzanzibari na sio *ID* ya Utaifa maana yake kuna ID ya Utaifa wala wasipewe wapewe ID ya Uzanzibari, wapewe haki ya kumili ardhi na nyuumba. Hivyo, ndivyo tunavyotakiwa ndugu zetu tuwapende wale hawakwenda kukukimbia wale wamekwenda kutengeneza maisha kuja kutengeneza nchi yao. Leo wanakuja hapa kama wageni. Kwakweli, haipendezi namuomba sana Mhe. Rais hili kwa hisani yake hawa Wazanzibari ambao wako wengi maelfu nje aweze kuwafikiria waweze kuwa na haki kama tulivyo sisi.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye suala la wizara hii namalizia kwa jambo la mwisho, kwa kweli ziara za Mhe. Rais zinatia nuru katika suala la uchumi, anaposafiri Mhe. Rais *automatically* kwenye ile *trip* inatangaza utalii leo angalia kenda kwenye Falme za Kiarabu utalii wenyewe nchi zote TV zote dunia nzima anaoneshwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Kwahivyo, pale nipeke yake ambapo hata nchi ambazo hawaijui Zanzibar wananchi ambao hawajawahi kusikia kuhusu Zanzibar wataona kwamba kuna nchi inaitwa Zanzibar itawavutia watataka kutafuta au watafanya *research* nini Zanzibar. Mhe. Rais wa Zanzibar kenda vile kapokelewa kama vile ni mambo mazuri, kwakweli hii yote upokeaji wake umekuja kutokana na heshima, hekma na uongozi mzuri. Kwakweli, asingepata mapokezi yale kama yeye mwenyewe ni mtu matatizo. Lakini tunamuona Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein ni msikivu anapeleka mambo vizuri na ndio maana hata akenda nje anapata heshima ya hali ya juu. Hivyo, naomba safari kama inawezekana ziwe zinazidi ikiwa za kudhaminiwa au za kwenda wenyewe kwasababu utalii na ile hali ya nchi inapata kuonekana nchini duniani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nakwenda kwenye Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili kwa juhudi zake zote anazozifanya. Lakini nimpongeze Mhe. Waziri wake makini kwa juhudi anazoziafanya, maana yake hapa anatupa majibu hata mimi mwenyewe nashindwa hata kumwambia kitu. Lakini vile vile nisimsahau ndugu yangu wakati anapata uteuzi tuko Pemba tunakula mihogo Mhe. Mihayo Juma N'hunga anapata uteuzi wa Naibu Waziri tupo Pemba ndani ya bahari nampongeza sana *(Makofi).*

Nikiendelea na mchango wangu Mhe. Mwenyekiti, naomba kuzungumzie suala la Muungano, jana nilizungumza suala la *Passport*, Mhe. Waziri wa Nchi hajanifahamu alikuwa nafahamu mzee wangu hajanifahamu, labda swali nililomuliza. Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza kwamba *passport* za zamani zote, na mimi nilizunguza jana kwamba mimi ninazo *passport* tano kwasababu huko nyumba zishajaa, zote pahala pa kuzaliwa imeandikwa Zanzibar, mahala pa kuzaliwa ni Zanzibar, *Issuing Authority* ni *PCO* Zanzibar, *Headquarter Office Zanzibar*. Lakini hii mpya nyekundu pahala pakuzaliwa Mjini, Kusini, Magharibi, Mashariki vitu kama hivyo, jana baada ya kutoka hapa nimekwenda kutafuta *passport* kumi za Waheshimiwa Wajumbe na zote hakuna kitu Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba vitu kama hivi vinatayarishwa vinavyohusiana na Zanzibar na Muungano kwanini upande wa Zanzibar hamuja-*dictate* vitu kama hivi kwenye *system* unapokwenda kujaza fomu ya Uhamiaji hakuna kitu Zanzibar wameiondosha kabisa haipo kuna kitu mjini wapi, Dodoma maana yake hakufahamiki mjini wapi, tuzungumze mjini Zanzibar, Mashariki Zanzibar, Kusini Zanzibar, lakini leo mjini, mashariki, kusini, kusini ya wapi Kenya. Hatuwezi kwenda Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kabisa ni lazima serikali ikae na kabla *passport* hazikuanza kutoka nyingi naamimi mpaka sasa hivi Zanzibar *passport* hazifiki hata mia zilizotoka. Ni vyema *passport* zile zikazuiliwa likarudishwa jina la Zanzibar katika *passport* leo jambo jengine ambalo *concern* yangu nnayo ndani ya *passport* mpya napongeza kuna picha ambazo zetu upande wa Zanzibar zina *represent*, Beit-el-Ajaib, na mmbo mengine na Karafuu lakini kuna picha ya Mhe. Julius Kambarage Nyerere baba wa Taifa ndani ya *passport* ile anamwaga mchanga wa

Muungano, lakini ya Mzee Abeid Amani Karume hakuna ndani ya *passport* ile vipi haya mambo. *(Makofi)*

Jee, Serikali ya Zanzibar ilikaa kwenye masuala haya wakakubaliana, wakashauriana, wakapeana mawazo, Baba wa Taifa yumo lakini, Baba yetu wa Taifa wa Zanizibar yuko ndani ya *passport* ile hayumo, na akanililetea mtu mmoja ushahidi basi mimi siitaki tena *Diplomatic* nitakaa na *passport* ya *ordinary*. Lazima tufanyiane haki ndio maana ya Muungano, picha ya Mhe. Abeid Amani Karume irejeshwe, ndani ya *diplomatic* iwemo nayo, isiwemo ya Mzee Julius Kambara Nyerere, jina la Zanzibar lirudi. *(Makofi)*

Lakini niende kwenye suala jengine la Muungano. Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii wala siimalizi kwasababu ninavyo vifungu vingi, nitakacho jaaliwa ndio hivyo hivyo nitakuwa nishaongea. Suala la Mabalozi lazima madhali Zanzibar tuna Muungano wa undugu na zaidi ya miaka hamsini, Balozi ndogo tuliomba zije Unguja *consulate, embassy* ziweko Tanzania Bara na kama sasa hivi zitaahamia Dodoma, basi zihamie Dodoma, lakini *embassy* ndogo ziwe Zanzibar. Kwahivyo, inakuwaje Wazanzibari wote 1.4 *million* kwamba tunapotaka ku *apply Visa* lazima twende sisi Tanzania Bara hakuna hata mtu mmoja Tanzania Bara anaekuja ku *apply Viza* yeyote Unguja. *Consulate of India, Consulate of China,* na nyengine ambazo tunazo hapa tayari kule Dar-es-Salaam zipo. Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba lazima kuwe kuna mashirikiano na makubaliano, sisi tunaongea kwasababu ni mambo ambayo tunataka nchi yetu nayo iende.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa maendeleo yake, kazi anazozifanya juhudi yake ni nzuri sana. Lakini tukija masuala haya lazima tupeane *fair, win win situation we need it here*, hakuna masuala kwamba upande mmoja uzidi masuali ya upande mwengine upunguwe. Kwahivyo,

naomba serikali ikae Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, balozi zile wakubaliana wanazo zi *shift* Dodoma zipelekwe na zizobakia zirudi Zanzibar angalau tufahamu na sisi kwambana sisi tunapata chochote.

Lakini, jengine niende kwenye suala hilo la Muungano wakakae Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Ofisi ya Tanzania Bara waangalie biashara za Zanzibar ambazo tunaumia zinazobanwa na kuzidisha mambo ya ushuru, wafanyabiashara Wazanzibari wanaumia kwenye masuala ya biashara hasa unapotaka kupeleka vitu bara. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana suala hili litatuliwe na Mhe. Waziri wa Mambo ya Muungano ni mtu mzuri sana Mhe. Januari Yussuf Makamba, ni mtu ambaye mfahamu tukae naye tumueleze atatue haya mambo.

Mhe. Mwenyekiti, la kumalizia kama ulipowapa wenzangu dakika tano na mimi naomba unipe dakika tano nende kwenye suala la mambo ya masuala ya muungano Jeshi la Polisi, niwapongeze sana Jeshi la Polisi viongozi wa juu wote, watu ambao wana hekima za hali ya juu na watu wasaidivu na watu ambao wana heshima. Lakini kuna baadhi wachache katika Kitengo cha *Traffic* ndio ninaowazungumzia hapa, kwa mfano hivi sasa mgeni anatoka *airport* Zanzibar anakwenda Nungwi atasimamishwa mara tisa hii kweli nchi ya utalii nchi yenye usalama huyo mgeni mwenyewe anaanza kuogopa na Polisi Kitengo cha *Traffic* baadhi yao hawana nidhamu wa chini wanawabandulia watu *road license* zao kwenye kiyoo *insurance* kisa kasahau leseni, wakati sheria ya kumpa mtu masaa ishirini na nne kuweza kwenda kupeleka ipo hawa wanasema hawaitambui.

Vilevile, isitoshe Polisi Kitengo cha *Traffic* baadhi yao wanatoa maneno ya kifedhuli hawajui kiongozi nani, raia nani, wao wakishavaa magwanda yao meupe wanasema kwamba wao ndio wao hata ukimgusa ukimwambia kitu wana nguvu. Mhe.

Mwenyekiti, naomba sana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, polisi haina haja Zanzibar kuwepo kila kona leo unatoka Mbweni unakwenda Malindi utasimamishwa mara tano hapo hapo ukienda mbele wapo, ukienda *Africa House* wapo, ukienda Malindi Polisi wapo hufiki Mlandege wapo wanamsimamisha nani, kwakweli linaudhi sana ni vyema polisi wakapewa taarifa wanawasumbua wageni wanasumbua raia.

Mhe. Mwenyekiti, naona unataka kubinya zamani, kwasababu nina vitu havijamaliza lakini nahisi nitakuja kuongea siku nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti hii naipongeza nampongeza Mhe. Rais tena kwa juhudi zake zote na vile vile nampongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na Mawaziri wote na watendaji wote kwa kazi zao wanazokwenda nazo, ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf nakushukuru kwa mchango wako lakini pia nakushukuru kwa kuwa umesema utamaliza siku nyengine lakini umemaliza. Sasa naomba nimwite Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis, atafuatiwa na Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi kuweza kuchangia Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uzima nikaweza kusimama mchana huu. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nichukue fursa hii kuipongeza kamati kwa taarifa ambayo wametuwasilishia ambayo ilikuwa na ufafanuzi

mkubwa na uwazi katika utekelezaji kwa wizara zetu hizi mbili. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kuipongeza serikali kwa namna ambavyo wamejipanga kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma za msingi bila ya ubaguzi wa aina yoyote. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipekee kabisa nichukue pia fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kutekeleza ahadi na kuweza kuwapunguzia mzigo wa ukali wa maisha wananchi wake ikiwemo kutangaza elimu bure. Ilianzia kwa elimu ya msingi lakini kutokana na umahiri wa Mhe. Rais sote ni mashuhuda ameongeza mpaka elimu ya sekondari kuanzia mwezi Julai, 2018. Kusema kweli haya ni mafanikio mazuri kwa serikali yetu na ya kujivunia. *(Makofi)*

Vilevile, kwa upande wa afya. Upande wa afya Mhe. Rais amejitolea kuhakikisha dawa zinapatikana katika hospitali zetu na ukweli kabisa tunapokwenda vituoni dawa tunazikuta. Haya yote ni matunda ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo tunapaswa kujivunia sote, nikiacha shukurani hizo niende moja kwa moja katika ripoti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa ukurasa wa tatu Tume ya Kitaifa ya Uratibu wa Udhibiti wa Dawa za Kulevya, kwanza niipongeza tume kwa shughuli ambazo zimefanya zikiwemo za mikutano ya uhamasishaji, lakini mafunzo mbali mbali wametoa kwa lengo la kuhakikisha wanapunguza madhara kwa watumiaji wa Dawa za Kulevya. Lakini pia tume imeweza kufanya utafiti kwa vijana kwa ajili ya kufuatilia tabia za vijana wanaotumia madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, tukija ukurasa wa nne kwenye changamoto. Baada ya kuangalia changamoto hizi Mhe. Mwenyekiti, kwa mawazo yangu nahisi bado tume wana kazi ya kufanya kubwa tu, kwasababu kama wanataka kudhibiti, lakini changamoto ya kwanza inasema upotevu wa vielelezo vya kesi, nafikiri kama vielelezo vya kesi vitapotea sifikirii kama tutaweza kuwa na takwimu nzuri. Kazi bado inahitajika, lakini kutokana na hili mimi niishauri tu tume ishirikiane na Kitengo cha Dawa za Kulevya, ili waweze kupata takwimu na kuandaa utaratibu mzuri wa kutunza vielelezo hivyo ili viweze kusaidia katika harakati za majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tukija katika changamoto ya pili, ukosefu wa takwimu halisi juu ya idadi ya vijana walioingia na kutoka katika *Sober House*. Mhe. Mwenyekiti, *Sober House* zipo nyingi na vijana wengi wanaingia, kama tume itakuwa haina takwimu halisi kwa maana hiyo inaonekana dhahiri kwamba ushirikiano wa tume unamapungufu kidogo kwa hizi *Sober House*. Kwa hivyo, naishauri tume kama ina mashirikiano na *Sober House* basi izidishe mashirikiano, ili kuratibu vyema vijana na kupata kujua changamoto ambazo zinazikabilli hizi *Sober House*. Lakini pia wataweza kuandaa mipango ya kuweza kuwaendeleza vijana ambao watatoka katika hizi *Sober House*, ambao wengi wao wanapotoka huwa wanarudia tena.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kipekee kabisa nichukue fursa hii kukipongeza Kitengo cha Dawa za Kulevya, kitengo hiki kwa namna ambavyo wanavyofanya kazi, tuseme kweli mwaka jana tulisimama hapa tukalalamikia sana kitengo. Lakini nafikiri wenzangu watakuwa mashuhuda kusema la kweli zile harakati za wale vijana kuwa wanajikusanya kwa wingi katika maeneo zimepungua na tunafika kuwatafuta hasa katika yale maeneo ambayo tulikuwa tunawakuta basi wamepungua sana, hata mitaani wamepungua kwa kiasi kikubwa. Kwahivyo, naamini jitihada za

kitengo zimepelekea vijana wale aidha, kupunguza au kuacha kutumia madawa na kupelekea kutafuta kazi za kufanya.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kwa kusema kuwa kuna *Airport* pale kuna Bandarini pana vifaa vya uchunguzi vimewekwa tunaviona lakini kusema kweli vifaa vile tukitizama bado sijui wale Watendaji au vifaa vyenyewe kunahitaji mkakati wa ziada. Kwasababu sisi sote tunasafiri tunapita katika yale maeneo na jinsi vinavyoangaliwa na jinsi ya ujanja walionao hawa wafanyabiashara wa madawa ya kulevya, kwakweli kwa uangalizi ule tu hata kama dawa zimo si rahisi kuziona kwa hivyo panahitaji mikakati ya ziada, ili kuona kwamba dhamira inatimia ya kuwekwa mashine zile pale.

Mhe. Mwenyekiti, nije ukurasa wa kumi katika ukurasa wa kumi kwenye Idara ya Watu Wenye Ulemavu. Mhe. Mwenyekiti nianze kwa kuipongeza serikali kwa kuanzisha Idara ya Watu Wenye Ulemavu ambayo inaratibu masuala ya Watu wenye Ulemavu. Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii kusema kwamba huko nyuma watu wenye ulemavu walikuwa hawana kitengo maalum au idara maalum ambayo inashughulikia masuala yake, na badala yake ilikuwa mara unaambiwa watu wenye ulemavu wapo chini ya Wizara ya Afya maana yake kama wagonjwa, lakini wakati mwingine Ustawi wa Jamii kama wanahitaji msaada kitu kama hicho.

Kwakweli, serikali imechukua jitihada kuhakikisa kuweka Idara ambayo inashughulikia masuala ya Watu Wenye Ulemavu na iko chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kusema kweli tunaipongeza sana serikali kwa jitihada zake. Na hii yote serikali yetu inajitahidi kuhakikisha inawawekea wananchi wake mazingira yaliyokuwa mazuri, ili waweze kufikia yale malengo ya dunia.

Mhe. Mwenyekiti, katika Idara ya Watu Wenye Ulemavu imeelezwa kuwa kuna changamoto mbalimbali ambazo zinaikabili idara hiyo, ikiwemo kuwa bajeti ndogo, pia kuna Baraza la Watu Wenye Ulemavu, Baraza lile linategemea bajeti ile ile ndogo ambayo inatengwa na serikali kwa ajili ya Idara wanaitumia Baraza. Kwahivyo, ukizingatia Mhe. Mwenyekiti Idara ya Watu wenye Ulemavu ina majukumu mengi sana, hasa ukiangalia sekta yenyewe watu wenye ulemavu wanamahitaji mengi na kuanzishwa kwa Idara hii Watu wenye Ulemavu wanahisi hapa ndio kimbilio letu la kumaliza matatizo yetu.

Hivyo, wana masuala mazima ya ujumuishi, imeelezwa hapa shughuli zao ni ujumuishi katika suala la ujumishi pana hitaji elimu hapa, kwasababu kama tunavyojua kila mmoja na uelewa wake kwa masuala ya watu wenye ulemavu, panahitajika kutolewa elimu ya kutosha, ili taasisi zote ziweze kuandaa mipango yake kwa kujumuisha masuala ya watu wenye ulemavu, ili kupunguza mzigo kwa hii idara. *(Makofi)*

Kwahivyo, panahitajika elimu ya kutosha, wanahitaji kuandaa pengine mafunzo kuwaelimisha watu, ili kuweza kutoa uelewa wa kutosha. Lakini uwezeshaji wa watu wenye ulemavu, suala zima la uwezeshaji ni pana, kumuwezesha mtu mwenye ulemavu wanatoa huduma ya kumuwezesha pengine kifedha, kuna watu wenye ulemavu ambao wanataka kujiendeleza na viwango vyao vya elimu haviwaruhusu kupata mikopo watu hao mara nyingi huwa wanakimbilia katika Idara ya Watu Wenye Ulemavu, ili kupata *suport* waweze kuendelea pengine kujiunga na taasisi ndogo ndogo za kuweza kujiwezesha kujiajiri wenyewe. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini hiyo haitoshi katika kuwawezesha Watu wenye Ulemavu inakuja na vile vifaa ambavyo watu wenye ulemavu wanahitaji kwa ajili ya marekebisho na kuweza kumudu kwa hiyo idara pia ina jukumu la kununua vile vifaa vikiwemo

wheelchair, crouches na vifaa vyengine kama tunavyovijua na tunavizungumza kila siku hapa. Kwahivyo, utakuta hivi vyote kama vile *wheelchair* moja ina thamani ya shilingi laki nne kwa ndogo kuinunua, kwa hivyo idara ina wajibu wa kununua hivi vitu na kuhakikisha wanawapatia hawa watu.

Kwa maana hiyo, pesa ile ambayo inatengewa idara pamoja na masuala ya utekelezaji, masuala ya kuendesha ofisi, ukikuta na pesa ile ile watumie kuendesha Baraza lao hivyo unakuta bajeti hii ni ndogo. Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali au wizara kufikira zaidi suala la kwanza kuwaongezea bajeti, lakini vilevile hili Baraza la Watu Wenye Ulemavu waweze kulipangia bajeti yake maalum katika bajeti inayokuja ya mwaka 2018/2019. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mengi yamezungumzwa mazuri, michango mizuri imetoka lakini pia nichukue fursa hii kuwapongeza Mawaziri wetu wa Wizara zote mbili hizi kwa jitihada zao wanazozifanya za kuhakikisha wizara zetu kuu hizi zinakwenda vizuri na mambo yanakuwa sawa kama tunavyoyaona. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mchango huo, nakushuru kwa kunipa fursa hii na ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis, Mwakilishi wa nafasi za Watu wenye Ulemavu kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Hamza Hassan Juma, na atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo na wachangiaji wengine watapata nafasi ya kuchangia jioni tutakapo kuja tena.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa leo Barazani, kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wetu. Vilevile, nikushukuru

wewe kwa kunipa nafasi hii nikaweza kutoa mchango wangu katika ripoti hii ya Kamati yetu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa inayoongozwa na Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Mwenyekiti, kwakweli nafarijika sana kwasababu niliwahi kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, na nilifanya kazi kwa karibu sana na taasisi hizi mbili Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na pia Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Kwahiyo, kuna mambo mengi ambayo tulikuwa tukiyashauri tulipokuwa kwenye kamati kupitia idara na taasisi mbalimbali zinazosimamiwa na Afisi ya Rais na Afisi ya Makamu wa Pili, kwakweli leo hii nafarijika sana kwamba miongoni mwa Ripoti ya Kamati ambayo ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeelezewa na kuna ufanisi mkubwa ambao umefanyika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika eneo ambalo kamati yangu kipindi kilichopita, ilikuwa ikikizungumzia sana kuhusu Kitengo cha Habari na Mawasiliano Ikulu, ambacho kinasimamia utekelezaji wa shughuli za Mhe. Rais. Kwakweli, kipindi cha nyuma kilikuwa kitengo kiko hali mbaya kilikuwa hakina vifaa vya kutosha, tuliishauri sana serikali na kipindi kile tulikuwa tukitoa mifano kwa ziara alizokuwa akifanya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete. Tulikuwa tunawaambia sisi tunaona tabu tunapoona Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anapokuwa katika ziara za nje ya nchi tunaona matukio mbalimbali ambayo anayafanya kule, wananchi wanafarijika.

Mhe. Mwenyekiti, tuliwahi kuwaambia kwamba ilifika pahala Bungeni wakawa wanahoji kwamba ziara za Mhe. Rais zina faida gani, zina tija gani. Kwa maana hiyo, tukawaambia ile kuonesha

zile *activities* ambazo Mhe. Rais anazozifanya nje ya nchi, basi inawapa matumaini wananchi kwamba kweli Mhe. Rais wetu tumemtuma kazi na anafanya kazi kwa niaba ya Wazanzibari wote.

Wenzangu wamezungumza ziara ambazo alizozifanya Mhe. Rais katika Falme za Kiarabu sisi zimetufarijisha sana zimezidi kutuongezea udugu na urafiki na kujenga imani, kwasababu kuna baadhi ya watu walikuwa wanahisi labda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na baadhi ya Falme za Kiarabu kwamba hatuna mahusiano mazuri. Lakini ziara ya Mhe. Rais imeweza kuuthibitishia ulimwengu kwamba Zanzibar haina uadui na mtu, na ziara ile imetusaidia sana kutufungulia milango ya biashara kwa nchi yetu pamoja na suala la uwekezaji. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama walivyozungumza wenzangu kwamba utalii unatangazwa kwa njia nyingi, kuna matangazo ya wenyewe Kamisheni ya Utalii iliyopewa jukumu la kushughukia masuala ya utalii, lakini kuna Balozi zetu za nje pia zinatangaza utalii, lakini ziara kama hizi za Mhe. Rais pamoja na Makamu wa Pili wa Rais zinatusaidia kutujengea udugu vilevile kufungua utalii katika nchi hii. Kwahivyo, tunakipongeza sana Kitengo hiki cha Habari na kama wenzangu walivyosema, kizidi kuongezwa nguvu kitiwe nyenzo, ili kiweze kufanya kazi kwa ubora zaidi. Mhe. Mwenyekiti, tunaaendelea tena kuwapa pongezi na waendelee kufanya kazi nzuri kama walivyofanya.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kazi zake anazozifanya kama walivyoeleza wenzangu, kwamba hali ya amani na utulivu tuliyokuwa nayo hapa Zanzibar mmoja aliechangia ni yeye mwenyewe Mhe. Rais wa Zanzibar kwasababu ni mtu ambae hapendi malumbano na mtu, hapendi uadui, ni mtu ambae mpole na akiwa kiongozi wa nchi anakuwa mpole basi hata nchi inatulia kwa sababu hata wale

wanaofanya vurugu wanajiuliza hii vurugu tumfanyie nani mtu wenyewe katulia hana makeke hana tabu na mtu kwa hiyo hata ukifanya vurugu utakuta hujisikii vizuri, hivyo tunashukuru nchi yetu imetulia. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini nawaomba Wazanzibari, isiwe tunasema nchi yetu imetulia tena wakaanza kuzuka wanatwambia tumelia aa! Tukitulia tunafanya shughuli zetu kwa uhuru zaidi. Kwahiyo, naomba hiki Kitengo cha Uratibu wa Shughuli za Mhe. Rais, kuna ahadi ya Mhe. Rais, ambayo iko katika jimbo langu na huu ni wajibu wangu, kwasababu wao ndio walonileta bila ya wao mimi hapa nisingefika. Kwakweli, ahadi hii nimeshajaribu kuizungumza sana kuna barabara yetu ya Shaurimoyo inayopitia Mboriborini mpaka Darajabovu, ile barabara hivi sasa inatumika daladala zinakwenda lakini kwa bahati kila zinaponyesha mvua daladala zile zinakuwa zinasita kutoka na uharibifu wa mvua hizo.

Lakini barabara hiyo katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2010/2015 ilikuwemo barabara hiyo, lakini kwa bahati mbaya sana haikuwahi kutengenezwa. Sasa kwa kuwa ni ahadi ya Mhe. Rais kama nilivyosema najua Katibu Mkuu itakuwa yupo, Waziri yupo na Mratibu wa shughuli za Serikali Mhe. Makamu wa Pili yupo, hivyo tunaomba sana kabla ya Mhe. Rais kumaliza muda wake, basi barabara ile tuweze kukamilishiwa, ili tuweza na sisi kufaidi neema na matunda ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na ahadi hiyo ya Mhe. Rais katika jimbo langu ambayo haijatekelezwa, lakini nisiwe mkosefu wa shukurani lazima nizungumze ukweli kwamba kuna ahadi ambazo Mhe. Rais aliziahidi katika kampeni za uchaguzi uliopita alituahidi kwamba atatumalizia ghorofa ya pili ya hospitali yetu ya Jimbo la Kwamtipura ambayo sasa hivi linaitwa Jimbo la

Shaurimoyo. Kwakweli, tunamshukuru sana na sasa hivi wananchi wanapata matibabu pale wa ndani na nje wanaotoka Mwera, Chwaka wanakuja pale wanatibiwa macho. Kwahivyo, tunamshukuru sana Mhe. Rais kwa jitihada ile na wananchi wetu wanapata faraja huduma iko karibu kuliko kwenda Mnazimmoja.

Vilevile, kuna ahadi ambayo Mhe. Rais alituahidi katika jimbo letu ameitekeleza tunamshukuru sana, mtaro wetu wa maji machafu maarufu unaitwa mtaro wa Darajabovu mtaro ule, kwakweli ulikuwa kadhia kubwa kwa wananchi wa Zanzibar hasa katika jimbo langu pamoja na jimbo la Chumbuni na Jimbo la Amani kwasababu mtaro ule umetugusa maeneo yote. Kwakweli, ilikuwa kila inapofika mvua za masika basi mimi hapa Barazani nakuwa situlii, simu mia mia Mhe. Mwakilishi njoo uangalie tunazama, lakini hata nikienda nafanya nini naangalia tu sina chengine ambacho nakiweza kukifanya nilikuwa namkamata sana rafiki yangu, mwalimu wangu, swahiba yangu Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ (Mhe. Haji Omar Kheir), namwambia Watumbatu wenzako wanazama kule Shaurimoyo.

Mhe. Mwenyekiti, tunashukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kwasababu mtaro ule unasimamiwa chini ya Baraza la Manispaa kwenye mradi wa *ZUSP*. Kwakweli, tunashukuru sana Mhe. Rais pamoja na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, mtaro ule sasa hivi kwa kweli haujamilika lakini unaendelea kujengwa.

Lakini pamoja kwamba haujakamilika, lakini *try* ya mvua za masika zilizopita, tuliona *impact* yake kwakweli maji yalikuwa yanapita hakuna nyumba hata moja iliyozama, hivyo ule mtaro umetekeleza hasa ile *program* ya kupunguza umasikini Zanzibar. Kwahivyo, ndani ya jimbo langu *program* ya kuondoa umasikini

umesaidiwa sana na mtaro ule na tunaomba tu salamu zetu zifike basi mtaro ule ukishamaliza Mhe. Rais aje kutuzindulia, ili na sisi tupate kufarajika kuwa pamoja na yeye.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba lazima kwanza nitangulize shukurani halafu baadaye ndio uombe lilie ambalo unataka. Kwahivyo, lile la mwanzo la kuomba nimetanguliza mwanzo lakini yale ambayo Mhe. Rais ametufanyia tayari nimeshayatanguliza.

Mhe. Mwenyekiti, katika Afisi ya Rais Ikulu katika ripoti hii limeelezwa suala la mmong'onyoko wa Ikulu ya Mkoani na kuna fedha karibu milioni 30 tayari serikali imetoa kwa ajili ya ujenzi wa mtaro ule. Sasa naomba Mhe. Waziri muhusika afuatilie kwamba zile pesa zitumike vizuri, ili kusije kukatokezea mmong'onyoko tukaweza kupata hasara zaidi. Kwakweli, wamejitahidi sana Ikulu ya Mkoani imeboreshwa, lakini ule mmong'onyoko lazima ushughulikiwe, ili kuhakikisha kwamba usalama wa jengo letu lile unapata utulivu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nije katika Kitengo cha *GSO* tunashukuru sana wanafanya kazi nzuri tunapata wafanyakazi waadilifu, *vetting* inafanyika vizuri na wakati mwengine vijana wetu wanashtuka wanapoitwa na Kitengo cha *GSO*, tunawaambia msishtuke hivi sasa serikali inataka kila kitu kiende sawa unapotaka kuajiriwa, lazima upimwe na uchunguzwe uadilifu wako, uaminifu wako, ili unapokwenda kupewa majukumu ya serikali uweze kiufanya kazi vizuri kwa kuaminiwa. Lakini, kuna kadhia yao jengo lao kwakweli linavuja tulikuwa tunaomba sana Afisi ya Rais kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, waweze kulishughulikia, ili lipate kuezekwa kwa ajili ya kulinusuru kuvuja na ndugu zetu hawa waweze kufanya kazi zao kwa utulivu.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nakuja kwenye Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Mhe. Mwenyekiti, naendelea tena kutoa shukurani zangu sana kwa serikali kupitia Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais tunamuona jitihada zake anavyohangaika huku na kule kututafutia maslahi Wazanzibari. *(Makofi)*

Kwakweli, tunamuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais asichoke pamoja na changamoto ndogo ndogo wakati mwengine bajeti hazitoshi lakini kwa kweli tunaona jitihada zake, na amepata wasaidizi makini Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Mhe. Mohammed Aboud Mohammed) sisi hapa Barazani tunamuita *midfield* chochote kinachokuja hapa kikikwama hata kidogo kama vyuma vimefanya kutu, basi akisimama yeye basi vyuma vyote vinalainika kwa kweli tunakupongeza sana. Lakini pia amepata msaidizi ambaye ni kijana wetu mdogo kabisa Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (Mhe. Mihayo Juma N'hunga), nampongeza sana ni kijana mtulivu anafanya kazi vizuri sana, ukweli timu imetimia na Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais tunawashukuru sana kazi wanafanya nzuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo kidogo nataka katika afisi hii yafanyiwe kazi kama walivyosema wenzangu Idara ya Wakala wa Uchapaji, pale kuna mashine za kisasa kama tulivyosema kipindi cha nyuma tulifanyakazi nao kwa karibu walipokuwa wakizama pale Saateni wakati wa mvua za masika ilikuwa lazima uende na kihori. Lakini tunashukuru jitihada za Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alituahidi kwamba jengo linahama na kweli wapo Maruhubi na wanafanya kazi nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa wito kwa serikali na hili namuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alikemee sana, kwamba bado kuna baadhi ya taasisi zetu za serikali zinachapisha machapisho yao nje ya Idara yetu ya Wakala wa Uchapaji hii ni

kusema sawa sawa na matumizi mabaya ya fedha za umma. Kwahiyo, kama serikali imehangaika mwanzo tunakumbuka machapisho yetu mengi vitabu tulikuwa tunachapisha Tanzania Bara hata vitabu vya bajeti, lakini leo serikali imefanya jitihada imenunua mitambo mipya ya kisasa, leo bado kuna baadhi ya watendaji au taasisi zinafanya machapisho yake nje ya *Government Press*. Kwakweli, hili sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hatulikubali, hivyo tunamuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alikemee suala hili na alichukulie hatua kwa haraka sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwakweli pale tume -*invest* ile *investment* iliyowekwa pale inatakiwa angalau irejeshe fedha na ijiendeshe vile vile, leo mitambo ile ya kisasa ikiharibika pale kama *Press* haina fedha za kutosha tutaweza kupata wapi, au itabidi lije liwe gofu. Kwahivyo, tunaomba sana watendaji wetu hawa waweze kuitumia *Government Press*, ili kuweza kufanya machapisho yao. *(Makofi)*

Jambo jengine ambalo naliomba kwamba zile ni mshine za kisasa sana, ni mashine ambazo ziko *modern* zinahitaji wataalam wenye taaluma kubwa. Mhe. Mwenyekiti, tunaomba sana bado tunahitaji vijana wetu wanaofanya kazi pale waweze kupatiwa mafunzo ya kisasa, ili zile mashine waweze kuzitumia vizuri, zile mashine zina mambo mengi sana. Lakini kama hawana taaluma nazo za kutosha wataweza tu kutoa kopi kufanya machapisho madogo madogo, lakini kumbe kuna kazi nyingi ambazo zinaweza kufanywa pale zikaweza kuleta tija kwa nchi yetu. Mhe. Mwenyekiti, hili naliomba Mhe. Waziri waifanyie kazi tunaamini vijana wetu wakipata taaluma ya kutosha basi naamini kazi itakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna kadhia hii aliyoizungumza Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf. Kwakweli, nampongeza sana Mhe.

Mwakilishi kwa utafiti wake mdogo alioufanya, unajua sio kila kitu unaweza ukakiona kwa haraka haraka kuna vitu vyengine mpaka vitokezee ndio unaweza kuona zile kasoro zake. Mhe. Mwenyekiti, hata mimi nimejaribu kuangalia *passport* mpya ambayo iliyotolewa nimeona mule kweli safari hii Beit- el- Ajab limo kwenye *passport* yetu kuna mnazi, mkarafuu. Lakini, mambo mengine sikuweza kuyazingatia na ni kweli kama kuna picha ya Mwalimu Nyerere katika *Passport* ile lakini picha ya Marehemu Mzee Amani Karume haimo kwa kweli sio sahihi sasna. *Passport* tunajua yale ni mambo ambayo sasa hivi kila kitu kipo katika *soft copy*, naamini kama yatafanyika maboresho basi tutaweza kufanikiwa vizuri. *(Makofi)*

Vilevile, kuna hili jambo ambalo kweli hata mimi nilijaribu kujaza ile lakini nilipitikiwa kuona neno Zanzibar kumbe Zanzibar haimo katika *passport* sasa hili kidogo, ni kweli na ukiangalia pale ukitaja mikoa yanakuja, ukiangalia kata zinakuja lakini kama neno Zanzibar halimo ukweli ile *passport* itakuwa haijatimia, kwasababu *passport* yetu ni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania neno Zanzibar *specific* likiwemo kwa kweli litaongeza tija katika *passport* hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuhusu Kitengo cha Uratibu wa Shughuli za Muungano. Kwakweli, bado kuna changamoto ambazo sisi Kamati ya Ardhi na Mawasiliano tuliwahi kufanya ziara Dar-es-Salaam tukaonana na Mhe. Waziri wa Muungano na tulikubaliana mambo mengi, miongoni mwa mambo hayo basi zile ambazo zinaitwa kero hasa zinazogusa na maisha ya watu kila siku ziweze kushughulikiwa, lakini bado kuna changamoto ndogo ndogo bado zipo hizi. Kwahivyo, naomba sana kwamba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, basi tuweze kufanya jitihada za kushughulikia changamoto hizi, bado kuna tatizo la biashara vibali vinavyotoka Zanzibar wenzetu hawavitambui Jamhuri ya

Muungano hawaoni kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na sisi vile vile tunavyo vitengo ambavyo vinaweza kutoa *document. (Makofi)*

Kwa mfano, wakati mwengine kuna *documents* zinazotoka Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi hawazithamini hawazitambui, pamoja na idara ama taasisi zake zote hawazitambui. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa kuna kero nyengine mpya imeshajitokeza juzi tulizungumzia Mswada wa Ushindani wa Viwanda kwa bahati mbaya mimi nilikuwa nina dharura kidogo sikuwahi kuchangia, kuna kadhia ya Kiwanda chetu cha Sukari Mahonda kwamba kinazalisha sukari ambayo *quality* yake ni nzuri sana inahitajika Tanzania Bara, hapa soko la ndani tunashukuru inakwenda vizuri. Lakini leo inapofika bara kule wanawekewa vikwazo mbalimbali wanaambiwa walipe ushuru na mambo mengine wakati hii bado tumo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Lakini kuna kadhia ambayo ni jana tu baada ya wananchi wetu kusikia kwamba tuko katika Baraza la Wawakilishi wametujia hapa kuna kadhia sasa hivi ya wauza madagaa, yaani sasa hivi madagaa yashakuwa ni kero za Muungano yaani, kuna vitu ambavyo vya ajabu ajabu leo ukiangalia serikali haiwezi kuajiri watu wote kuna mwenzangu mmoja kazungumza, lakini wananchi wanaweza wakajiajiri katika sekta nyengine binafsi. Tunashukuru sana watu wetu sasa hivi wavuvi, Wakojani na wengine wanatusaidia sana dagaa linavuliwa kwa wingi sana na ndio maana *Zanzibar Heroes* kule safari hii ilifanya kazi nzuri sana kwa ajili ya madaa, madagaa Mhe. Mwenyekiti yana nguvu sana ukipiga dagaa, basi ukipiga shuti kwa kweli linakuwa kubwa sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, dagaa leo limekuwa na *market* kubwa linasafirishwa mpaka Congo watu wanauza kwa dola, lakini sasa

hivi tayari kuna changamoto imeshaanza kujitokeza wanasafirisha dagaa hapa wanapata vibali kila kitu wanalipia, wanapita Dar-es-Salaam hakuna tatizo lolote, lakini wanapofika Tunduma kuingia Zambia wanaambiwa walipe ushuru, ushuru wa nini dagaa linatoka Zanzibar na Zanzibar ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa nini halikulipishwa ushuru bandari ya Dar-es-Salaam, Dar-es-Salaam wamelipa *wharfage* kila kitu.

Sasa leo wanakwena wanazuiwa pale wanaambiwa kila kilo moja walipe dola moja leo gunia la dagaa linajazwa kilo 180 ina maana pale walipe dola mia moja na thamanini, huu ni wizi na unyang'anyi, kwasababu lile dagaa kama ni maliasili imevunwa Zanzibar na tayari kuna *documents* zote wameruhusiwa leo wanafika pale Tunduma wanaingia Zambia, hivi sasa tunavyozungumza kuna magunia zaidi ya 200 yamezuiwa mpakani pale Tunduma Zambia yanashindwa kwenda kwasababu watu wanataka kutozwa pesa ambazo hawakujiandaa.

Mhe. Mwenyekiti, huu nasema ile sio kodi wala ushuru isipokuwa ule ni wizi, serikali lazima ihakikishe kwamba vijana wetu wa Zanzibar ambao wameamua kujiajiri, basi waweze kupata nafasi ndani ya Tanzania yao wajivunie. Kwakweli, leo ni aibu tunasema tunakwenda katika vikao vya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki tunasema tunafungua Soko la Pamoja la Afrika ya Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, juzi Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika sasa hivi Mhe. Paul Kagame amezungumza anasema sisi tunapata tabu hebu tufungue Soko la Afrika, Waafrika tuuze ndani wenyewe kwa wenyewe hatuna haja ya kuomba misaada ya nje. Sasa leo tayari ndani ya Tanzania yenyewe tunawekeyana vikwazo, je leo utategemea ufanikiwa katika Soko la Afrika. Kwakweli, hii sio haki kwahiyo naomba sana serikali yetu nasema inaongezeka kero nyengine, kwahivyo kabla ya kuwa kero hii changamoto ishughulikiwe isije ikaingia kwenye kero za Muungano.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumza haya kwasababu mimi ndani ya jimbo langu nina wajasiriamali waanika madagaa wengi sana hawapungui 300 wengine ukienda Maruhubi sasa hivi wapo, ukenda kule Zingwezingwe Mahonda kule wapo, ukenda Mangapwani wapo sasa hao wote ni wananchi wangu sasa leo biashara ile hapa hawazungumzii suala la *market*, *market* ipo kubwa sana watu wanauza dagaa kwa dola. Lakini leo atatizo Watanzania wenzetu mpaka wa Tunduma wanaanza kutufanyia wizi na sijui kama ile kodi wanayoi-*charge* kama inaingia katika kodi ya serikali. Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais lishughulikie suala hili na kodi ile kama haikuingia kwenye serikali, basi hao walioshughulika na kuwanyang'anya vijana wetu wa Kizanzibari waweze kutumbuliwa mara moja. Mhe. Mwenyekiti, kero hii ya wananchi wangu kwakweli imebidi niizungume hapa kwasababu imeniuma sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimalizie kwasababu naona unaniganalia angalia kidogo nataka nimalizie katika changamoto ya madawa ya kulevya. Kwakweli, naipongeza sana serikali suala la madawa ya kulevya pamoja na tunavyosemwa Zanzibar, lakini tumefanya jitihada kubwa sana, Kitengo cha Jeshi la Polisi kinafanya kazi kubwa sana, kwasababu lazima tukubali Zanzibar ni visiwa kwa njia ya kuingilia ndani ya visiwa vyetu njia za panya *roads* zinakuwa wakati mwengine ni nyingi. Lakini hali ya madawa ya kulevya kwa hapo ilivyokuwa hapo nyuma na sasa hivi ilivyo ni tofauti sana, hivi sasa hata ukiangalia wale watumiaji wa madawa ya kulevya wa kusinzia sinzia unawatafuta tofauti na walivyokuwa zamani na hii yote ni jitihada ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, hivyo lazima tuwapongeze. *(Makofi)*

Lakini bado naomba kuweko mashirikiano baina ya Afisi ya *DPP*, Mahakama Kuu na Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia Jeshi

la Polisi. Kwa maana hiyo, bila ya mashirikiano ya watu hawa kwakweli tutakuwa sawa sawa tunatwanga maji kwenye kinu, afisi itakuwa inafanya kazi yake vizuri lakini wanapokamatwa wakipelekwa huko kunakohusika kama hawashughulikiwi, basi tutapata tabu sana. Kwahiyo, nawapongeza sana na naunga mkono ripiti hii ya kamati pamoja na naunga mkono jitihada za serikali kupitia taasisi mbalimbali zilizokuweko Afisi ya Mhe. Rais pamoja na Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana ahsante sana.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaakhirisha kikao nami niwashukuru wachangiaji wote wa ripoti hii pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ambae amewasilisha hii ripoti. *(Makofi)*

Lakini, naomba niwatangazie Wajumbe Wanawake wa UWAWAZA kuwa baada ya kuakhirisha kikao hichi wanawake wote wa UWAWAZA wabakie humu ndani, taarifa kutoka kwa Mwenyekiti wa UWAWAZA. *(Makofi)*

Nawashukuru sana na naomba nichukue nafasi hii kuakhirisha kikao hichi mpaka saa 11.00 jioni.

(Saa 12.53 mchana Kikao liliakhirishwa mpaka saa. 11:00 jioni)

(Saa 11 .00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza kunipa na mimi fursa ya kuchangia ripoti ya Kamati ya

Kudumu ya Kusimamia Afisi ya Viongozi wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi kwa Mwaka wa Fedha 2017/18.

Awali ya yote nichukue nafasi hii kwanza kabisa nimpongeze Makamu wa Pili wa Rais, pamoja na Mawaziri wote na Manaibu Mawaziri ambao wapo chini ya kamati hii kwa namna wanavyotekeleza majukumu yao.

Pili nimshukuru mtoa mada hoja hii ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Omar Seif Abeid, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii ya Kudumu ya Kusimamia Viongozi Wakuu kwa namna walivyowasilisha taarifa yao hii mbele yetu nasi tukapata fursa ya kuweza kuichangia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze ukurasa wa 3 kwenye Tume ya Kitaifa ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Kwanza tuwashukuru viongozi wakiongozwa na ACP Heriyangu Mgeni Khamis, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tume hii, kwa namna anavyojitahidi kuhakikisha kwamba dawa za kulevya zinapungua nchini. Tuwapongeze kwa kazi kubwa na ngumu ambayo wanayo, licha ya kwamba kunachangamoto nyingi, tunawasihi kwamba wajitahidi kuchapakazi na sisi viongozi wenzao tuko nyuma yao kuhakikisha Wimbi hili la dawa za kulevya linapungua nchi kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, Tume hii ya kuratibu dawa za kulevya kwa kweli ina mazingira magumu sana, ipo haja kwa serikali iangalie hasa lile jengo lao limechakaa sana na wao wenyewe wamebanana banana. Tume hii ina majukumu mazito basi iendane na hadhi ya jengo. Jengo lao kwa kweli si zuri, ipo haja ya kuwapatia fedha, basi kule Kidimni walikokabidhiwa jengo lile la Kurekebisha Tabia ya Vijana wetu basi watengewe eneo kule wajenge jengo lao la kiofisi kama Afisi nyengine hizi hamna

kuliko kuweza kubanana eneo lile alilokuwepo pale kwa kweli inatilisha huruma sana.

Lakini pia wana uhaba sana wa wafanyakazi, kwa hivyo wizara hii ya Afisi ya Rais Makamu wa Pili wa Rais ishirikiane na Afisi ya Katiba na Sheria na Utumishi wa Umma ili kuhakikisha kwamba inawapatia wafanyakazi wa kutosha ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa vizuri zaidi. Kwa upande wa Pemba pengine wafanyakazi hata 10 hawafiki, sasa tutizame Pemba ilivyopanuka miji ya Chakechake, Wete na Mkoani ilivyozidi kuwa mikubwa na halafu wafanyakazi wao wenyewe ni wachache sana. Ipo haja Mhe. Waziri kuangalia suala zima la uhaba wa wafanyakazi kwenye Tume hii ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, halikadhalika kuna suala la usafiri hawa wenzetu wanafanya kazi sana ya kutoa taaluma katika maeneo tofauti. Wanakwenda kwenye taasisi za serikali, NGO`s lakini vile vile wanakwenda katika maskuli katika Wilaya zote, gari iliyokuwepo ya Mkurugenzi tu. Sasa Mkurugenzi kama ana shughuli zake nyengine basi zile program ambazo wamezipanga za kutoa elimu katika maeneo mengine zinaweza zikakwama. Niwaombe wawapatiwe usafiri wenzetu hawa ili waweze kutoa elimu zao.

Ipo haja kwa Tume hii kufanya semina maalum kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa sababu sisi ni wadau muhimu hasa katika suala zima la vita kwa dawa za kulevya. Umefika wakati Tume pamoja wakishirikiana na Wizara hii ya Afisi ya Makamu wa pili wa Rais, kuandaa semina maalum ya siku nzima kwa kubadilishana mawazo namna gani ya kuweza kutafuta njia ya kupunguza hizi athari pamoja na udhibiti wa dawa za kulevya nchini.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoka hapo kwenye Tume ya Dawa za Kulevya niende kwenye ukurasa wa sita kwenye Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Tuwapongeze wenzetu wa Tume ya Uchaguzi kwa kazi kubwa ambayo wameifanya licha ya kwamba wapo mwishoni mwishoni kumaliza muda wao wa miaka mitano. Tumshukuru Mwenyekiti wa Tume pamoja na Wakurugenzi na watendaji wengine wa Tume hii ya Tume ya Uchaguzi. Tuwasihi tu kwamba kama tulivyopitisha ule Mswada wa Sheria ya Uchaguzi kabla ya kufika uchaguzi wa mwaka 2020 tuhakikishe basi Afisi za Uchaguzi za Wilaya ziwe zimeshakamilika ili kila Wilaya basi iwe na Afisi yake kuliko tukawa tunajibana katika jengo moja Wilaya zote zipo katika jengo hilo hilo. Tujitahidi kabla ya uchaguzi Afisi hizo za Wilaya ziwe zimekamilika.

Mhe. Mwenyekiti, halikadhalika uongozi wa Tume ya Uchaguzi uwe makini sana na wataalamu wao wa IT. Kitengo cha IT cha Tume ya Uchaguzi kwa kweli ndiyo roho ya nchi, wapiga kura wote wapo pale katika *data base*. Kwa hivyo kama hatukuwa na watu ambao wazalendo wana uchungu wa nchi yao, kwa kweli wanaweza wakakwamisha na wakaharibu ile dhana nzima ya kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi. Tunasema kwamba lazima wawe makini na wataalamu hawa, kwa sababu katika uchaguzi uliopita katika jimbo langu kwa kweli ilileta mkanganyiko kwa baadhi ya wapiga kura. Wapiga kura wapo katika jimbo la Fuoni lakini wamekwenda kupiga kura katika majimbo mengine kabisa. Kuna wapiga kura kama katika Shehia ya Mambosasa walimepiga katika jimbo la Pangawe, wapiga kura wa Shehia ya Migombani na Shehia ya Kipungani ambayo wapo katika jimbo la Fuoni wamepiga kura katika jimbo la Kijitoupele, lakini kuna wengine wapo katika Shehia ya Chunga ambao ni Fuoni yenyewe wamepiga kura jimbo la Dimani.

Mhe. Mwenyekiti, wapiga kura wangu wa jimbo la Fuoni wengi wamepiga kura katika majimbo mengine ya jirani na mimi

nikabakishiwa wapiga kura kidogo na wengine wakadhani kwamba jimbo la Fuoni linawapiga kura wachache sana. Dhana hii kwa kweli si kweli jimbo la Fuoni halina wapiga kura wachache, lakini kutokana na mkanganyiko uliotokezea na hasa hawa wataalamu wa IT wamesababisha kuonekana jimbo la Fuoni linawapiga kuwa wachache. Tunaomba sana wenzetu wa Tume tunajua wanafanya kazi kubwa na ngumu, lakini tunawashauri hasa katika hii IT inayohusiana na *data base* ya wapiga kura basi kwa kweli wawe makini sana. Tupate vijana wataalam wenye uchungu wa nchi yao na wasiorubuniwa. Kwa sababu tunashuhudia kwamba kipindi cha uchaguzi kile pesa zinakuwa nje nje kwa hivyo mtu yeyote ukimpeleka pale ambaye roho yake kidogo hakuiweza vizuri basi anaweza akapoteza ile dhana nzima ya Tume yetu hii ya uchaguzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 9 kwenye Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa. Tunashukuru juhudi ambazo zinafanywa na Kamisheni hii lakini nathubutu kusema bado kuna maeneo Kamisheni hii bado haijafikia na ambayo yanakumbwa na maafa kila wakati wa mvua zinaponyesha. Mfano mzuri katika jimbo langu la Fuoni kwenye eneo la Fuoni Kiembeni, Mambosasa Angaza, kuna Bonde la Jangamizini pamoja na Bonde la Kibondemzungu. Kwa kweli maeneo haya niliyoyataja katika jimbo la Fuoni yanakabiliwa na mafuriko wakati wa mvua za mara kwa mara.

Tunaiomba hii Kamisheni ya kukabiliana na maafa iende katika maeneo haya na ifanye tathmini ya kutafuta njia bora zaidi ya kuweza kuyaondoa maji haya na kuyapeleka katika sehemu nyengine ili yasilete madhara zaidi. Tumeshuhudia kama pale Kibonde Mzungu watu wawili katika msimu wa mvua zilizopita wamefariki dunia. Kwa hivyo laitani kama yale maji yangekuwa hayatuwami pale mimi nadhani madhara haya yasingetokezea. Kwa hivyo Kamisheni hii ya maafa ijikite zaidi katika kutafuta

njia bora zaidi ya kuweza kutatua tatizo na iliangalie zaidi chanzo cha tatizo lile ni nini halafu wao watafute dawa ya kuweza kutusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, hapa vile vile niiombe serikali kwa ujumla kwa kweli serikali imefanya kazi kubwa sana kuondoa maji pale Mpendae, lakini na huku eneo la Karakana Chumbuni, sasa tutaona kwamba zaidi serikali imejikita kwa upande wa mjini, lakini upande wa Magharibi "A" na "B" bado juhudi kidogo naona hazijawa kubwa zaidi. Tunaomba sisi wana Magharibi "A" na Magharibi "B" serikali itutizame kwa jicho la huruma zaidi ili zile sehemu zinazoleta athari kama Ziwamaboga, Mwanakwerekwe na maeneo ambayo nimeyataja ya Fuoni kwa upande wa Magharibi "B" na hata zile Magharibi "A" basi yaweze kutatuliwa matatizo haya na madhara mengi yataweza kupungua.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo kubwa hasa kwa upande wa Magharibi zote mbili hatuna mfumo mzuri wa maji taka *(drainage system)* hatuna kwa upande wa Wilaya ya Mjini hakuna tatizo, lakini kwa upande wa Wilaya ya Magharibi hizi mbili hatuna. Lazima serikali ikae, ifikirie na iandae mfumo maalum kwa upande wa Magharibi zote mbili "A" na "B" kwa ajili ya kufanya *drainage system* ya maji haya na kuyapeleka baharini au sehemu nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile njia nyengine ni kuweza kuyavuna haya maji ya mvua, tunaona kwamba kipindi kile cha mvua tunakuwa tuna maji mengi sana, lakini maji yanapotea bure bure. Tutafute wataalamu wetu tutizame njia nzuri ya kuweza kuyavuna haya maji ya mvua ambayo yanaleta athari, kwa hivyo badala ya kuleta athari yawe yanaleta faida, tuyageuze na yaweze kutumika maji kwa ajili ya matumizi mengine ya baadaye, kama kipindi cha kiangazi au katika masuala la kumwagilia maji.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 12, kwenye Baraza letu hili la Wawakilishi. Imezungumzwa kwenye kitabu hichi cha Kamati changamoto kubwa ni suala la *echo*, kwa hivyo tuwakumbushe wenzetu na tuwasisitize kwamba suala la *echo* linaathiri mawasiliano mazuri katika Baraza letu hili, ipo haja ya kulitafutia ufumbuzi kwa hali na mali.

Lakini la pili katika Ofisi zetu zile za mikutano midogo kule juu, hasa ile ya Kamati, kwa kweli inakuwa haiko rafiki zaidi, *Air Condition* kule nako inakuwa haifiki. Kwa hivyo ipo haja ya kufanya *modification* yoyote kuhakikisha kwamba basi na vyumba vyetu vile vya mikutano midogo ya kamati vinakuwa rafiki kwa ajili ya mikutano kuliko ilivyo hivi sasa. Hivi sasa hali hairidhishi, utulivu unakuwa mdogo katika vikao vyetu vile kutokana na mazingira yaliyopo. Hivyo, Wizara hii kwa kushirikiana na Baraza letu hili basi litafute namna ya kuweza kulitatua tatizo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 17 kwenye Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa. Tupongeze tu kwamba Idara hii ya sherehe imefanya kazi kubwa sana hasa katika sherehe zetu za kutimia miaka 54 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Lakini Waswahili wanasema kila penye mafanikio hapakosi mapungufu ya hapa na pale. Mimi hapa nataka nishauri jambo dogo tu ambalo kidogo limeleta stofahamu kwa baadhi ya viongozi wetu. Utoaji wa kadi za mialiko katika masuala ya uzinduzi wa miradi mbali mbali au sherehe hizi za Mapinduzi baadhi ya viongozi wanakuwa hawapati kadi hizi za mialiko ya uzinduzi pamoja na uwekaji wa mawe ya msingi. Sasa tungeomba hii idara ijitahidi sana katika kutoa hizi kadi kwa viongozi wote wanaostahiki.

Nimeshuhudia tukio moja pale tarehe 4 Januari, Mhe. Rais alipokuwa akifungua jengo lile la Takwimu, ile sherehe ilifanyika ndani, kama huna kadi huwezi kuingia, alikuja kiongozi mmoja

pale akadaiwa kadi akasema mimi kadi sikupata, akaambiwa kama hukupata kadi inabidi urudi. Hiyo *function* ambayo imefanyika iko ndani ya Wilaya yake. Lazima hizi changamoto tujaribu kuzitafutia ufumbuzi ili zisije zikarejea tena. Tunajifunza kutokana na makosa ambayo yametokezea. Sheria zinazokuja japo kwamba sheria hizo zitakuwa zipo Pemba lakini hii itasaidia sana sherehe nyengine ambazo zitafanyika hapa Unguja. Tuhakikishe kwamba katika masuala yote ya miradi ya maendeleo basi kadi, viongozi wote katika Wilaya ile au katika Mikoa ile basi wanapata kadi na kama kadi ni kidogo basi Idara ifanye juhusi ya kuchapisha kadi nyingi zaidi ili viongozi wengi zaidi waweze kushiriki kikamilifu katika sheria zile kwa sababu zile sherehe ni zetu sote.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba umalize kwa sababu muda wako umeisha.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Haya namalizia kwa suala moja tu hili ukurasa wa 19, katika changamoto iliyokuwepo hapa Kamati inasema kwamba Makamo wetu wa Pili hana Ofisi ya Uhakika kule Pemba. Sasa najiuliza kipindi chote hicho hana Afisi ya uhakika, kwa nini tumechelewa kiasi hicho, bajeti nyingi tunapitisha hapa, hii itakuwa ni bajeti ya nane kwa awamu hii ya Saba. Tuwaombe tu wahusika waharakishe ujenzi wa nyumba ya Kiongozi wetu huyo anapokuwa kule Pemba basi iweze kutengenezwa na awe na uhakika sasa makaazi yake akiwa kule Pemba.

Baada ya maelezo hayo machache sana Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Fuoni tunaunga mkono hoja hii ya Mhe. Mwenyekiti kwa asilimia 100. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Yussuf Hassan Iddi kwa mchango wako sasa naomba nimwite Mhe.

Mohammedraza Hasanaali Mohamedali atafuatiwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi na Mhe. Jaku Hashim Ayoub ajiandae.

Mhe. Mohammedraza Hasanaali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti kwanza awali ya yote napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi nikaweza kufika hapa.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja kuwashukuru Afisi mbili hizi kubwa za viongozi ambao ziliwasilishwa mbele yetu kwenye Baraza hili la Wawakilishi asubuhi hii. Changamoto na mambo ambayo wanayabili viongozi hawa katika Wizara zao. Mimi nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na wasaidizi wake wote pamoja na Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na uongozi wake mzima kwa hekma na busara na usikivu wanaokuwa nao.

Mhe. Mwenyekiti, katika ripoti hii kwa ujumla ningependa nizungumzie sehemu zote mbili kwa pamoja, changamoto kubwa ambazo zilikuwa zimewasilishwa kwetu sisi kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi *challenge* iliyokuwa ni zana za kufanyia kazi. Zana za kufanyia kazi maana yake kunahitajika mapato, kunahitajika fedha, kwa hivyo tukizunguka sote humu ndani tunakuja pale pale kwamba kubwa serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo inaongozwa na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein inajitahidi sana pamoja na watendaji wake wote yaani wasaidizi wake katika utafutaji wa fedha.

Utakuta kwamba ripoti hii inazungumza kwamba kuna uhaba wa fedha. Serikali yetu sikivu inataka kusaidia sehemu zote na kubwa leo Mhe. Mwenyekiti, imezungumzwa suala la walemavu, suala la maafa ma mambo mengi mengineyo yaliozungumzwa sasa Mhe.

Mwenyekiti, mimi ningeliomba serikali kwa upande wa walemavu.

Mhe. Mwenyekiti, sisi pale ni viongozi wa wawakilishi lakini ni wafanyabiashara tuna zaka vile vile za kutoa. Sasa nilikuwa naomba Mhe. Mwenyekiti, Wizara inayohusika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwamba mtupe takwimu *statistic* za majimbo yote ya Unguja na Pemba ili tuone tunasaidia vipi kwasababu mimi nikisimama nikianza Uzini kuna walemavu wangapi hatuwezi kufika, lazima tuwe tunajali sehemu yote. kwasababu tunapozungumza siye tunakuwa na *freedom* ya kuzungumza majimbo yetu lakini mawaziri wanakuwa hawana sauti ya kuzungumza kwa sababu wako mbele wao wanatakiwa ku *defend*, kwa hiyo uzuri wa *fairness* jambo kama hili
Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nipate takwimu ya majimbo yote ya Unguja na Pemba katika masuala ya vitendea kazi kama *wheelchair*, milango mitatu pamoja na vifimbo halafu tuone tunaweza kusaidiana vipi.

Mhe. Mwenyekiti, jambo lolote wahisani, wafanyabiashara ndio siye na siye wakati mwengine tuna mvuto kwa wafanyabiashara kutoka nje. Kwa hivyo mimi ningeliomba kuanzia jimbo langu la Uzini na majimbo yote kuanzia Micheweni mpaka Makunduchi nipate tathmini orodha ya mahitaji ya majimbo yote *wheelchair* zana zote baskeli ya miguu mitatu halafu tuone vipi tunashirikiana kuwezesha ndugu zetu hawa ambao wamepata mtihani wa Mwenyezi Mungu tunaweza kuwakabili na kuwasaidia maisha yao ya vitendea kazi.

Mhe. Mwenyekiti, suala la walemavu wanapenda kujituma hivyo kuna wakati mwengine wanashinda na *wheelchair* au maringi matatu yale, lakini wanaweza kuwa na shamba zuri, wanaweza kuwa na kilimo, wakiwa na hamu ya kufanya kazi ya kilimo lakini ile nyenzo ya baskeli kumpeleka shambani pengine hali yake

ngumu. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeliomba kwamba tutizame maslahi ya sehemu zote zinazohusika halafu tujithamini. Mimi nashukuru Mhe. Jaku yuko nani wote wafanya biashara Mhe. Ahmada sote humu kuna wajibu wa kusaidia jamii kwa pamoja kuliko kwenda na moja moja ili kuona tatizo hili tunaweza kulitatua na Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nikuhakikishe kwa uwezo wa mwenyezi Mungu kwa Zanzibar tulivyo na utamaduni wa Zanzibar uwezo, nia tunayo na tunaweza kundosha matatizo haya ya walemavu na watu ambao wanahitaji mahitaji muhimu.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba wizara inayuhusika ikanipatia takwimu ya majimbo yote ili na mimi naweza kwenda na mvuto wangu nikawakusanya wafanyabiashara huyu akatoa *wheelchair* nne, huyu akatoa fimbo, tukapeleka sehemu zote na niwaombe wawakilishi na sisi vile vile tuoneshe nia ya kuisaidia Serikali yetu, kusaidia majimbo yetu kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naliomba sana katika hili.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, katika suala zima la maafa najua Mhe. Mwenyekiti, mitihani hii huja na Mwenyezi Mungu yanapokuja mafuriko huwezi kuyazuwia ni kwasababu ni Mwenyezi Mungu atatuletea neema ile hatuwezi kuwa ni kisirani, kwa hivyo lazima tujipange lazima tujuwe kwamba mwaka jana tulipata matatizo ya mafuriko maji huwezi kuyazuia ni kazi ya Mwenyezi Mungu yakisha kutua sasa unaweza kuyazuwia lakini ikija mvua huna njia ya kuyazuwia na kuyapeleka. Kwa hivyo mimi nitowe rai yangu kwamba tutizame tathmini ya mwaka jana Mwenyezi Mungu akitujaalia *inshaallah* atuepushe na mambo haya masika kesho kutwa Mhe. Mwenyekiti, jee uko nyuma tumejitayarisha vipi kwmba kulitokea na maafa tumefanya vipi *statistic* inasemaje, wataalamu wanatuambiaje ili tuweze kuona kwamba maafa yake yanatokea tuyaweze kuyakabili.

Lakini mara nyingi katika maafa haya Mhe. Mwenyekiti, tunakuja kuyavaa mara moja badili ya kutumia shilingi mia na mtihani unapokuja unakuja kutumia milioni moja. Kwa hivyo mimi nasema Mhe. Mwenyekiti, niombe serikali mawaziri wanaohusika wizara hii wakae tufanye tathimini jee maafa haya mvua ya masika lazima kwasababu ninachoomba mimi kwamba tufanye utaratibu mzima Mhe. Mwenyekiti, ya kutizama maafa haya tumejikinga vipi.

Halafu Mhe. Mwenyekit,i ningeliomba Kamati ya Maafa ikatupa vile vile wakati mwengine kunakuwa la *challenge statistic* jamani Kamati ya Maafa iko sehemu fulani tuandikiwe kwamba bwana hapa patakuwa panahitajika mabati, panahitajika chakula, panahitajika saruji kuweko na *statistic* za kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, tusisubiri jambo ambalo linaweza likatuathiri na jambo hili Mheshimiwa tusha-*experience* miaka mingi. Mimi nimshukuru Rais wa Zanzibar na Makamu wa Pili wa Rais baada ya mambo haya utakuta sehemu zote wanaanza kuhangaika.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi niombe taasisi zinazohusika mawaziri kuwepo na *coordination* kitu kikubwa Mhe. Mwenyekiti, ni *communication*. *Communication* inasaidia mambo mengi ni mawasiliano kwa hivyo uzuri wa mambo kama hayo tunakwenda na *statistic* zetu tunajua kwamba sasa hapa tuna tatizo hata wakati mtu anapotaka kutoa misaada tunamwambia bwana tuna chakula cha kutosha lakini sasa hivi haja yetu mabati, haja yetu maji kwa hivyo twendeni na utaratibu ambao utaweza kusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipokuwa kabla sijaumwa mwaka jana mwezi wa Mei palipotokea na maafa haya Mwenyezi Mungu alinijaalia mimi na ndugu yangu Bopar na Ahmada tulikabidhi tenda ya chakula kwa Unguja na Pemba. Lakini bado tunasema

kwamba watu wote wanapenda nchi yao kwa hivyo kwa uzuri Mhe. Mwenyekiti, tukaelekezwa tukafanya *statistic* ili kuona tunasaidia na pale sehemu ambayo yalipotokea tuone mambo yake yanatekelezeka.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa niombe kwa watendaji tuwe wa kweli kwa viongozi wetu sisi tunaomba sana kwa sababu kubwa naona sisemi kwamba watendaji wote lakini pia anayepepesuka mlevi, lakini watendaji tunapofika kwa viongozi lazima tume wa kweli tuwape vitu ambavyo vitasaidia kwa nchi si kuigawa nchi. Sasa uzuri kwa watendaji wanapofika kwa viongozi wakuu jambo ambalo na Rais alisema mimi namshukuru Rais alituambia Baraza la Wawakilishi, aliwaambia watendaji, aliwambia mawaziri jamani kama hakuna jibu la uhakika rudini katuambia Rais mara nyingi. Kwa hivyo, Rais amekuwa ni mtu ambaye ametunyooshea katika njia *Siratul Mustakin.* Kwa hivyo na mimi ninafikiri tuwe na haja sisi watendaji tuwe wakweli ili kusaidia nchi yetu katika mazingira mengi ya matatizo ya kundosha.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti mimi nilikuwa naomba sana mambo kama haya maafa tulikuwa tunazungumza, mambo ya walemavu wengine wana hali mbaya wagonjwa kwa hivyo tuone njia sasa ya kuweza kusaidia katika hali hii.

Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kutoa wito kwa wafanyabiashara suala la kodi ni jambo muhimu sana iwe kila wakati sisi tukisimama tuhimize kodi si kupunguza kodi. Kwa sababu Baraza la Wawakilishi tunakaa ndani kila mjumbe akisimama anazungumza kwamba jimbo jale halina maji, barabara mbovu, afya hakuna lakini mjumbe huyo anasimama watu wasemehewe kodi, watu wapunguziwe kodi sasa *we have to be very serious*, tufike mahala sote tujuwe umuhumu wa ulipaji wa kodi, tujuwe kwamba hizi kodi tumeingia hapa kwenye Baraza la

Wawakilishi tuwe na *interest* ya nchi, tuwe na *interest* ya kuweza kukaa kwa pamoja kuona kodi zinalipwa.

Kw hivyo Mhe. Mwenyekiti, wito wangu mimi tunapofika ndani kwasababu siye ndio tunawakilisha wananchi sote humu wawakilishi wa wananchi na tunakwenda huko tunakuja kuishambulia serikali Rais fanya nini, serikali sio sikivu, balozi katoa ahadi hakuna naleta hoja binafsi lakini suala la kodi lazima tuwe kipa umbele wa kusimama kwamba kodi zetu bado Mheshimiwa katika Afrika ya Mashariki na ya Kati, katika *West Africa* kwa Zanzibar kodi ni ndogo sana. Mhe. Mwenyekiti, mimi namshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa huruma zake alikuwa nazo na wasaidizi wake.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi niombe sana kwamba tutafute njia za kuongeza angalau sisi wawakilishi tupewe nyenzo. Leo tutasimama Wizara ya Mawasiliano inakuja, Wizara ya Maji inakuja, barabara tunao watendaji wazuri, tunao ma *engineer* wazuri lakini kote kunahitajika fedha, kifusi kinahitajika fedha, kokoto zinahitajika fedha na serikali yetu hii inachokipata ndio inachotumia. Kwa hivyo, mimi niombe sana wenzangu na sote sisi kwamba tuelekeze kuisaidia serikali, tuelekeze nini tutaisaidia serikali na nini tunaweza kutoa mchango wetu kwa serikali.

Lakini vile vile namna gani namna ya kuwaelemisha wafanya biashara wa kuweza kusaidia kulipa kodi mimi Mhe. Mwenyekiti, haya mambo mengine hizo kampeni zilokuwa za kesho kesho ndio hayo tuliokuwa tnasema kesho, kesho, kesho hatuwezi kufika hakuna taasisi moja ya Zanzibar inayotoza kodi kama Zanzibar kuliko Afrika nzima na Tanzania kwa hivyo huo ndio ukweli wa jambo lazima tuwe wa kweli Mheshimiwa, lakini tufike tuzungumze maslahi ya nchi hatuwezi kufika ukasema umimi, umimi, *those base have gone* ule wakati umekwenda.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, huku ndani tumechukua msahafu, tumekula kiapo kwa jina la Mwenyezi Mungu, lazima tuwe wa kweli tutizame jinsi gani, tukosoane tuzungumze lakini jiambie wewe umeifanyia nini Zanzibar...

Mhe. Mwenyekiti: Malizia Mheshimiwa...

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali: *This is very important*. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi nishukuru wizara zote mbili hizi kwa usikivu wao niwashukuru na watendaji na naamini na watendaji watabadilika ili tuone vipi tunaweza kuendesha nchi yetu katika hali nzuri ya usalama na kweli nchi yetu imetulia.

Mhe. Mwenyekiti, ile dhana ya leo, kesho, kesho hakuna tena kwa hivyo sasa hivi kazi yetu kubwa tutekeleze ilani ya chama tunarejea kwa wananchi tunakwenda kuwaelezea wananchi Chama cha Mapinduzi kimefanya jambo gani hilo ni jambo muhimu sana kwa hivyo, nguvu zetu zote tuelekeze kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakushukuru sana nazishukuru wizara zote mbili hizi kwa kazi nzuri zilofika lakini niombe wizara mbili sasa kuweko na mawasiliano, kuweko na utaratibu mzuri sisi wananchi Mwenyezi Mungu aliotujaalia kwamba bila ya wananchi hata mimi nisingelifika hapa. Hiyo namshukuru Mwenyezi Mungu nawashukuru wananchi wangu wa Zanzibar bila ya wao mimi nisingefika hapa, bila ya Mapinduzi ya Zanzibar nisingelifika hapa mbele ya Baraza la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nashukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mohammedraza kwa mchango wako sasa naomba nimiwite Mhe. Rashid Makame

Shamsi atafuatiwa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Khadija Omar ajiandae.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa michango yangu katika ripoti hii ya Ofisi za Viongozi Wakuu wa Serikali.

Awali niipongeze Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu kwa ripoti yao nzuri iliyopangika iliyosheheni mambo yote muhimu, hususan nimpongeze mwenyekiti kwa usasilishaji wake Shekh Omar Seif Abeid. Lakini vile vile nichukuwe fursa hii kuwapongeza watendaji wote wa ofisi za viongozi kwa juhudi kubwa wanayoichukua katika kusimamia vyema majukumu yao akiwemo Mhe. Rais na watendaji wake pamoja na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze wajumbe wote ambao wamechangia ripoti hii kwa michango yao mizuri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba mimi nielekee katika mambo manne muhimu pamoja na kwamba wajumbe wengine wamekwisha yakazia lakini na mimi naona kuna haja ya kuweza michango yangu kuielekeza huko kutokana na umuhimu wa taasisi hizi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na Tume ya Kitaifa ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Mhe. Mwenyekiti, tume hii ni muhimu sana katika suala zima la janga tulilonalo la madawa ya kulevya na tuipongeze kwa kazi zake ambazo inazifanya.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye changamoto hususan changamoto ya tano ambayo wenzetu wana kamati walibaini kwamba kuna kuokosekana kwa takwimu na taarifa juu ya skuli zilizopatiwa elimu kuhusu madawa ya kulevya, ili tufahamu kiwango cha idadi ya skuli zilizofikiwa kwa kipindi cha mwaka 2017/2018.

Mhe. Mwenyekiti, hii inasikitisha kidogo kama Tume inakosa kuwa na takwimu sahihi na taarifa juu ya skuli ambazo wamezipatia elimu hapa kidogo kunahitaji marekekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, katika ulimwengu huu hatuwezi kufanya mambo muhimu kama haya bila ya kuwa takwimu sahihi na hususan kwamba suala la madawa ya kulevya hivi sasa pamoja na kuendelea kulidhibiti lakini vijana wengi wanajishughulisha au wanajiingiza katika suala hili la madawa ya kulevya na wengi wao wanaanza kuwa katika ngazi ya wanafunzi. Kwa hiyo, kuna haja ya kuwa na takwimu muhimu lakini vile vile kuna haja ya kuendelea kupita katika maskuli mbali mbali ili kuweza kutowa elimu hii ili vijana wetu wasijiingize katika janga hili ambalo linaumiza nguvu kazi ya taifa.

Mhe. Mwenyekiti, katika chagamoto ya nane ambayo wenzetu kamati wameibaini imesema kutoshirikishwa kikamilifu Wakuu wa Mikoa katika kupata taarifa ili kudhibiti madawa ya kulevya nchini.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ushirikishwaji wa Wakuu wa Mikoa na hata Wakuu wa Wilaya ni suala ambalo halina mbadala kama tunataka tupige vita na kuweza kuondosha janga hili ya madawa ya kulevya nchini. Wakuu wa Mikoa ndio wasimamizi wa Mikoa yao na Wakuu wa Wilaya ni wasimamizi katika Wilaya zao. Kwa hiyo kuna umuhimu mkubwa sana wa Tume yetu hii kuweza kuwashirikisha viongozi hao ili kuona kwamba wanasaidiana na Tume kuona kwamba tunapunguza na hatimaye kuondosha kwa kiasi kubwa suala la madawa yakulevya nchini.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nielekee katika Tume ya Uchaguzi katika ukurasa wa sita Tume ya Uchaguzi imezunguzumziwa na changamoto mbali mbali ikiwemo ghala, vyombo vya usafiri, majengo ya kudumu na uhaba wa wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Uchaguzi ni moja kati ya chombo muhimu sana, Tume ya Uchaguzi ni sawa sawa na Baraza la Mitihani katika nchi, lazima liwe na *candidate* na *candidate* wa Tume ya Uchaguzi ni sisi ambao tumo katika Baraza hili. Maana yake uwepo wetu basi ni mchango mkubwa sana wa kazi za Tume ya Uchaguzi Zanzibar. Kwa hiyo, kutokana na changamoto hizi mimi niombe sana serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuweza kuzitazama changamoto hizi na kuweze kuzifanyia kazi mapema kwasababu tume yetu ina majukumu mengi.

Kwa hiyo, tunapaswa kuweza kujiandaa mapema tusisubiri elfu 2020 tume iweze kupunguziwa yale matatizo yake mbali ili iweze kujipanga vizuri, Tume inahitaji kufuatilia mambo mbali mbali, inahitaji kutoa elimu, inahitaji kuweka kumbukumbu lakini katika kitabu hiki tumeona hata vifaa vya tume vyengine vinahifadhiwa katika majengo ambayo siyo ya tume ambayo hii Mhe. Mwenyekiti ni hatari, vifaa vinavyohusiana na Tume ya Uchaguzi kuhifadhiwa katika maghala ambayo sio yake hii ni hatari kubwa sana. Kwa hiyo niombe serikali iweze kutizama changamoto za Tume ili kuweza kuona kwamba Tume inafanya majukumu yake kama tulivyo itarajia ili na sisi watahiniwa au *candidate* wa tume basi tuone kwamba tunarudi tena elfu 2020.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika Wakala wa Serikali wa Uchapaji. Mhe. Mwenyekiti, hiki ni chombo muhimu sana katika serikali zote ulimenguni lazima ziwe na *government press* yake, lakini kidogo katika changamoto ambazo kamati imebaini ningependa kuzungumzia kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, lengo la wakala huyu wa serikali ili iweze kuweza kujiendesha au kujitegemea tukizungumza wakala aweze kujitegemea maana yake tunazungumzia wakala aweze kufanya biashara. Sasa inashitusha katika changamoto tunaambiwa

kwamba kuna uhaba wa soko, lakini ukiacha uhaba wa soko tunaambiwa kuna upungufu wa wafanyakazi, kuna wafanyakazi muhimu wanaohusiana na biashara.

Mhe. Mwenyekiti, kama unataka kufanya biashara lazima uwe na wataalamu wa mambo ya uchumi, biashara na masoko. Kwa hiyo, niiombe serikali kama wafanyakazi hawa hawapo katika wakala wa uchapaji, basi tuweze kuwaajiri wafanyakazi ambao wana utaalamu wa mambo ya biashara na masoko hapo wanaweza kuratibu vyema. Mhe. Mwenyekiti, lakini sio hilo tu, suala la wakala wetu kama tunataka ajiendeshe na kufanya biashara lazima aweze kusoma hali ya soko ilivyo. Soko letu katika mambo ya uchapaji hivi sasa lina ushindani mkubwa sana. Kwa hiyo, tunalazimika kusoma vizuri ushindani uliopo wenzetu wana nini, wanatoa huduma gani ili na sisi tuweze kujipanga. Lakini baada ya kuona hali hiyo tunapaswa kuwa na mtaji. Niingeiomba sana serikali baada ya kukamilika hayo kuweza kuiwezesha wakala huyu kuweza kupatiwa mtaji wa kuweza kuendesha biashara ya ushindani, vyenginevyo taasisi hii itategemea ruzuku kwa muda mrefu sana.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la kuendesha biashara inahitaji ubunifu na utengenezaji wa vitu ambavyo vinahitajika katika soko. Sasa hili ni muhimu sana kwa wakala wetu kuweza kuwa na ubunifu, kuna kazi nyingi sana akiweza kubuni wakala wetu basi taasisi hii inaweza kujiendesha. Lakini kubwa zaidi ni kuweza kujitangaza, tuwapongeze sana wakala wetu huyu anajitangaza. Mimi nimeshuhudia wakala wetu katika maonesho ya saba saba pale Dar es Salaam alikwenda na baadhi ya bidhaa tuliziona, lakini nashangaa unaweza ukakaa siku chungu nzima huwezi ukaona matangazo katika TV juu ya wakala wetu. Sasa hatuwezi kujiridhisha tu kwamba tuna taasisi ya uchapaji lakini hatujitangazi, bila ya kujitangaza maana yake taasisi hii haiwezi kwenda. Kuna usemi hapa ulizungumzwa kwamba zamani

kulikuwa na usemi unaosema kwamba "chema chajiuza kibaya chajitembeza". Lakini katika ushindani huu wa biashara basi chema na kibaya pia vinapaswa kujitembeza. Kwa hiyo, lazima taasisi yetu iweze kujitembeza kwa kujitangaza ili iweze kutegemewa na kuweza kujiendesha.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie na taasisi moja muhimu sana, taasisi hii ya Idara ya Usalama wa Serikali (*GSO*). Mhe. Mwenyekiti, changamoto ambazo wenzetu wamezitaja na ambazo nimezibaini kuna ubovu wa uchakavu wa jengo, kuna upungufu wa vitendea kazi na upungufu wa bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, nimefanya *reference* ya Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo wa Kazi za Kamati ya Oktoba, 2017. Katika maagizo ambayo Ofisi ya Rais ilipewa na kamati moja ilikuwa ofisi imeagizwa kulifanyia ukarabati mdogo jengo linalotumika kwa sasa ili liweze kuwa na hali nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, hili ni agizo la ripoti ya mwaka jana, sasa leo tunapoona kwamba tatizo bado linaendelea ina maana labda hakuna utekelezaji. Lakini maelekezo ambayo yalitolewa yalisema hivi katika utekelezaji.

"Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka 2017-2018 imepanga kulifanyia matengenezo madogo jengo la Ofisi ya Usalama wa Serikali kupitia mradi wa maendeleo. Kazi zinatarajiwa kufanyika kwa mwaka huu ili kuezeka upya, kuweka dari, ukarabati wa ndani na matengenezo ya vyoo, kazi hii inatarajiwa kuanza mwezi Novemba, 2017".

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi tuko Februari, 2018 tunapopokea changamoto hii sijui hizi kazi kama zimefanyika au hazikufanyika na kama zimefanyika basi sijui zipi zimebakia. Lakini kutokana

na ripoti hii kazi za ukarabati wa ofisi hii muhimu kwa serikali iwe zimemaliza.

Mhe. Mwenyekiti, ukija katika upungufu wa vifaa kuna agizo Nam. 2 liliwahi kutolewa. Kamati imeshauri wizara kuipatia idara nyenzo za msingi za utendaji kazi ikiwa ni pamoja na samani za ofisi kama vile meza, viti na kompyuta. Mhe. Mwenyekiti, hili ni agizo la mwaka jana na wenzetu katika Ofisi ya Rais katika utekelezaji walisema hivi. Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi imenunua gari moja kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za Ofisi za Usalama wa Serikali. Aidha, mwaka huu 2017-2018 *GSO* itapatiwa samani na zana za kufanyia kazi kwa mujibu wa mahitaji yake. Haya ilikuwa ni mwaka 2017-2018 sasa leo tunapopokea kama kuna changamoto nyengine ya upungufu wa vifaa kwa kweli mimi nashangaa. Tunatarajia kwamba vifaa hivi iwe wameshapatiwa na kama hawajapatiwa basi tujitahidi sana serikali kwa sababu Ofisi ya *GSO* ni ofisi moja muhimu sana katika serikali yoyote duniani. Halafu baya zaidi ofisi hii iko katika nyumba ambayo ina heshima kubwa. Kwa hiyo, tunatarajia vile vile na ofisi hii basi iwe na heshima kubwa ili kuweza kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, katika ofisi hii hii ya *GSO* imezungumziwa juu ya upungufu wa bajeti, lakini nikitazama kitabu cha mwaka jana kulikuwa na agizo Nam.4 kamati imeagiza kuongezewa bajeti idara hii katika bajeti ya mwaka 2017-2018 kwani ni muhimu sana kwa serikali na watumishi wake kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu wa Ofisi ya Rais katika utekelezaji majibu yao yalikuwa kama ifuatavyo:

Kwa mwaka 2017-2018 Ofisi ya Usalama wa Serikali imeongezewa bajeti kutoka shilingi milioni 40,000,000 za Kitanzania hadi shilingi 75,000,000. Hata hivyo, Ofisi ya Rais na

Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi itaangalia uwezekano wa kuongeza bajeti ya Ofisi ya Usalama wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2018-2019 ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, sasa haya ni majibu ya matumaini bajeti imeongezwa na niwapongeze sana Ofisi ya Rais kwa kuongeza bajeti kutoka milioni 40,000,000 kuja milioni 75,000,000, kwa sababu hii ni sawa karibu asilimia 90 ya ongezeko la bajeti. Sasa leo tunapoambiwa bado kuna upungufu wa bajeti mimi nashangaa sana, na vile vile imetolewa ahadi mambo yakiwa mazuri wataongezwa zaidi. Sasa pungufu hili nina wasi wasi nalo kwamba inawezekana aidha ziwe pesa hawajaingiziwa. Kwa hiyo, niiombe serikali kama fungu hili la pesa hawaingiziwi kwa wakati basi waingiziwe lakini ongezeko hili la bajeti ni kubwa sana ofisi hii iweze kujiendesha.

Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hiyo na mimi niunge mkono ripoti hii asilimia mia kwa mia na niwaombe washiriki wengine kuweza kuichangia. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nami nakushukuru Mhe. Rashid Makame Shamsi, sasa naomba nimwite Mhe. Jaku Hashim Ayoub akifatiwa na Mhe. Khadija Omar Kibano na Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii kuchangia jioni hii ya leo, lakini wengi wamezungumza karibu wote waheshimiwa humu ndani kumpongeza Rais, ni haki yao ya msingi kwa kazi anayoifanya sisi sote ni mashahidi. Niwaombe tu wale wanaotaka kutuukanisha na Rais wetu si kitu kizuri kwa lugha wanazozitumia.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kuzipongeza wizara zote mbili na niwatakie kila la kheri viongozi Mhe. Rais, Mhe. Issa Haji Ussi, Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi na Mhe. Mihayo Juma Nhunga.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais alisema katika majumuisho yake Wilaya ya Kusini ameziunda wizara nyingi zitumikie wananchi, sio kila kitu Mhe. Rais. Aliyasema hayo na niwaombe mawaziri wafate nyayo zake Mhe. Rais, Rais amefanya kazi kubwa sana na sisi sote ni mashahidi jinsi anavyotumikia wananchi. Ameondoa ada za elimu wengine wakafata kuona umuhimu wa elimu, kwenye maji tunakwenda tunayaona, mtoto akizaliwa haendi mbio hutambaa akakweta mpaka akakamata kiambaza kidogo kidogo ndio mwendo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais ana msemo nina heshimu mkubwa na mdogo aliyazungumza siku ya tarehe 24/12 alipotokea Dodoma katika kumpongeza Amani na alisema nchi hii hatoiongoza kwa mafamba wala nguvu wala vishindo, na hii ndio sifa ya kiongozi. Pia ana msemo kiongozi hatakiwi awe na kibri, si maneno yangu mwenyewe Mhe. Rais anasema, na ana msemo anasema hakuna kazi inayofanywa na mtu mmoja uwe kiongozi makini. Huu ndio uongozi lakini hapa nitoe masikitiko yangu na kuomba radhi si ujinga. Baadhi ya watendaji wakiwemo mawaziri, manaibu waziri, makatibu wakuu, wakurugenzi mnafika kiongozi wetu mkubwa kumdanganya, dhambi kubwa hii mnayofanya. Haitaki kutaja mifano tutakutana pahala tutaelezana na aliye na wasi wasi na mimi anitafute nitamueleza. Lakini tusimdanganye tunapata dhambi kiongozi kama yule, kiongozi msikifu kwa yule tutampata wapi sisi. Mimi siku moja niko Pemba bango kitita Mhe. Rais anadanganywa machozi yananitoka kwenye bango kitita anadanganywa.

Mhe. Mwenyekiti, kiongozi anajituma usiku na mchana mwenyewe ana msemo anasema zege halilali, tumsaidieni Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na Wakurugenzi kazi anayoifanya kubwa nchi hii nyinyi nyote ni mashahidi. Juzi nimeona neema ile nimwambie tu Mhe. Issa Ussi Haji *rehmatullahi wasiiah,* rehema za Mwenyezi Mungu hakuna wa kuzizuia. Tumepata magari mapya Mawaziri na Manaibu Waziri ni kitu cha kumpongeza Mhe. Rais wakati wenyewe huu mnauona jinsi anavyowajali mawaziri basi msimuangushe Mawaziri na Manaibu Waziri na watendaji wote, msifike mkataka kumdanganya haya mambo yanageuka aliyekuwepo mbele mngoje nyuma. Tufanye kazi kililahi tumsaidieni Mhe. Rais, sisemi kama nataka kujipendekeza mimi aah! Narudia tena tusimuangushe mimi sitaki uwaziri wala unaibu waziri na anaijua elimu yangu kuwa ni ndogo, lakini mnafika pahala mnataka kumdanganya. Niko Pemba mimi machozi yanataka kunitoka kitu kiliniuma ndani ya moyo wangu kile, anaambiwa mambo mazuri, mambo mazuri, Mhe. Mwenyekiti, nimuombe wakati mwengine Mhe. Rais arudi *field* kidogo aangalie.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nimuombe tu na hapa nizungumze kwa lugha nyepesi na kidogo ya unyenyekevu unajua ukizungumza na kiongozi wako kitu cha mwanzo mimi nilifundishwa na walezi wangu ni adabu. Nimuombe kwa lugha nyepesi tu Mhe. Rais ana ahadi kule Michamvi ni ya muda mrefu na wale wazee wangu wanateseka kipindi kirefu hawajui wakati wa kilimo, hawajui wakati wa kwenda hospitali, hawajui wakati wa kwenda skuli maji ni uhai, *wajaalna minalmay kuli-shaiyn* na kila kitu kimetokana na maji. Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Rais kwa lugha nyepesi na kwa unyenyekevu hapa sitaki kutumia lugha huyu ni kiongozi wangu na heshima kitu cha bure na mwanzo nimefundishwa malezi na wazee. Nimuombe hali kidogo si nzuri Michamvi ni ahadi yake Mhe. Rais kwa kipindi kirefu

nahimiza tu na kuna msemo unasema “hoi hei nacho kidindo”. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii tena kumpongeza Mhe. Balozi Seif Ali Iddi. Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Balozi Seif Ali Iddi pindipo nilipompigia simu kuhusu mswada Bungeni wa *ZMA* kutaka kupitisha jamaa na bahati nimekuja nao na nilipokushauri moja kwa moja hukurudi nyuma na ukasikia katika kero za Muungano zimo, ukurasa wa 6.

Not westing subsection (1), matters of maritime administration, maritime environment, safety and security shall apply to the United Republic of Tanzania”.

Mhe. Mwenyekiti, ungepita huu kama si jitihada za Mwenyezi Mungu, wa pili wewe Mhe. Balozi Seif Ali Iddi wa tatu naweza kusema wabunge nikiwemo na mimi maana sitaki kutaka sifa peke yangu, wabunge tuliopelekwa kule, kingepita hiki jahazi ilikuwa tukasajili Bara, meli zote zikasajiliwe Bara. Niliwaambiwa huu Muungano kwa upande mmoja ndani mle au imekuwa kama lugha ya Kiarabu ukiandika unavutia kwako, maana Kiarabu unavutia kwako tu. Kwa umakini huu Mhe. Balozi nikushukuru kwa dhati lakini vyengine vyote ingekuwa mtihani, umefanya jitihada kubwa Mhe. Balozi kutatua kero hii. Lakini nikuombeni bado kero zingalipo sisi wengine mle ndani hata kuchangia inakuwa mitihani Bungeni. Bunge ni la watu wengi utaambiwa muda haupo, lakini naambiwa hili Bunge haliitwi la Tanzania Bara, hili Bunge ni la Jamhuri ya Muungano ikiwemo ya Zanzibar, ndio hapo kidogo natumia *gear* hiyo, lakini kero hizi bado Mhe. Mohammed Aboud Mohammed wewe ni msikivu, kero zitatueni vikao havijakaa.

Nakumbuka kikao labda walipokuja kwenye sherehe za Mapinduzi ndio kikao kikakafanyika Baraza la Wawakilishi la

zamani, twendeni hoi hoi nacho kilindo kama hukusema mtu akakusaidia bado kero zipo tunapata shida. Watu wamezungumza ubalozi tumepata ngapi sisi, nilipigia kelele angalau waongezeke aliniuliza Mhe. Abdalla Maulid Diwani umefanya nini ulipokwenda Bungeni, nikamueleza kwamba nafasi za ubalozi zimeongezeka. Lakini bado changamoto zipo wafanyabiashara wetu na Zanzibar ukiacha karafuu uchumi wake nini mwengine? Ni biashara tutafute mazingira mazuri vita vya panzi neema ya kunguru hapa ndio pakufanya kazi sasa hivi. Biashara ndio uchumi wa nchi hii, wafanyabiashara wanateseka, wanaumia leo gari ikatoka Zanzibar ikienda Tanzania Bara mtihani, ikitoka Bara ikaja huku hakuna tatizo. Lakini hili kidogo huenda likapata ufumbuzi si muda mrefu, hili halina muda huenda likafanikiwa nasikia wakati wowote gari ya Zanzibar kwenda Tanzania Bara ikatumika katika changamoto nilisikia alinambia Mhe. Januari Makamba, sasa sijui kanambia kwa mdomo au ndio vitendo.

Mhe. Mwenyekiti, hizi kero kama hamkufika viongozi wetu na nyengine mtueleze msiogope, kuna tatizo hili na hili sisi ndio wasemaji mengine inabidi tuyatafute wenyewe. Kuna mengi mengine hatuwezi kuyazungumza hapa na kila mtu anasikia, mengine inabidi tuyahifadhi. Hata Mhe. Rais mwenyewe katika ufunguzi wake kwenye jengo lile la Takwimu alisema kuhusu Muungano huu, yeye ni kiongozi mkubwa sitaki kunukuu maneno yake kila wakati. Mhe. Mwenyekiti, jaribuni kukaa wafanyabiashara wanaumia na mimi ni-*declare interest* na mimi ni mfanyabiashara na siwezi kudharau dafu kwa embe ya msimu. Dafu ukiwa nalo kwenye mnazi siku zote utapata embe mwaka hata mwaka ndio izae.

Mhe. Mwenyekiti, nimeshuhudia Mhe. Balozi Ali Karume amekula kiapo wapi, amekula kiapo kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar bahari si mambo ya Muungano. Leo tunafika pale lala inuka twende, leo atakuja kusema mengine tufikirieni jamani

matatizo ni makubwa, nyinyi ombeni tu nasaha zangu Waheshimiwa Mawaziri, Manaibu Waizri tumsaidieni Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub una dakika tatu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana. Mhe. Mwenyekiti, nije katika Baraza letu la Wawakilishi wenzangu wengi sijasikia kitu *echo* tunachozungumza. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mohammed Aboud Mohammed bado *echo* zina matatizo na hiki ni kilio cha muda mrefu si cha juzi wala jana. Wakati mwengine unakuta ukumbi uko mtupu watu wanakwenda kusikiliza kwenye mkahawa huko nyuma ndio ukweli ulivyo *echo* bado. Mhe. Waziri achukue jitihada bado matatizo, hatuelewani kuhusu *echo*. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

Mhe. Khadija Omar Kibano: Ahsante na mimi nashukuru kwa kunipatia nafasi hii nikazungumza machache niliyonayo. Kwanza naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Rais wake wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein. Pili nampongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, nazipongeza ofisi zake mbili zote zilizounda kamati hii, nampongeza mwenyekiti wa kamati hii.

Mimi moja kwa moja niende kwenye Idara ya Walemavu. Idara hii kwa upande wa elimu ya jamii hadi hivi sasa wizara zote, idara au taasisi nyingi hazina wakalimani kama *ZBC* na Baraza la Wawakilishi, hawamo katika kuweka watu hao. Ninachokizungumza mimi ni kuwa walemavu kama hawa viziwi na mabubu wanapokwenda katika kuhudumikiwa katika wizara au hospitali au sehemu yoyote walemavu hawa huwa hawana watu wa kuwashughulikia katika shughuli zao za kibinafsi. Elimu hiyo mjumuisho imetolewa katika wizara mbili tu, ikiwemo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Shirika la *ZBC,* kwa

sababu hawa ndio wanaokuwa wanatoa kwenye masuala ya picha za televisheni.

Mhe. Mwenyekiti, hadi hivi sasa ninachokizungumza kuhusu habari ya walemavu hawa wakienda kwenye huduma za hospitali wakitaka kujieleza hawapati huduma zilizo sahihi kwa watu hawa, kwa sababu hawamo wakalimani wao. Mimi naomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wawapatie elimu kila idara au wizara na wapatikane watu hawa ili kuwaelimisha walemavu kama hawa. Wanapohudumikiwa katika wizara zao wapatiwe huduma kamili. *(Makofi)*

Sasa naelekea katika upande wa *TASAF*. Upande wa *TASAF* kuna watu wengi walikuwa hawamo katika majumuisho ya watu wenye ulemavu, wametengwa na sijui kwa nini hata wakawa hawa hawakupatiwa nafasi za wao kupewa kipaumbele katika huduma za walemavu, kwa sababu hawakupewa kipaumbele walemavu na wao wakaingizwa katika masuala ya *TASAF*.

Mhe. Mwenyekiti, semina zifanyike na elimu itolewe katika wizara zote ili kuelimisha wananchi na wao wapate kujua watu wao kwa masuala ya huduma za walemavu katika idara zao na wizara katika masuala yao ya binafsi. Kwa sababu wanapokwenda katika mawizara huduma hizi hawapati kabisa maana wale wakalimani hawapo. Kwa hivyo, mimi nalisisitiza hili suala lihudumikiwe kwa vilivyo sahihi sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi nilikuwa nataka nieleze hayo kwa mchango wangu, naipongeza ripoti hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana nami nakushukuru Mhe. Khadija Omar Kibano kwa mchango wako, sasa naomba nimwite

Mhe. Ahmada Yahya na atafuatiwa na Mhe. Hassan Khamis Hafidh na Mhe. Masoud Abdalla Masoud ajiandae.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia ripoti hii iliyowasilishwa mbele yetu. Kwa hakika naipongeza kamati kwa jinsi ya taaluma na uwazi ulio wa hali ya juu kuhusu ripoti hii yenye kuonesha mafanikio, changamoto na mambo mbali mbali. Kwa hakika mwenyekiti wake inaonekana ni mtu makini na mahiri, maana yake hakuacha kitu chochote katika ripoti hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitajikita na mchango wangu katika ripoti hii katika ukurasa wa 15 kwenye Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za Serikali Dar es Salaam. Mhe. Mwenyekiti, jengo lenye kutumika kwenye Ofisi ya Uratibu hali yake ni mbaya na ni mbaya mno na ukilinganisha na majengo yenye kukaribiana pale hili limejinamia. Hayo tuliyaona mwezi mmoja nyuma tulipotembelea Kamati yetu ya Ardhi na Mawasiliano tukaiona hali si ya kuridhisha ukilinganisha pahala ilipo ofisi ni pahala *very potential*. Kwa hivyo, juhudi za kukarabati na kulingana na hadhi ya ofisi yaende sambamba.

Kadhalika, hata nyumba ambayo anayoishi Makamu wa Pili inafanyiwa matengenezo. Kwa hivyo, matengenezo hayo pamoja na matengenezo ya Ofisi ya Uratibu yaende sambamba kusudi ile heshima na hadhi ilingane na ofisi yenyewe na nyumba yenyewe. Hiyo *point* ya kwanza.

Nukta *number two* ni kwamba la kufurahisha ofisi hii hii kuna kitengo chetu cha mawasiliano (*ZBC*) kipo palepale na kinatoa habari kila siku. Kwa hiyo, nacho pia madhali wamo kwenye jengo lile basi nacho kadhalika kiboreshwe kiende na mazingira ya kisasa.

Wakati tulipokuwa na Kamati yetu ya Ardhi wiki mbili nyuma muda wote tulikuwanao waandishi wa habari na kwa kweli wanastahiki watunzwe na wapatiwe posho maalum ya mazingira ya Dar es Salaam. Wanawake walioko pale wanafanya kazi nzito na wengine wanakaa nje ya mji yaani wavuke kivuko halafu warudi na imeshawahi kutokezea mpaka saa tatu na nusu tunao, tunaachana njiani wanachukua bodaboda wanarudi. Kwa hivyo, nao kadhalika wakati umefika na wao wapate posho maalum la mazingira maalum ya kutupatia habari nchini kwetu ambazo zinatufurahisha na sasa kitengo kile kimebadilika kinatoa hata ripoti ya *day to day* kwa hiyo, tunawapa hongera sana.

Jengine ambalo linalinganisha na ripoti hii ni kwamba, ofisi inayofanyiwa kazi inahitaji si kuboreshwa tu katika hali ya majengo, lakini hata samani (*funitures*). Wako hoi hailingani na wakati wa sasa hivi. Kwa hivyo, wakati umefika nao wapatiwe samani za kisasa kusudi ilingane na hadhi na heshimia ya serikali yetu. Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache nakwenda kwenye ukurasa mwengine.

Ukurasa wa 16, Kamati inashauri Serikali Kuu kufuatilia suala la upatikanaji wa mgawanyo. Kamati yangu ya Mawasiliano na Ujenzi imekuta kesi hii ya mgawano wa gawio la minara yenye kutumia meli za Kimataifa. Bajeti yao kwa hakika imeathirika sana na Shirika la Meli kwa kuwa wao *every three month* walikuwa wanapata shilingi 300 milioni na sasa zuio lile limezuiliwa mpaka likafika shilingi bilioni moja.

Ripoti inaonesha waratibu wao wamechukua hatua zao za kudai haki ile na ripoti inaonesha sasa hivi tunadai shilingi bilioni moja ukurasa wa 16. Kwa hivyo, juhudi zifanywe kupitia ofisi hii deni lile la shilingi bilioni moja liweze kulipwa Shirika la Bandari.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli wameonesha masikitiko makubwa kamati yetu ilivyotembelea Shirika la Bandari, kwamba fedha zile zimewaparaganya katika bajeti yao ya matumizi. Kwa hivyo, ofisi hii itie mkazo tena zaidi kusudi utaratibu uliorithiwa wa miaka mingi, nasema tena Mwenyekiti, utaratibu uliorithiwa wa miaka mingi wa fedha zile au tozo ile inayolipwa Shirika la Meli uendelee, vyenginevyo bajeti yao imeharibika na imewaathiriwa mno.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache kwa imani moja na kwa yakini wa nafsi yangu ripoti hii ni nzuri na haina mashaka na inafaa ipitishwe kwa asilimia mia moja. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nakushukuru Mhe. Ahmada Yahya kwa mchango wako, sasa naomba nimwite Mhe. Hassan Khamis, lakini kabla ya Mhe. Hassan yeye aliniomba dakika tano na kuna Mhe. Masoud Abrahman Masoud na Mhe. Suleima Makame Ali wao wote waliniomba dakika tano tano nitawapatia hizo dakika na mchangiaji wetu wa mwisho Mhe. Ali Khamis Bakari na baadae nitawapa nafasi Waheshimiwa Mawaziri ambao wametaka kuchangia ripoti hii. Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kwa kunipa fursa hii, lakini ukumbuke kwamba leo tunachangia katika ofisi mbili kubwa katika nchi hii, Ofisi ya Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Hizo ndizo ofisi mbili kubwa katika nchi hii zinazoweka *image* ya nchi, heshima ya nchi, zinazolinda na kutetea Mapinduzi Matukufu ya Januari, 1964 kwa niaba ya wakwezi na wakulima.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuiongoza nchi kwa hekima na busara na kuleta maendeleo

yanayofaa kwa Wazanzibari, kwa manufaa ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 yenye lengo la kuwaletea maendeleo wakwezi na wakulima.

Pili, napenda kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa kufanya kazi nzuri za kuleta maendeleo na kusimamia na kufanya shughuli zote za serikali. Tatu, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza waziri katika ofisi zote mbili hasa Ofisi ya Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kadhalika kumpongeza Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu Ndugu Salum Maulid Salum kwa kufanya kazi nzuri katika Ofisi ya Rais Ikulu.

Pia napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza watendaji wote wa Ofisi ya Rais Ikulu akiwemo Katibu Mkuu, Katibu wa Rais, Naibu Katibu wa Rais na wengine wote Wakurugenzi na kadhalika kwa kufanya kazi nzuri pale Ikulu. Leo hii Ikulu ikabakia kuwa Ikulu pahala patakatifu, bila ya wao mimi naamini pale pasingekuwa kuendelea na hadhi yake ya kuwa ni pahala patakatifu. Mhe. Mwenyekiti, kila mtu anajua nchi hii kama Ikulu ni pahala patakatifu kwa kazi nzuri inayofanywa na viongozi hao.

Mhe. Mwenyekiti, pili napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Rais kwa kutembelea Falme za Kiarabu *UUE* na kupata mapokezi makubwa yenye hadhi ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, alivyopokelewa kwa hoi hoi na vifijo. Vyote tumeviona na tumejua kama Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ameingia nchi za Kiarabu na amepokelewa kwa mapokezi ya aina yake. Tumeyaona sote na tumeyashuhudia.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nataka kuwaambia wale wote wanaosema Rais akienda nje hapokelewi, leo wameona mitandao yote imeonesha, televisheni zote zimeonesha jinsi Rais alivyopokelewa. Hii inathibitisha wazi kwamba Rais wetu kila

mtu anamjua na kwa sababu ya kazi yake anayoifanya, anafanya kazi nzuri katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar wakwezi na wakulima. Sasa wale wanaosema hivyo mimi nawaambia lile neno la kileo walie tu, sisi tunaendelea kujenga nchi, tunaendelea kuwaletea maendeleo wananchi, tunaendelea kuyalinda na kuyatetea Mapinduzi Matukufu ya Januari, 1964.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo napenda kuipongeza Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa pale Ikulu kwa kazi nzuri inayoifanya kwa uratibu wa Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi. Lakini kadhalika Mheshimiwa napenda kuzipongeza idara zote zinazofanya kazi pale Ikulu hasa Idara ya Utumishi pamoja na Idara ya Mawasiliano Ikulu kwa kazi nzuri inayofanya ya kuweka *image* ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Pia Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Ikulu kwa kufanya kazi nzuri ya kuiweka Ikulu hadhi yake ya Ikulu. Kuna Mwakilishi mmoja wa Baraza la Nane lililopita alisema, 'kama utakwenda kwa mganga utaambiwa upeleke nzi wa Ikulu unaweza ukamkosa, kwa sababu pale Ikulu usafi umetakasika", unaweza ukamkosa kwa sababu ya hali ya usafi wa Ikulu. Kwa hivyo, napenda sana kupongeza kazi hii, lakini kazi hii yote kwa sababu ya uweledi wa Katibu Mkuu na kufanya kazi nzuri ya ukatibu mkuu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunatambua nini Ikulu, lakini pia nilikuwa nachukua fursa hii kwa vile Ikulu ni pahala patakatifu basi wale watumishi wa pale natumai wote ni watakatifu, kwa sababu wanafanya kazi pahali patakatifu. Ningewaombea basi watumishi wa Ikulu kwa sababu ni watakatifu, wanafanya pahali patakatifu, si vibaya yale maposho yao yakawa matakatifu, kama walikuwa wanalipwa hivi yaongezewe zaidi ili waweze kuendelea kuweka *image* ya pale pahala patakatifu.

Kadhalika nilikuwa napenda wale watumishi wa Ikulu kama walikuwa wanapewa fomu mara mbili za kuvaa wapewe mara nne, kwa sababu ya kufanya kazi pahala patakatifu waendelee kulinda *image* ya pahala patakatifu.

Mhe. Mwenyekiti, hata watumishi wa Ikulu waongezewe vipando madereva wote, watumishi wote wapewe vespa au gari ili waendelee kuweka *image* ya Ikulu kwa sababu ni pahala patakatifu. Mheshimiwa kuhusu Ikulu pahala patakatifu si maneno yangu ni maneno ya Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alisema, Ikulu ni pahala patakatifu sio pahala pakuchezea. Kwa maana hiyo, mfanyakazi wa Ikulu, kila mtu wa Ikulu ni mtakatifu kwa sababu anafanya kazi katika mahala patakatifu. Wako wengi wanaoitamani Ikulu hata kuingia na mpaka anafika anakufa hajawahi kuingia, wapo wengi wanaoitamani Ikulu hata kufanya kazi wakae tu katika kile kiti cha Rais lakini mpaka leo hawajaweza kukaa na wanakufa hawajaweza kukaa na hawatokaa milele daima, ujue jinsi gani Ikulu ni pahala patakatifu ndio maana wako watu wanahangaika, wanataabika, wanalia wanaitaka Ikulu lakini alivyoona mtu mmoja yaguju pale hataingia.

Mhe. Mwenyekiti, Ikulu ni pahala patakatifu naomba sana pale wale watumishi wake wapewe motisha.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakwenda katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, namjua kaka yangu Mhe. Mohamed Aboud Mohamed anafanya kazi nzuri Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Makatibu Wakuu kwa kufanya kazi nzuri. Mwenyezi Mungu awajaalie hivyo hivyo, tunasema humu Barazani bila ya *senator* Baraza halijakamilika kwa sababu pale linaposhinda tunamjua *senator* mwenyewe ndio anaingia uwanjani anaweza kutuliza ile hali inayoweza kutokezea.

Mwenyezi Mungu amjaalie na moyo huo huo wa kuwa mwanasiasa bora katika Baraza hili, katika mawaziri tunamjua Mhe. Mohamed Aboud Mohamed yeye ndiye waziri bora kwa sababu inapotokea hali ya mtafaruku kina Mhe. Abdalla Maulid Diwani wanapoanza unaona jinsi gani Mhe. Waziri anaweza kutuliza ile hali ya mtafaruku, kwa sababu ya alivyoweza kushiba siasa na kujua nini siasa katika kuitumikia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwatetea wakwezi na wakulima wana Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo napenda kumpongeza sana dada yangu katika Tume ya Kitaifa ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya inayoongozwa na dada yangu *ACP*, *Assistant Commissioner* dada yangu Kheriyangu Mgeni kwa kufanya kazi nzuri. Leo kuna watu nchi hii wanautafuta unga umekuwa tabu kidogo, unapatikana inasemekana lakini umekuwa tabu kwa kazi nzuri anayoifanya *ACP* dada yangu Kheriyangu namuomba aendelee hivyo hivyo tuhakikishe kwamba unga nchi hii utabakia usiingie kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana, najua taa yako umewasha, Tume ya Uchaguzi ambayo iko chini ya wizara hii. Tume ya Uchaguzi sote kama si hiyo kufanya kazi yake kwa umahiri na umakini tusingekuwa humu, lakini tumo humu kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kujua kazi zake na kufanya kazi kwa umahiri na umakini na tunashukuru. Nachukua nafasi hii tena kumpongeza kaka yetu, mzee wetu, baba yetu Mhe. Jecha Salum Jecha kwa kufanya kazi nzuri ya kutufanya sote tuwe humu leo tunayalinda Mapinduzi, tunayatetea, tunayaimarisha, tunayadumisha kwa niaba ya wakwezi na wakulima.

Mhe. Mwenyekiti, kadhalika napenda kumpongeza sana ndugu yangu Salum Kasim Ali kwa kufanya kazi nzuri maarufu anaitwa Mtoto wa Jecha kwa kufanya kazi nzuri.

Baada ya hayo machache napenda kuchukua fursa hii Mhe. Mwenyekiti, kadhalika na wengi hasa *TASAF*. Idara ya *TASAF* wanafanya kazi nzuri ndugu yangu Haroub kafiwa na mzee wake Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema kwa kazi nzuri anayoifanya.

Kadhalika naomba kuchukua fursa hii Mhe. Mwenyekiti, kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya dakika nane badala ya tano kwa kuyalinda na kuyatetea Mapinduzi ili wananchi wapate kusikia.

Baada hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Hassan Khamis Hafidh kwa mchango. Sasa naomba nimwite Mhe. Masoud Abrahman Masoud, Waheshimiwa mlioniomba dakika tano nawaomba sana ziwe tano za kweli kweli, isiwe kama Mhe. Hassan Khamis Hafidh kaomba tano ameachiwa nane.

Kwa hiyo, nakuombeni sana zile basi mzitumie ziwe halali tano. Kwa hiyo, Mhe. Masoud Abrahaman Masoud atafuatiwa na Mhe. Suleiman Ali na Mhe. Ali Khamis Bakar ajiandae.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia jioni hii kuingia tena kwenye kikao hichi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake mzuri.
Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Afisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa kazi yao nzuri ambayo wameifanya.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukuwe nafasi zaidi ya kumshukuru Mhe. Balozi Seif Ali Idd kwa kazi nzuri ambayo anaisimamia kwenye utekelezaji wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niende ukurasa namba 9 Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa. Mhe. Mwenyekiti, ndani ya jimbo langu mwaka jana kulitokea maafa makubwa baada ya kunyesha mvua tuliokuwa hatukutegemea kama itanyesha. Kwa bahati nzuri nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili alifanya ziara katika eneo lile na akaona wananchi ambao wamepatwa na maafa yale.

Mhe. Balozi Seif Ali Idd alitoa agizo baadhi ya maeneo kuna nyumba za *plan* ambazo zipo karibu na njia ya maji, lakini kuna wananchi ambao wamejenga niseme ndani ya hizo njia za maji. Mhe. Balozi Seif Ali Idd alitoa amri kuwa zile nyumba zihakikishe ziandaliwa utaratibu mzuri na Idara ya Ardhi ili nyumba zile ziondoke zipunguze maafa katika eneo lile. Lakini kwa bahati mbaya nyumba zile mpaka leo zipo. Niombe sana atakapokuja Mhe. Waziri atwambie agizo lile la Mhe. Balozi Seif Ali Idd limefanyiwa kazi au mpaka leo kwa sababu mvua zimeshapita ndio limeachiwa.

Jengine niende kwenye ukurasa wa 3 Tume ya Kitaifa ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya. Mhe. Mwenyekiti, mimi nichukuwe nafasi hii kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kazi nzuri ambayo anaifanya kama alivyosema

Mhe. Hassan Khamis Hafidh hapa sasa hivi madawa ya kulevya kwenye Mkoa wetu kidogo adimu adimu. (*Makofi*)

Lakini niombe sana hapa mjini ni adimu lakini wajanja sasa wameelekea vijijini. Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Mkuu wa Mkoa Makamanda wa Polisi wa Wilaya wakafanye kazi kwenye maeneo ya vijijini ili madawa ya kulevya katika visiwa vyetu yaweze kuondoka.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nililotaka kuchangia ni Idara ya Utumishi suala la ajira. Suala la ajira Mhe. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kwa Zanzibar ni tatizo kubwa sana inapotangazwa nafasi za kazi mia moja, wanaokwenda kuomba kuajiriwa pale karibu elfu moja na nafasi zenyewe ni mia moja.

Ninachokiomba kwa Tume ya Utumishi wanapokaa kujadili na kupunguza yale majina kwa awamu ya kwanza na wakatoa kwenye magazeti wananchi huwa wanapata taarifa. Lakini kwa awamu wa pili inakuwa taarifa haziopatikani vizuri. Mwisho wa siku unakwenda kuwakuta watoto wa viongozi ndio wanaoajiriwa, kuna watoto wetu wa wanyonge maneno ya Mhe. Hassan Khamis Hafidh ya wakwezi na wakulima ambao wako vijijini wana elimu ya Digirii, lakini Digirii yake anamaliza kwenda kuilimia mpunga. Unaowakuta kwenye maofisi sasa hivi wanajiriwa ni wale watoto wa "*Ibun Kinainatan*, *Ibun Khuzaymatan*". Kwa hiyo, tujitahidi serikali na wale wanyonge ambao wamesoma na wana elimu wa Digirii zinapotaka nafasi Tume ya Utumishi serikali iangalie vizuri ili vijana wale nao waweze kupatiwa nafasi na wafaidi matunda ya Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine Idara ya Maadhimisho ya Sheria za Kitaifa. Mhe. Mwenyekiti, wenzangu wamelizungumzia suala hili lakini na mimi nataka niliseme. Kwenye Sherehe za Mapinduzi mwaka huu baadhi ya maeneo ilikuwa kadi Waheshimiwa

Wawakilishi hatupati unakwenda kwenye shughuli unajiona mnyonge sana unakwenda kukaa kiti cha mwisho tena bahati itokezee kiongozi ambaye anakujua.

Lakini baya zaidi kwenye sherehe hizi kuna mipira ambayo inaandaliwa mechi ya mwanzo mpaka mwisho, mimi na wenzangu kina Mhe. Abdalla Maulid Diwani huwa tunashiriki siku zote na kuwa wageni rasmi kwenye mechi zile. Lakini siku ya mwisho kwenye *final* kwenye viti vya *VIP* unaondoshwa uaambiwa wewe hufai kukaa hapa.

Sasa niombe Mhe. Mwenyekiti, ikiwa *final* zile viongozi yaani Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunashiriki toka mwanzo mpaka mwisho na siku ya *final* tusiondoshwe kwenye viti kwa sababu unakuta watu hawahusiki kuja kukaa pale si viongozi lakini wana kadi na wakaa maeneo yale. Niombe sana wahusika hilo walichukulie hatua ili mara nyengine lisiweze kujirudia.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa namba 13 Idara ya Uratibu masuala ya *TASAF*. Mhe. Mwenyekiti, *TASAF* nia yake ni kuondoa umasikini kwa wananchi wetu. Lakini kwa bahati mbaya sana baadhi ya maeneo miradi ambayo Maafisa wetu wanakwenda wanaibulia pamoja na Wanashehia ndio wanaotakiwa waibue. Lakini wasimamizi wao ni wataalamu miradi mingine Mhe. Mwenyekiti, inakuwa haiwafaidishi wananchi. Mfano mradi wa kwenda kupanda miti, mti unaupanda leo baada ya miaka kumi na tano ndio unataka kuvua na nia ya serikali kuwaondoshea umasikini wananchi wetu.

Sasa niombe tu wasimamizi hawa wataalamu wasiwapeleke wananchi wetu kwenye kupanda mti ambayo baada ya miaka kumi na tano ndio unavuna. Kuna miradi mingi ambayo wananchi wakifanya watafaidika kwa haraka. Niwapongeze wale ambao wanaibua miradi ya kilimo cha Umwagiliaji maji serikali

inahimiza na miradi hiyo inafanyakazi vizuri na bado mabonde Zanzibar yapo wakulima wa Zanzibar bahati nzuri maeneo yetu ya mraba ni madogo sana. Kwa hiyo, unaweza ukawachukua watu wa Cheju ukenda nao eneo jengine na wa eneo jengine ukawapeleka eneo jengine. Kwa vile serikali ina pesa nyingi ambazo za *TASAF* tunaweza tukawasogezea umeme na watu hao wakaweza kufaidika. Kuliko ile miradi ambayo inaenda kumsababisha mtu apande mti leo baada ya miaka kumi na tano ndio anafaidika ule umasikini unakuwa haukuondoka. Kwa hiyo, niombe sana serikali kwenye hii miradi ya *TASAF* iwapeleke wananchi wetu kwenye miradi ambayo watafaidika kwa haraka sana.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru wewe kwa kunipa dakika zako tano na nimezitumia vizuri. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Masoud Abrahman Masoud Mwakilishi wa Jimbo la Bububu kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Suleiman Makame Ali na Mhe. Ali Khamis Bakar nae ajitayarishe.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Ripoti hii ya Kamati ya Viongozi Wakuu.

Mhe. Mwenyekiti, pia niipongeze Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, niipongeze Afisi ya Rais na Baraza la Mapinduzi kwa kazi kubwa wanazozifanya ili kuhakikisha wanatuletea maendeleo pamoja na wananchi kwa ujumla Zanzibar yetu hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile umenipa dakika tano nitakwenda haraka haraka ili zile dakika tano zisizidi. Mhe. Mwenyekiti, niende ukurasa wa 3 hadi ukurasa wa 4 kwenye Tume ya Kitaifa ya kuratibu na kudhibiti Madawa ya Kulevya. Mhe. Mwenyekiti,

katika changamoto namba moja wamesema "Upotevu wa vielelezo vya kesi za madawa ya kulevya katika baadhi ya kesi zinazowakabili watuhumiwa"

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimeshangaa hivi kuna vielelezo ambavyo vinapotea. Mimi Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi nikisimama katika kuchangia husimama na Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu ndio jembe Chama cha Mapinduzi ndio Chama imara. Mhe. Mwenyekiti, katika vyama vyote vya siasa hakuna chama hata kimoja kilichosema kwamba kitapambana na madawa ya kulevya isipokuwa Chama cha Mapinduzi ukurasa wa 214.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi kila siku husema na kushauri humu kwamba wale ambao wanashindwa kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi basi waondoke kwa hiari yao. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nilichokibaini tuna tabia ya kulindana lindana haiwezekani kwamba vipo vielelezo vya Madawa ya Kulevya tuambiwe kama vimepotoa hiyo haiwezekani kabisa, mimi nasema haiwezekani. Mhe. Mwenyekiti, nataka watu kama hawa wachukuliwe hatua ili kuhakikisha kwamba tunapambana na madawa ya kulevya uovu huu unaondoka Tanzania na Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende moja kwa moja hadi ukurasa wa 10 Idara ya Watu wenye Ulemavu. Mhe. Mwenyekiti, wengi waliochangia hapa waliwasemea watu wenye ulemavu na mimi naungana mkono nao kuwatetea na kuwasemea watu wenye ulemavu, kwa sababu watu wenye ulemavu Mhe. Mwenyekiti, niseme labda kama hawathamini hivi wanaonekana kwamba yale maradhi ni ya kurithi yale matatizo. Mhe. Mwenyekiti, ulemavu si maradhi ya kurithi ni mambo ya kawaida na yoyote yanamtokezea huenda ukawa mzima na ukapata ulemavu.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, niiimbe sana Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais inayoshughulikia watu wenye ulemavu kuhakikisha watu wenye ulemavu nao wanathaminiwa wanaonekana kama na wao ni watu wana haki katika jamii na kupewa kile chote ambacho kwamba wanastahiki.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende ukurasa wa 13 Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali za Muungano. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze sana *TASAF* kwa kuhakikisha kwamba wanawaletea maendeleo wananchi. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya kupongeza hivyo katika Jimbo langu Shehia ya Ndagoni wananchi wapatao zaidi ya mia tatu na ilikuwa wameshakata tamaa kukosa na kulimo cha mpunga ilikuwa mpunga wanausikia tu katika redio. Lakini Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa ulipokuja mradi huu wa kudhibiti maji chumvi nashukuru kwamba wakulima wale wamefarijika na wanaendelea vizuri katika mradi huo.

Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana *TASAF* kuhakikisha kwamba na zile Shehia ambazo kwanza hazijafikiwa kama mfano Michungwani na Shehia nyengine Wesha katika Jimbo langu na Shehia nyengine hata kwa Mhe. Khadija Kibano Mtambwe kule basi kama hawajafikiwa basi wafikiwe kwa sababu ni jambo muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende ukurasa wa 14 changamoto za usimamizi wa miradi ya *TASAF*. Mhe. Mwenyekiti, ukurasa huu wamesema baadhi ya Masheha wanapostaafu hushindwa kurejesha vifaa hivyo ambavyo vile vinavyotolewa katika *TASAF*. Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kwamba sikustaafu tu hawa Masheha baadhi ya Masheha wengine, wengine wazuri lakini baadhi ya wengine Mhe. Mwenyekiti, ipo haja ya kuchunguzwa kwamba hivi vifaa

vinapelekwa kwa lengo jema nia nzuri lakini Masheha hawa huchukuwa na kuvifanyia unyemela unyemela kuviuza.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, niiombe sana Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuhakikisha kwamba hawa walioleta mradi huu wanatuthamini basi ni kuwaunga mkono kuhakikisha kwamba wale wote wanaokwenda kinyume kama inavyotakikana wachukuliwe hatua za kisheria. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru naunga mkono. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Suleiman Makame Ali wa Jimbo la Ziwani kwa mchango. Mchangiaji wetu wa mwisho Waheshimiwa Wajumbe Wawakilishi namwita Mhe. Ali Khamis Bakar nae dakika tano.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi japo mchangiaji wa mwisho katika Wajumbe kuweza kuchangia Ripoti ya Kamati ya Viongozi Wakuu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi niipongeze wizara kwa kazi nzuri walioifanya kuweza kutoa mashirikiano juu ya kamati hii ambayo ilifika mbele yao ili kutoa taarifa inavyopasa ili kuweza kuwasaidia wana kamati hawa kuweza kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa ulinambia kuwa dakika zangu ni tano naomba niende haraka haraka. Kwanza niwapongeze wenzangu wote ambao walishaichangia ripoti hii kwa ufanisi mzuri ambao wameutaja. Lakini niende haraka haraka nianze katika Tume ya Kitaifa ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, sehemu kwa kweli kila mtu kaigusa kuona kwamba Madawa ya Kulevya ndio jambo ambalo ni janga kuu la taifa kuona kwamba kuna vijana wetu wengi bado ukiangalia katika mitaa yetu wanasinzia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme kwamba kwa kweli nitoe mfano serikali najua imechukua jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba jambo hili linaondoka tumetunga sheria, tukaeka kanuni na kuziba mianya yote lakini bado jambo hili ni kubwa na naiomba serikali iendelee kuchukua jitihada za makusudi ili kuhakikisha kwamba jambo hili linaondoka ili vijana waendelee kuwa salama.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, mie nikitoa mfano kwamba hutokezea kipindi cha mvua kama hizi ambazo zinakuja za masika watu wanapigiwa karantini ya ulaji wa vyakula ovyo ovyo kwa mambo ya vinywaji na mambo mengine. Lakini tunashuhudia kwamba tayari watu wanaichukua karantini ile na wanakuwa wasikivu. Lakini bado kwenye masuala ya madawa ya kulevya kwa kweli sijui ni sehemu gani ambayo kuna mianya ambayo inapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kwamba bado serikali ingali na kazi kubwa lakini sote tukiwa *mas-uli* naomba *Inshaallah* tutahakikisha kwamba tunasaidiana juu ya serikali yetu kuona kwamba mambo haya yanaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, nikondoka hapo niende kwenye ukurasa wa 14 katika sehemu ya *TASAF*. Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba miongoni mwa changamoto ambazo zimetajwa hapa kutokuwepo kwa taarifa za walengwa wa miradi wanapohama katika maeneo yao. Hapa imeelezwa kuhusiana na masuala ya Masheha. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna baadhi ya Masheha hawatoi taarifa vizuri pale ambapo watu wao wameondoka na miradi hii inabakia kuwa haiwafikii wale walengwa na kwa sababu ya kwamba taarifa imeeleza ni kwamba hawa waliokwenda watu katika kuangalia hizi taarifa waliona hili jambo lipo na ni kweli kwamba kuna baadhi ya Masheha hawatoi ushirikiano mzuri.

Niiombe tu wizara pamoja na serikali kwamba itoe muamko na maelezo mazuri juu ya hawa Masheha na kuwapa darasa pamoja na elimu kwamba jamani ile sehemu watu wanapohama wapewe taarifa vizuri kwamba jamani mimi nimehama. Lakini vile vile Masheha na wao kuwe na sehemu ya kuwa kila baada ya wiki wafanye utafiti kujua nani na nani kaondoka ili zile taarifa zifikie katika sehemu husika.

Lakini vile vile uwepo kwa Kaya masikini ambazo hazijafikiwa na mpango kutokana na upungufu wa Raslimali Fedha. Ni kweli Mhe. Mwenyekiti, kwamba hapa miongoni mwa changamoto ambazo zimetajwa kuwa kuna baadhi ya Kaya masikini ambazo bado mpaka leo hazipata pesa ni kweli pamoja na kwamba serikali yetu bado uchumi wake ni kama tunavyouona. Lakini naiomba serikali kwamba iwaangalie mimi katika Jimbo langu la Tumbe bado kuna wana Kaya masikini ambao mpaka leo mpango huu haujawafikia.

Mhe. Mwenyekiti, nikindoka hapo nije katika Afisi ya Faragha ya Rais wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, hapa kumetajwa changamoto kwa kusema ukweli changamoto hii ukiiangalia imeeleza hapa kuwepo kwa athari kubwa za mmong'onyoko wa ardhi karibuni katika nyumba zote kwa mfano wameeleza nyumba ya Migombani, Kibweni, Bwefumu, Mkokotoni kwa Unguja na kwa kule Pemba wamesema Mkoani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa nataka niseme kwamba imenifanya kidogo nipate hofu. Mhe. Mwenyekiti, hili ni jengo zuri tena la Rais leo utaangalia kwamba miongoni mwetu sie nyumba zetu tu ukiambiwa zinavuja basi unakaa na wasiwasi, je, leo nyumba ya Rais kama hii unaambiwa kwamba kuna mmong'onyoko wa ardhi kwa kweli ni jambo ambalo halipendezi. Naomba sana serikali iangalie jambo hili ili kuweza kunusuru maeneo haya ambayo ni

mazuri na ni ya Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, nikimalizia kwanza nimpongeze Mhe. Machano Othman Said japo kama simuoni kwa kulizungumzia suala la Mifuko ya Jimbo. Mhe. Mwenyekiti, kila mmoja kaligusia kwa upande wake. Lakini mimi nataka niseme kwamba naipongeza serikali kwa kuweza kutoa hizi fedha kwa ajili ya kusaidia majimbo yetu kuondoa kero baadhi ya changamoto zilizomo katika majimbo.

Lakini bado Mhe. Mwenyekiti, fedha hizi mimi naiomba serikali iziengezee kwa sababu bado miradi yetu tunayofanya ukiiangalia fedha milioni ishirini si ndogo ukiitaja. Lakini unapoifanyia kazi Mhe. Mwenyekiti, unaweza ukanunua mabati mia tu ukaja kuangalia umekosa misumari. Kwa hiyo, naiomba wizara pamoja na serikali jambo hili wakae waliangalie kwa kina vile vile fedha hizi ziongezwe baada ya milioni ishirini angalau ziwe ishirini na tano.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako. Washimiwa Wajumbe sasa naomba nimpe nafasi Mhe. Said Soud Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum atafuatiwa na Mhe. Dkt Sira Ubwa Mamboya, Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum na baadae nitampisha Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohammed Aboud Mohammed. Lakini niikumbushe serikali kwamba hoja au majibu ya hoja hii ya kamati iliyotolewa hapa ni mwezi wa 9 ndio majibu yake hasa. Kwa hivyo, kama kuna baadhi ya hoja ambazo mnahisi zitatolewa ufafanuzi ndio hizo zitolewe ambazo zimeshafanyika. Mhe. Said Soud.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kweli leo ni siku ambayo tunachukua nafasi ya kuwaambia wale ambao kwa makusudi hawajui jinsi gani serikali ya Dkt. Ali Mohammed Shein inavyofanyakazi. Kwa sababu ripoti hii ambayo inasema Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi, ripoti hii hata ikichapishwa kwenye magazeti ikatolewa ili ikasomwa na wananchi basi pia sio jambo baya. Lakini ninachotaka kusema tu ni kwamba Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kujali sana Katiba ya Zanzibar. Rais wa Zanzibar anaithamini sana Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na anafanyakazi kwa mujibu wa katiba inavyomuelekeza. Kwa misingi hiyo ndio mambo ambayo kwa haraka nimeona iko haja niyaeleze ili wananchi wa Zanzibar waweze kuyaona.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais kwanza anathamini kwa nguvu zake zote ilani ya Chama cha Mapinduzi, chama ambacho kinatawala katika nchi hii na yale yote yaliyoelekezwa katika ilani ni maslahi ya Wazanzibar, ili waweze kufaidika na uongozi wa Chama cha Mapinduzi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais wa Zanzibar amekuwa akithamini sana utawala bora, utawala ambao umetoa haki kwa watu wote wa Zanzibar kwa mujibu wa katiba. Jambo ambalo si nchi nyingi zinazothamini katiba au utawala bora. Lakini unapoona pahala pana watu wanaongozwa kwa katiba na sheria, basi pahala hapo panakuwa na utawala bora. Sasa Dkt. Ali Mohammed Shein anasimamia utawala bora. Katika mazingira ambayo yamefanya kuwa na utawala bora katika nchi yetu watu wanaishi kwa amani na utulivu. Katika hali kama hiyo pia Rais wa Zanzibar amefika

pahala anathamini demokrasia ya vyama vingi katika nchi hii, amechukua nafasi ya kuthamini demokrasia na anaifanyia kazi demokrasia, katika mazingira ya kuthamini vyama vya siasa katika nchi hii. Siku zote anakuwa mstari wa mbele kulinda misingi ya demokrasia, ili iweze kufanyakazi kwa umakini kabisa katika nchi yetu.

Kwa vile sisi ambao kwa bahati nzuri tumeingia katika Baraza hili la Wawakilishi kwa misingi ya demokrasia, tunachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar kwa maamuzi yake. Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein amekuwa mstari wa mbele katika mazingira ya kulinda na kuheshimu huduma za jamii. Huduma za jamii katika nchi yetu zimeweza kupata nafasi kubwa sana na zimetanuka katika mazingira mbali mbali. Ukienda katika mazingira ya afya, ukienda katika mazingira ya maji, ukienda katika mazingira ya umeme. Yaani mimi nataka niseme hasa kwamba visiwa kama Fundo kule Pemba, dunia ingemaliza lakini umeme usingekwenda pale.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nazungumza kwa uhakika kabisa. Mimi ni mzaliwa wa Pemba na Pemba naielewa, Fundo nakujua. Lakini nataka niseme kwamba dunia ingemaliza hii lakini Fundo umeme usingekwenda. Lakini kutokana na uongozi wake bora uliojaa busara na hekima kwa Wazanzibari basi leo Fundo wana umeme wa uhakika. Maana nataka niwaambie kwamba watu wa kisiwa cha Pemba sasa hivi kwa pamoja basi hawana tatizo la umeme hata ile nusu saa haifiki umeme unarudi, haya ni mazingira mazuri yaliyoletwa na uongozi wake katika mazingira ya kusimamia Katiba ya Zanzibar na Wazanzibari wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, Dkt. Ali Mohammed Shein ameimarisha mashirikiano ya kimataifa, watu wengi walikuwa wanajaribu kuleta lugha za aina mbali mbali, hasa wakiona Wazungu wamekuja hapa wanajaribu kuleta lugha za ajabu, kwamba wale

wamekuja kuna mabadiliko kesho au keshokutwa, kumbe Wazungu wamekuja kwa mazingira ya kuendeleza utalii, kudumisha mashirikiano na kuendeleza hali halisi ya dunia kwa ufupi. Mashirikiano ya Kimataifa yameweza kutufikisha, Rais amefungua uwanja wa kusafiri na kusafirisha mawaziri wake mara kwa mara kwenda katika nchi mbali mbali ili katika yale mazingira ya kuijengea Zanzibar uwezo. Hata yeye mwenyewe tumeshuhudia alipokwenda hivi karibuni katika ziara yake ya Falme za Kiarabu, jinsi gani alivyopokewa, sio Marais wa Afrika wengi wanaopata mapokezi kama yale. Yale ni mapokezi ya Wazanzibari kutokana na uongozi wake na ustahamilivu wake na ushujaa wake wa kusimamia demokrasia.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein amani na utulivu alioisimamia Zanzibar ni wa aina yake. Nchi kama hii ambayo watu walikwishazoea asubuhi, jioni, mchana saa sita kila wakati wanapeana *drip* mpaka *drip* nyengine hazina maana, maana hata ukimpiga ng'ombe anaanguka. Lakini amani imetawala leo, watu wanakwenda mashariki na magharibi na wanafanya kazi zao bila ya bughudha na *drip* zimekauka, maana ile mipira haitoi tena na hata ukiitundika haitoi tena hata ukiitundika haiteremki. Hii ni misingi ya ushujaa wake aliokuwa nao katika uvumilivu wa kisiasa, yaani *tolerance* aliyonayo ni ya aina yake.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein ameshuhudiwa na watu mbali mbali katika kuvumilia, yaani anavumilia mpaka dakika ya mwisho, lakini katika mazingira ya kuifanya Zanzibar watu waishi kwa amani, nampongeza sana Mhe. Rais.

Mhe. Mwenyekiti, hatua aliyoichukua Dkt. Ali Mohammed Shein katika kuimarisha umoja wa Wazanzibari ni jambo kubwa sana, kwa sababu hapa katika ulikwishatokea mpasuko kati ya

Wapemba na Waunguja. Lakini Dkt. Ali Mohammed Shein kwa uvumilivu wake na ushujaa wake, amerudisha ile hali ya kuwafanya Wapemba na Waunguja wawe kitu kimoja na hili tunajivunia kwamba tuko kitu kimoja na tutaendelea kuwa wamoja, chini ya uongozi wake na chini ya uongozi wa Chama cha Mapinduzi, kwa sababu ndio chama pekee kilicho na mamlaka sasa hivi ya kuongoza dola. Kwa maana hiyo nataka niseme kwamba ukiwa na askari, ukiwa na dola basi una uwezo wa kupambana na mambo yote, kapambana hata na wauza unga na madawa ya kulevya, maana una dola.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii pia kusema kwamba thamani ya Dkt. Ali Mohammed Shein kwa wazee wa Zanzibar ni wa aina yake, maana amefika pahala kila mzazi anayefika miaka 70 basi anapata pencheni ya shilingi 20,000/- na nina imani sio muda mrefu pencheni hiyo itaongezwa. Ni jambo la kujivunia, sio nchi nyingi za dunia zenye uwezo huo, lakini yeye pamoja na unyonge wetu tulionao ameweza kulifanya hilo, la kwamba leo mtu anapata shilingi 20,000/- na watu wengi tuna wajukuu wenye uwezo, lakini hakupi mjukuu wako shilingi 20,000/-, lakini Dkt. Ali Mohammed Shein anagawa shilingi 20,000/- zaidi ya shilingi bilioni 7 zinapotea, hili ni jambo la kujivunia Wazanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein ameweza kuthamini jitihada za vijana juu ya michezo na ameboresha sekta ya michezo, ndio maana leo tunafika pahala tunajivunia kwamba tuna wanamichezo ambao wanaweza kuiletea heshima Zanzibar, na imeletewa heshima Zanzibar, huu ni usimamizi wake na uongozi wake wa busara.

Mhe. Mwenyekiti, thamani ya Rais wa Zanzibar kwa wakulima na wafugaji

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, naomba umalizie kwa mujibu wa kanuni zetu 108(14)(15) za kanuni za kudumu. Kwa hivyo, ulikuwa uchangie baadae ripoti za kamati zinaletwa mwezi Februari. Kwa maana hiyo nilikuwa naomba sana kama nilivyosema mwanzo Waheshimiwa Mawaziri au serikali kwa jumla, kinachotakiwa hapa ni kuchangia, kwa hivyo majibu yatakuja mwezi wa tisa. Kwa hivyo, naomba sana ili niweze kumpa nafasi Mwenyekiti wa Kamati kutokana na muda wetu, nawaomba sana Waheshimiwa Mawaziri au serikali kwa jumla. Kwa hivyo, naomba umalizie ili tuwape nafasi na mawaziri wengine mheshimiwa.

Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. Lakini nilikuwa nachukua nafasi hii kuwaambia watu waliokuwa hawajui jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, wako wengi sana huko nje, wanaotusikiliza na wale wanaojaribu kukejeli. Sasa mimi singojei CCM wakajisifu, nawasifu mimi CCM, maana nawasifu mimi sasa, kama kuna mtu ana lugha ya kujibu basi anijibu mimi kwa sababu mimi ndio namuona Dkt. Ali Mohammed Shein na uongozi wake. Ndio maana nikachukua nafasi hii kuwaambia hao wapinzani wenzetu kwamba hali iko hivi.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii pia kusema kwamba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Makamu mwenyewe wa Pili wa Rais, amekuwa mstari wa mbele katika harakati za kuleta umoja wa Wazanzibari katika maafa yote yanayotokea, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais halali usiku wala mchana kwa mazingira ya kupambana na maafa ya nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa dakika moja nitamalizia. Kimsingi ni kwamba ameweza kupambana na mazingira ya madawa ya kulevya, ameweza kupambana na watu wa *sober*. Namuomba

Mhe. Makamu wa Pili aongeze bidii katika majumba ya *sober*, hata wale watu wanaosema kesho, keshokutwa, mwezi ujao wapelekwe *sober* ili wakapumzike pale kwa sababu wana matatizo ya akili. Sasa wakitulia inawezekana kidogo wakajua nini kinachoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, umenikatisha sana. Lakini mimi nataka niseme nakushukuru sana Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Dkt. Sira Ubwa Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum, na baadae Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa dakika chache tu, na mwisho nitampa nafasi Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ili tuweze kumpa nafasi Mwenyekiti wa Kamati na yeye amalizie.

Mhe. Sira Ubwa Mamboya (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa na mimi fursa hii. Mimi sina mengi nitatumia muda wangu vizuri kwa kutoa pongezi zangu kwanza kwa kamati, kwa ripoti nzuri waliyotuwasilishia ambayo imetafakari mengi na mengi yaliyomo katika maoni yao, ushauri wao na maagizo yao ni ya kujenga na wala sio kuilaumu serikali. Nimejaribu kuipitia ripoti hii tangu mwanzo mpaka mwisho, nikakuta kwamba mambo makubwa yaliyokuwa yametokea humu ni mambo ambayo yakutupa maelekezo ya kutaka tufanye vizuri kama serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano, kama kunakamatwa dawa za kulevya basi tuhakikishe kweli zinawekwa katika utaratibu mzuri na wasije wakapewa taarifa kwamba hazipo, takwimu zina umuhimu wake na bila ya takwimu sahihi basi hatuwezi kuwa na maendeleo kwa takwimu za kughushi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile wamezungumzia ushirikishwaji. Utakapofanya jambo kwa wananchi bila ya kuwashirikisha usitegemee mafanikio. Wamezungumzia taaluma ambapo nafikiria ni muhimu kwa jambo lolote lile na hata kuna baadhi ya vipengele ambavyo wamezungumzia, tuseme kwa mfano, wamesema Shirika la Wakala la Uchapaji hawana wafanyakazi wenye taaluma na ndio maana wanapata shida ya kufanya kazi kwa uhakika na yale mambo ambayo tulikuwa tunatakiwa yafanyike, kwa hivyo yamepungukiwa na nguvu kwa sababu hiyo. Mimi nilikuwa nataka niwaambie wenzangu, tunajaribu kuwasomesha watoto wetu wengi katika taaluma za aina moja.Tujaribu tunapotaka kuwasomesha watoto tutafute mapungufu yapo wapi katika serikali, ili tukisomesha watoto wale wasipate shida ya kupata kazi, kwa sababu kuna nafasi za kazi nyengine serikalini ambazo zinakosa wasomi wa aina ile. Kwa hivyo, kama tutakwenda kusomesha hapa mambo ya uchapaji na fani zinazohusiana na hayo basi nafasi zipo. Lakini kama tutasomesha wote katika fani zile pamoja, halafu tunawakuta watoto miaka mitatu au minne hawawezi kuajirika, kwa sababu ni kwamba waliosomeshwa ni wengi na nafasi zinakuwa zimejaa na serikali inaajiri kwa mujibu wa uwezo uliokuwanao. Kwa hivyo, mimi nafikiri tufanyeni pia utafiti ili tutizame wapi kuna mapungufu na tuelekeze nguvu zetu kuwasomesha watoto wetu katika utaratibu huo.

Mhe. Mwenyekiti, pia nilikuwa nataka nizungumzie kidogo kuhusu suala la Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa. Kweli tunataka tuwe tuna mfuko na kweli tunataka tuweke pale linapotokea tuweze kulikabila kama serikali, lakini sasa serikali ina mambo mengi. Lakini hata hivyo kama kutatokea maafa huwa tunakata pua tukaunga wajihi ili kukabiliana na maafa yale. Lakini hatuwezi tukachukua pesa tukaziweka wakati kuna shida nyengine pembeni yake tunasubiri maafa wakati hatujui yatatokea lini. Kwa hivyo, serikali inalitambua hilo na pale linapotokea

tunafanya kila jitihada kuweza kuyakabili. Kwa hivyo, wasiwe na wasiwasi likitokea hilo serikali yao ipo na maafa yale yatakabiliwa na hakuna hatakayekufa kwa hilo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi pia ningependa kuishukuru sasa serikali ambayo inatekeleza haya ambayo yaliyoletwa hapa. Nataka niwaahidi Waheshimiwa Wawakilishi kwamba tumeyasoma na tumeyaona na kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu yale tutakayoweza kuyafanyia kazi basi tutahakikisha kwamba tunayafanyia kazi. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi. Vile vile nimshukuru sana Mwenyekiti wetu Mhe. Omar Seif Abeid na Wajumbe wa Kamati hii ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri na kubwa waliyoifanya.

Pia niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe waliochangia na wale waliokuwa hawakuchangia, kwa sababu wote wameridhia ripoti hii ya kamati. Mhe. Mwenyekiti, kama ulivyokwishaelezea kwamba wajibu wetu leo ni kuipokea ripoti hii na sisi kwa niaba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na serikali kwa ujumla wake tunaipokea ripoti hii, ili tukaifanyie kazi na mwezi wa Septemba kama kawaida tutaleta majibu ya kutosha na ya kuridhisha kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na wajumbe waliotangulia nitumie fursa hii kumpongeza sana Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kazi kubwa anayofanya ya kuongoza nchi yetu busara zake, hekima zake uvumilivu wake ambao umewezesha nchi yetu kuwa katika hali hii ya amani na kutuwezesha kufikia hatua kubwa ya maendeleo. Lakini pia naomba uniruhusu nimshukuru sana sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa namna anavyotuongoza hapa Barazani lakini pia

anavyotuongoza Wizarani na tukaweza kumudu kutekelea majukumu yetu.

Mhe. Mwenyekiti na Washehimiwa Wajumbe kwanza nimhakikishie Mhe. Jaku kwamba Mawaziri na watendaji wa Serikali wamekula kiapo kuisaidia Serikali kuwa waaminifu kwa Rais na watafanya hivyo, wale ambao wanaokwenda kinyume na hivyo basi kuna hatua zinachukuliwa kwa mujibu wa mwenyewe anayeteua anavyoona inafaa. Kwa hivyo nataka nimhakikishie kwamba Mawaziri wote tuko tayari kabisa kusikilia maelekezo ya Mhe. Rais ili kutekeleza wajibu ambao yeye ametaka tuutekeleze kwa mujibu alivyotutuma, nataka nikuhakikishie wewe Baraza lako tukufu na wananchi kwa jumla.

Aidha Mheshimiwa kwa sababu ya jambo moja kubwa limezungumzwa hapa linalohusu suala zima la mambo yanayoitwa kero za Muungano, Mheshimiwa haya mambo yanafanyiwa kazi vizuri na yote ambayo yalisemwa tunayapokea kwa kwenda kuyafanyia kazi hususan yale aliyoeleza sana Mhe. Hamza Hassan Juma ili tuone matatizo haya yanapata ufumbuzi muafaka, lakini niseme tu kwamba Muungano ni jambo linaloendelea kukua linaloishi kwa hivyo changamoto za hapa na pale zitatokeza, lakini wajibu wetu kama nchi kama viongozi kushirikiana kuzipatia ufumbuzi na dhamira njema ipo kwa pande zote mbili kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar ili kuondosha yale ambayo ni matatizo kwa wananchi wetu. Nakuhakikishieni kwamba tutakuja na majibu mazuri yatakayokidhi haja kama ilivyozungumzwa.

Kuhusu suala la *passport* mpya Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf alielezea yeye alitaka sana kuelewa kwa nini *passport* za amani zilikuwa zinaandikwa ulipozaliwa kama umezaliwa Pemba inaonyesha Pemba na kama umezaliwa Unguja ilikuwa inaonyesha Zanzibar kwa hivyo akataka utaratibu huo

uendelee, kilichotokea sasa ni kwamba tumekubaliana kwamba sasa pahala pa kuzaliwa ionyeshwe Wilaya uliyozaliwa na ndio maana akaona Kusini, ikitajwa Kusini ni moja tu ni ile Kusini Unguja ka mwana ya Wilaya ya Kusini Unguja haitojitokeza kusini nyengine kwa Tanzania nzima. Na yule aliyezaliwa Chake chake kama mimi *passport* yangu inaandikwa Chake Chake, na atakayezaliwa Mkoani itaonyesha Mkoani, atakayezaliwa Tumbatu itaonyesha Kaskazini (A) na kadhalika, huo ndio utaratibu ambao kwa sasa wanaonyesha kiwilaya.

Lakini wapi ilikpotolewa utaona katika kila *passport* pale na mimi nimeichukua hapa katika kila *passport* inaonyesha kabisa pameandikwa *PCO* Zanzibar, maana yake *Passport Control Office* Zanzibar. Kwa maana na hapa ameonesha Mamlaka iliotoa, kwa hivyo waliozaliwa mjini itaonyesha Wilaya ya Mjini kwa hivyo hivyo ndivyo ilivyo wamekwenda zaidi kuonesha kiwilaya na wamekwenda kuonesha ilipotolewa *passport*. Lakini kwa upande wa picha Mhe. Nadir alisema kuna picha ya Mwalimu Nyerere tu hakuna picha ya Mzee Karume katika *passport* hii, hii picha iliyotolewa humu ilitolewa kuonesha kuashiria Muungano wetu kwa maana ya nchi mbili za Zanzibar na iliyokuwa Tanganyika zilivyoungana na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hapa Mwalimu ndio alikuwa anachanganya udongo, kwa hivyo ilitiwa hiyo kuonesha kuwa *symbol* ya Muungano wetu haikuwa na tafsiri nyengine.

Kwa hivyo naomba Mhe. Nadir na wananchi wengine na Wajumbe wa Baraza hili tukufu waridhie kwa sababu kitendo hichi kilifanyika siku ya tarehe 26 April, 1964 wakati tunasherehekea kwa mara ya kwanza sherehe za Muungano wetu na pale ndipo Mwalimu alichanganya udongo huo baada ya kusainiwa hati ya makubaliano tarehe 22 April, 1964. Kwa msingi huo niwaombe Waheshimiwa Wajumbe tukubaliane na picha hizi zilizomo na hali iliyopo katika *passport* yetu ili tuendelee

kuitumia *passport* yetu kwa dhamira ile ile ya kuimarisha muungano wetu na pale ambapo patahitajika marekebisho mengine kwa mambo mengine basi tutafanya hivyo. Lakini kwa sasa niwaombe Waheshimiwa kwamba *passport* yetu hii imekidhi vigezo vya kitaifa na kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, mambo yaliyoelezwa ni mengi lakini nataka niseme moja kubwa hapa ambalo limezungumzwa sana kuhusu madawa ya kulevya, nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba kazi kubwa ya kupambana na madawa ya kulevya imefanyika na matokeo yake hata kupatikana kwake sasa madawa ya kulevya ni tabu ukilinganisha na ilivyokuwa mwanzo. Haipo kama ilivyokuwa mwanzo na pia vijana wetu wengi wameamua kupata ile dawa ya kupunguza kuhitaji madawa ya kulevya na kwa kiasi kikubwa vijana wanaongezeka katika jambo hilo na suala zima la udhibiti wenyewe wa uingiaji hatua zinachukuliwa. Kwa sababu ya muda wako Mhe. Mwenyekiti, na kwa sababu tutakuja kutoa taarifa rasmi kwenye mambo haya naomba kuwahakikishia Wajumbe kwamba haya ambayo wameyasema tutaleta majibu ya kutosha.

Kwa upande wa Eko kwa Baraza la Wawakilishi Baraza kwa kushirikiana na Serikali wanaifanya kazi hii na ipo katika hatua nzuri sasa ya kuanza rasmi ya marekebisho hayo, tayari mshauri mwelekezi ameteuliwa na sasa anatengeneza kujua gharama ni kiasi gani ili kazi ianze ya matengenezo na sote tuweze kupata sauti ya kusiklizana humu ndani, kila mmoja jambo hili linamvunja moyo sana.

Basi baada ya maelezo hayo kwa heshima na taadhima naunga mkono ripoti hii nakuhakikishia kwamba ushauri uliotolewa tutaufanyia kazi na pale penye changamoto tutazirekebisha ili tuendeleze kutenda vizuri majukumu yetu katika Serikali ya kuwatumikia wananchi kwa unyenyekevu mkubwa na aweze

kupiga hatua ya maendeleo katika nchi yetu. Baada ya maelezo hayo nakushuru sana Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante na mimi nakushukuru Mhe. Waziri wa Nchi sasa naomba nimpishe Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pili kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kuweza kunipatia nafasi nami kuweza kutoa mchango wangu katika uwasilishwaji wa taafira hii ya kamati. Kwanza kabisa sina budi kumshukuru kwa dhati Dkt. Ali Mohammed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa imani yake kwangu na wenzangu aliowateua waliokaa mstari wa mbele. Lakini pili kwa namna ya kipekee ambavyo amekuwa akituongoza na akiongoza nchi yetu katika kuimarisha amani, umoja na mshikamano. Tumuombe Mwenyezi Mungu amjaalie kuendelea kuwa na afya njema ili anayoyatenda kwa faida ya nchi yetu tuendelee kuya-*enjoy* sote tuliopo hapa na wenzetu walioko nje.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa ya kamati tumeisikia na wenzetu waliochangia tumewasikia na wote kwa ujumla inaonekana wazi kwamba tumeridhika na taarifa ya kamati hii, na sisi kama Serikali Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi nasi tunaunga mkono taarifa hii, lakini kuna mambo mawili kwa matatu ambayo yamesemwa na wajumbe wengi nadhani Mhe. Mwenyekiti, naweza kuyachangia katika kuwapa utaratibu na mwongozo mzuri zaidi ili kuweza kuona kwa kiasi gani hisia na mawazo yao sisi Serikali tumeweza kuyapokea na itafika wakati tutakuja kutoa majibu ya ukamilifu wake.

Mhe. Mwenyekiti, michango pamoja na taarifa imezungumzia baadhi ya mmong'onyoko na uharibifu wa maeneo ya jengo la Ikulu niwahakikishie tu Waheshimiwa Wajumbe kwamba kabla ya majibu ya mwezi wa tisa, hatua zimeanza kuchukuliwa na itakapofika mwezi wa tisa tutaelezea ukamilifu hatua ambazo tumeweza kuzichukua. Tunachowathibitishia kwamba tutayalinda majengo haya yataendelea kubaki salama na yataendelea kuwa mazuri na yatazidi kung'ara na kumeremeta. Usimamizi na utendaji wetu tutahakikisha kwamba majengo haya tunayaenzi kama ambavyo tunaenzi vitu vyengine ambvyo ni tunu kwa taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, la pili niithibitishie tu Kamati kwamba Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa namna yoyote ile tutaendelea kushirikiana nao ili kuweza kufanya kwa maslahi ya nchi yetu na kwa maslahi ya wananchi wetu. Niwaombe tu kila wanapohisi kwamba kuna jambo la msingi la kuweza kubadilishana mawazo kupeana michango basi wasisite sisi tuko tayari katika kushirikiana nao ili tuweze kufikia malengo tuliyoyakusudia ya kiuwatumikia wananchi wetu.

Jambo la tatu Mhe. Mwenyekiti, limezungumzwa suala la Mawasiliano niwathibitishie tu Waheshimiwa Wajumbe kwamba Mawasiliano ya taarifa za Ikulu na Serikali nayo pia yameimarishwa na yamekuwa bora zaidi, wengi wamesikia ziara ya Mhe. Rais alipokuwa katika nchi za Ghuba lakini wamesahau kwamba hata ziara za ndani zote alizofanya Mhe. Rais zinaonesha kwamba hakuna *event* yoyote ambayo anakwenda Rais ambayo haiko live katika *Social Media* tutaendelea kuimarisha mawasiliano hayo ili kuweza kuona walioko nyumbani, wanapata fursa ya kuangalia vyombo vya habari kwa maana ya kwamba redio, Televisheni na Magazei. Lakini walioko ughaibuni wanaweza kupata *accesse* kumuona Mhe. Rais kazi zake anazofanya kwa kupitia njia za *Social Media.* Imani yetu kwamba

jambo hili litaendeleza ukaribu na kufikisha mawasiliano ya na taarifa kwa wananchi wetu ili kuweza kutambua Serikali kwa ujumla inafanya nini katika kuimarisha huduma walizozijenga kufikishiwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa katika kumalizia mchango wangu naomba tu sote wanasiasa tuliomo humu tuendelee kuhubiri amani, umoja na mshikamano ili tuweze kufikia malengo tuliyoyakusudia na hasa utekelezaji wa ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi. Tukishirikiana tukiweka amani upendo na mshikamano ni imani ya wazi kwamba tutaweza kutekeleza kwa vitendo ahadi na mkataba wetu wa Chama cha Mapinduzi kwa wananchi tunaowaongoza hapa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mhe. Omar Seif Abeid (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Vingozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Mwenyekiti, wa Baraza la Wawakilishi kwanza sina budi na mimi kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia tena kusimama hapa mbele yako na kufanya majumuisho ya ripoti ya Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2017 na 2018, lakini pia kabla ya kusoma hiyo huo muhtasari wa majumuisho yenyewe napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza kwa dhati, wale wote ambao wameichangia ripoti hii wamenionesha moyo mkubwa wameunga mkono ripoti yetu na ni imani yangu pamoja na imani ya kamati yetu kwamba Baraza limeridhika na kazi iliyofanywa na kamati hii.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba sana kuwatambua wale wote ambao wamechangia kama ifuatavyo. Mhe. Mwenyekiti, ripoti yetu imepata baraka kubwa ya kuchangiwa na wajumbe ishirini na moja wa moja kwa moja na wajumbe kumi na mbili kwa maandishi, hii ikifanya jumla ya watu wote waliochangia kwa kuzungumza moja kwa moja pamoja na maandishi kufikia wajumbe 33. Kwa hivyo kwa ruhusa yako naomba niwataje kwa mpangilio kama walivyochangia.

1. Mhe. Ali Suleiman Ali
2. Mhe. Simai Mohammed Said
3. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis
4. Mhe. Nadir Abdullatif Yussuf
5. Mhe. Machano Othman Said
6. Mhe. Hamza Hassan Juma
7. Mhe. Shehe Hamad Mattar
8. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
9. Mhe. Mohammedraza Hasanali Mohamedali
10. Mhe. Rashid Makame Shamsi
11. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
12. Mhe. Khadija Omar Kibano
13. Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil
14. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
15. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
16. Mhe. Suleiman Makame Ali
17. Mhe. Ali Khamis Bakari

Kwa upande wa Mawaziri waliochangia alikuwa ni:

1. Mhe. Said Soud Said
2. Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya
3. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
4. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Kwa upande wa Wajumbe waliochangia kwa maandishi ni:

1. Mhe. Miraji Khamis Mussa
2. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
3. Mhe. Tatu Mohammed Ussi
4. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
5. Mhe. Panya Ali Abdalla
6. Mhe. Ame Haji Ali
7. Mhe. Shaibu Said Ali
8. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
9. Mhe. Khamis Juma Maalim
10. Mhe. Mussa Ali Mussa
11. Mhe. Salha Mohammed Mwinjuma

Mhe. Mwenyekiti, karibu ya wajumbe wote waliochangia walikuwa wana sehemu ambazo zinajirudia katika maelezo yao, maelezo ya ujumla yaliyozungumzwa yalikuwa yanalenga moja kwa moja kuhusu utendaji wa Serikali ambao mimi sina haja ya kuueleza kwa sababu maelezo na majibu yatatolewa na Serikali kama walivyoahidi mwezi wa tisa, lakini ni imani yangu kwamba kutokana na ripoti tulioiwasilisha imefafanua kila kitu na Serikali ndio itakayotoa majibu na ni imani yangu kuwa majibu yao yatakuwa ya kutekelezeka.

Lakini pia Wajumbe wengi waliochangia wamejikita katika madawa ya kulevya ambayo Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ameeleza kwa kina, wameeleza uwepo wa takwimu sahihi ambayo pia majibu yake yatapatikana, wameeleza kufanyiwa matengenezo kwa Ofisi za *GSO* Waziri wa Nchi Afisi

ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ameeleza na ataeleza majibu yake siku itakapofika.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa niaba ya kamati sina la kuliongeza zaidi ya yaliyozungumzwa, kwa sababu yaliyozungumzwa ni mazuri na hayana haja ya kuyaongezea tukaja tukayaharibu tuiachie Serikali ifanye kazi yake na muda ukifika watatoa majibu.

Kwa hivyo baada ya maneno haya Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa kwa ridhaa yako kutamka kwamba natoa hoja juu ya majumuisho ya Hotuba yetu ya kamati. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa (Makofi)

Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa na imeungwa mkono sasa naomba niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mweyekiti, wanyooshe mikono wanaokataa, wanaokubali wameshinda *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaahirisha kikao chetu hichi naomba nitoe taarifa ya kuwa Waheshimiwa wote waliokuwemo humu barazani wamepewa barua ya mwaliko wa Mahafali ya *SUZA* kesho asubuhi Saa 3.00, lakini shughuli zetu za Baraza zinaendelea kwa maana hiyo watakaotakiwa

waende Mhe. Spika, na Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii inayohusiana na mambo ya elimu wao watatuwakilisha sote. Kwa upande wa Mawaziri basi na wao naona atakwenda Mhe. Waziri au taratibu zitakazofaa ili tusiathiri shughuli zetu za Baraza.

Waheshimiwa nawashukuru sana na mimi nichukue fursa hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati na Kamati yake kwa jumla kwa kuwasilisha ripoti hii, lakini pia niwashukuru wajumbe wote waliochangia na niishukuru Serikali kwa kuikubali hii ripoti na imani yetu kwamba ripoti hii itaenda kufanyiwa kazi na ifikapo mwezi wa tisa inshaallah basi majibu yatakuwa mazuri. Nawashukuru sana Wahsehimiwa Wajumbe naahiridha kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 1.22 Usiku Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 15/2/2018 Saa 3.00 asubuhi)